# HAZINA YETU

## TOLEO LA NNE 2025



# Kutoka Meza ya Katibu Mkuu

Ndugu Wasomaji,

Nawakaribisha kwa dhati katika Toleo hili maalum la Jarida la Hazina Yetu, likijumuisha taarifa na matukio muhimu yaliyojitokeza katika Robo ya mwisho ya mwaka wa fedha 2024/2025, kuanzia tarehe 1 Aprili hadi 30 Juni, 2025.

Katika kipindi hiki, Wizara ya Fedha imeendelea kutekeleza majukumu yake ya msingi kwa ustadi na dhamira ya kuhakikisha uchumi wa Taifa unaimarika. Tunajivunia kushuhudia mwenendo thabiti wa uchumi, licha ya changamoto mbalimbali za ndani na nje ya nchi.

Mfumuko wa bei uliendelea kudhibitiwa katika viwango vya kuridhisha (wastani wa 3.2), ukuaji wa Pato la Taifa uliendelea kuimarika, na hatua madhubuti zimechukuliwa kuhakikisha kunakuwa na usimamizi makini wa matumizi ya umma na mapato ya Serikali.

Kipindi hiki pia kimekuwa cha mafanikio makubwa kwa nchi yetu kimataifa, ambapo mnamo Juni 2025, Shirika la kimataifa la Fitch Ratings lilithibitisha tena hadhi ya Tanzania katika kiwango cha B+ yenye mtazamo thabiti cha uwezo wa nchi kukopesheka katika masoko ya kimataifa.

Hii ni ishara ya imani ya kimataifa juu ya uhimilivu wa Sera za kifedha na uchumi wa taifa. Tathmini hii inatoa fursa kwa nchi yetu kuendelea kupata mikopo ya gharama nafuu na kuvutia wawekezaji wa kimataifa.

Aidha, Wizara imeendelea kushiriki kikamilifu katika majadiliano ya kisera na wadau wa maendeleo, ikiwemo mikutano ya kimataifa ya majira ya kipupwe ya Benki ya Dunia na IMF, pamoja na Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Benki ya Maendeleo ya Afrika, AfDB, ambapo Tanzania ilitoa mchango wake katika mijadala ya kimataifa kuhusu mageuzi ya kifedha na maendeleo endelevu.

Kwa niaba ya Wizara ya Fedha, napenda kuwashukuru wadau wetu wote wa ndani na wa nje kwa ushirikiano wao endelevu. Tutaendelea kuwa mstari wa mbele katika kuandaa mazingira bora ya kifedha kwa maendeleo ya Taifa letu.

**Karibu usome Jarida la Hazina Yetu – Toleo la Nne, 2024/2025, linalopatikana katika mfumo njia ya nakala tete (softcopy) na nakala mango (hardcopy).**

Dkt. Natu El-maamry Mwamba,
**KATIBU MKUU**



# Kutoka Meza ya Mhariri Mkuu

Ndugu Wasomaji,

Karibu tena kwenye Toleo la Nne la Robo mwaka la Jarida la Hazina Yetu kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Kwa niaba ya timu nzima ya uhariri, nina furaha kukuletea jarida hili lenye mkusanyiko wa habari, makala, na uchambuzi wa kina kuhusu masuala mbalimbali yaliyotokea katika kipindi cha mwezi Aprili hadi Juni, kipindi ambacho kimekuwa cha shughuli nyingi, mabadiliko, na mafanikio katika nyanja mbalimbali za uchumi na fedha za umma.

Robo hii ilisheheni matukio muhimu ya kisera kama usomaji wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2025/2026 bungeni. Katika ukurasa huu wa kihistoria, tumeangazia maudhui makuu ya namna Serikali ya Awamu ya Sita, inayoongozwa na Jemedari wetu, Mhe. Dkt.Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alivyofanya kazi kubwa ya kusimamia uchumi na maendeleo ya nchi katika kipindi cha miaka yake minne ya uongozi wake, pamoja na Bajeti Kuu ya Serikali iliyopitishwa kwa kishindo na Bunge la 12, ikiwemo vipaumbele vya Taifa, mikakati ya kukusanya mapato na matumizi, pamoja na mwelekeo mpya wa kuimarisha ustawi wa wananchi.

Vilevile, Toleo hili linaangazia ushiriki wa Tanzania katika mikutano mbalimbali ya kimataifa ikiwemo Mikutano ya Kipupwe ya Benki ya Dunia na Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) iliyofanyika Washington D.C, Marekani, pamoja na Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) uliofanyika Abdjan-Ivory Coast. Kupitia ripoti maalum, tunakuletea muhtasari wa vikao, majadiliano ya kisera, na fursa zilizojitokeza kwa Tanzania kushiriki kikamilifu katika mazungumzo ya kimataifa kuhusu uchumi jumuishi, usimamizi wa madeni, na uhimilivu wa fedha za umma.

Kwa lengo la kukupa taarifa za ndani na maoni kutoka kwa viongozi waandamizi, tumeandaa mahojiano ya ana kwa ana na baadhi ya Watendaji Wakuu wa Wizara ya Fedha. Kupitia mazungumzo haya, utapata kujua maono na mafanikio ya kisera katika kusimamia uchumi wa Taifa. Viongozi hawa wametoa mitazamo yao kuhusu mageuzi ya kiutawala, matumizi ya TEHAMA katika ufanisi wa utoaji huduma, pamoja na mustakabali wa fedha za umma nchini kwa ujumla.

Aidha, tunakuletea matukio mbalimbali yaliyofanyika ndani ya Wizara ya Fedha pia tumejumuisha pia makala za kitaalamu, tafiti, na mijadala ya kisera ambayo inalenga kukujengea uelewa na kukuimarisha katika kushiriki kikamilifu katika safari ya maendeleo ya Taifa letu.

Tunakushukuru kwa kuendelea kuwa msomaji wa kudumu wa Hazina Yetu, hakika mnalifanya jarida hili kuwa jukwaa la maarifa, taarifa sahihi, na majadiliano yenye tija kwa Taifa.

Tunakaribisha maoni na mawazo kutoka kwenu, na tunawakaribisha kwa moyo mkunjufu kuendelea kufurahia, kujifunza, na kushiriki maudhui ya Toleo hili.

Soma, fahamu, shiriki kwa maendeleo ya pamoja.

Kwa Niaba ya Timu ya Uhariri



**Benny Mwaipaja**
**Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini Wizara ya Fedha**

Makala
Makala Makala Makala










# Makala

# MAFANIKIO YA MIAKA MINNE YA SERIKALI YA AWAMU YA SITA (6)



Na. Benny Mwaipaja

Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilitimiza miaka minne Machi 2025 tangu iingie madarakani mwaka 2021. Katika kipindi hicho, Serikali imefanya mambo mengi na mazuri kwa ustawi wa jamii yetu ya Tanzania.

Katika kipindi cha miaka minne ya uongozi wake, Mhe. Rais ameonesha dhahiri kuwa ni kiongozi makini, shupavu, mchapa kazi, mwadilifu, msikivu na aliye na dira thabiti ya kuendelea kuiletea nchi yetu maendeleo makubwa.

Aidha, Mheshimiwa Rais ameendelea kutekeleza miradi ya zamani na miradi mipya, miradi mikubwa na miradi midogo, miradi ya kuchochea uchumi na miradi ya huduma za jamii, kukuza demokrasia nchini na diplomasia ya uchumi.

Katika kipindi cha miaka minne ya uongozi wa Dkt. Samia Suluhu Hassan, nchi ya Tanzania imesonga mbele licha ya nchi nyingi duniani kupita kwenye misukosuko ya kiuchumi.

## (a). Mafanikio

### (a) Ukuaji wa Uchumi Shirikishi

Serikali ya Awamu ya Sita iliingia madarakani wakati dunia bado inakabiliwa na changamoto za ugongwa wa UVIKO-19. Katika kipindi hicho, kasi ya ukuaji wa uchumi ilikuwa imeshuka kutoka asilimia 7.0 mwaka 2019 hadi asilimia 4.8 mwaka 2020.

Aidha, mbali ya kuwepo kwa janga la UVIKO – 19, zilijitokeza changamoto nyingine zilizoathiri uchumi wa dunia ikiwemo Tanzania zikiwemo vita inayoendelea katika mataifa mbalimbali duniani ikiwemo vita baina ya Urusi na Ukraine pamoja na mabadiliko ya tabianchi hususani mvua kupita kiasi zilizosababisha mafuriko yaliyoleta maafa na uharibifu wa mindombinu katika maeneo mbalimbali nchini.



Pamoja na changamoto hizo, Serikali ya Awamu ya Sita iliweza kuimarisha uchumi kufikia wastani wa asilimia 5.0 kati ya mwaka 2021-2024. Kwa mwaka 2024 uchumi ulikua kwa wastani wa asilimia 5.5 ikiwa ni ongezeko la nukta ya asilimia 0.4 kutoka ukuaji wa asilimia 5.1 mwaka 2023. Ukuaji huo ulichangiwa na:

- Utekelezaji endelevu wa miradi mikubwa ya kimkakati na ya kielelezo inayohusisha miundombinu ya nishati na usafirishaji;
- Kuanza kwa uzalishaji wa umeme katika Bwawa la Kufua Umeme wa Maji la Julius Nyerere;
- Kuanza kwa usafirishaji wa abiria kupitia Reli ya Kati ya Kiwango cha Kimataifa – SGR kwa kipande cha kutoka Dar es salaam hadi Dodoma;
- Kuongezeka kwa mikopo kwa sekta binafsi iliyochachua shughuli za kiuchumi; na
- Uwekezaji wa Serikali katika kuboresha na kuleta karibu huduma za jamii, ikiwemo elimu, afya, na maji.

## (b) Mfumuko wa Bei

Katika kipindi cha mwaka 2021 ambacho Mhe. Rais aliingia madarakani, mfumuko wa bei ulikuwa wa wastani wa asilimia 3.7. Kutokana na kuvurugika kwa mnyororo wa usambazaji wa huduma na bidhaa kulikosababishwa na changamoto zilizokabili uchumi wa dunia ikiwemo mlipuko wa UVIKO 19, mabadiliko ya tabianchi pamoja na vita baina ya Urusi na Ukraine kulipelekea kuongezeka kwa bei za bidhaa na huduma hususan bidhaa za mafuta, mbolea na baadhi ya vyakula kama ngano.

Ili kuimarisha uchumi na kuwezesha wananchi kuendelea na shughuli za uzalishaji mali, Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi madhubuti wa Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, iliwezesha kutolewa kwa ruzuku ya kila mwezi kwenye bidhaa za mafuta ya petroli takribani shilingi bilioni 477.1 kwa kipindi cha miezi sita pamoja na kutoa ruzuku ya mbolea ya takribani shilingi bilioni 244.7 kwa wakulima na kuwezesha mbolea kupatikana kwa bei nafuu ambayo ilikuwa nusu ya bei ya soko.

Ruzuku iloyotolewa kwenye mbolea na pembejeo imesababisha nchi kuwa na utoshelevu wa chakula katika masoko ya ndani kwa kiwango cha asilimia 128 mwaka 2024 na hivyo kuwa na ziada ya kusambaza kwa nchi jirani.

Hakika Mhe. Rais anastahili pongezi kwa moyo wake wa kujitolea kuwatumikia wananchi wa Tanzania. Mwenendo wa mfumuko wa bei umeendelea kuwa katika wastani wa chini ya asilimia 5.0 ambapo katika kipindi cha mwaka 2024 ulifikia wastani wa asilimia 3.1, kiwango ambacho ni cha chini kabisa kuwahi kutokea katika kipindi cha zaidi ya miongo miwili.

Hii ilitokana na kuwepo kwa utekelezaji madhubuti wa sera za bajeti na fedha na uwepo wa mazao ya chakula katika masoko ya ndani na nchi jirani.

## (c) Mapato ya Ndani

Katika kipindi cha uongozi wake, mapato ya ndani yamekuwa yakiongezeka kila mwaka licha ya kuwepo kwa changamoto zilizokabili uchumi wa dunia na kuadhiri mwenendo wa bajeti na uchumi wa Tanzania. Mafanikio yaliyopatikana kwenye ukusanyaji wa mapato katika kipindi cha miaka minne ya uongozi wake yameonesha dhahiri kuwa ni kiongozi makini, mchapa kazi na aliye na dhamira ya dhati ya kuendelea kuiletea maendeleo ya Tanzania.

Katika kipindi cha mwaka 2020/21 makusanyo ya mapato ya ndani yalikuwa takribani shilingi trilioni 20.59, sawa na wastani wa shilingi trilioni 1.72 kwa mwezi. Mapato hayo yaliendelea kuongezeka mwaka hadi mwaka chini ya uongozi wa Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan katika Serikali ya Awamu ya Sita ambapo mwaka 2023/24 makusanyo ya mapato ya ndani yalifikia takribani shilingi trilioni 29.83, sawa na wastani wa shilingi trillion 2.49 kwa mwezi.

Aidha, katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, mapato ya ndani yamezidi kuongezeka kufikia wastani wa shilingi trilioni 2.85 kwa mwezi. Vile vile, uwiano wa mapato ya ndani kwa Pato la Taifa uliongezeka kutoka asilimia 13.7 mwaka 2020/21 hadi asilimia 15.0 mwaka 2023/24.

Mwenendo huu chanya unadhihirisha mageuzi makubwa kwenye ukusanyaji wa mapato ya ndani kutokana na maboresho mbalimbali yaliyofanywa na Serikali ya awamu ya sita kwa ajili ya kugharamia utekelezaji wa miradi ya maendeleo pamoja na utoaji wa huduma za kijamii kwa wananchi.

Jitihada zilizochukuliwa na Serikali zinajumuisha maboresho ya sera za kibajeti; kuendelea kuboresha mifumo ya TEHAMA ya ukusanyaji wa mapato na kuhakikisha kuwa inasomana; kuboreshwa kwa mazingira ya biashara na uwekezaji; na uhamasishaji kupitia elimu ya kodi na uimarishaji wa mahusiano na walipa kodi.

## (d) Ugharamiaji wa bajeti

Moja ya jukumu la msingi la Wizara ya Fedha ni kutafuta fedha kutoka vyanzo vyote vya ndani na nje ya nchi ili kuwezesha ugharamiaji wa mahitaji mbalimbali kama yalivyopitishwa na Bunge kupitia Bajeti ya Serikali. Katika kutekeleza jukumu hili la kikatiba, Wizara ya Fedha iliwezesha ugharamiaji wa miradi mbalimbali kama ifuatavyo:

### Ujenzi wa Reli ya Kati kwa Kiwango cha Kimataifa



Katika kipindi cha miaka minne ya Serikali ya Awamu ya Sita, Serikali kupitia Wizara ya Fedha imeendelea kugharamia ujenzi wa mradi wa SGR ambapo vipande viwili vya mwanzo kutoka Dar es Salaam hadi Makutupora, ujenzi umekamilika na tayari safari za abiria zimeanza tangu mwezi Juni 2024 kutoka Dar es Salaam hadi Dodoma.

Uwepo wa huduma hiyo ya treni umepunguza muda wa safari kati ya Dar es Salaam na Dodoma kutoka wastani wa saa 10 kwa basi hadi kati ya saa tatu na nne na kuchagiza kasi ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii nchini. Aidha, ugharamiaji wa vipande vingine (Lots 3 – 7) unaendelea na ujenzi uko katika hatua mbalimbali.



### Kuimarisha Shirika la Ndege Tanzania - ATCL

Serikali imeendelea kuimarisha Shirika la Ndege Tanzania ili kutoa huduma bora za usafiri wa anga kwa abiria na mizigo ndani na nje ya nchi.




Serikali katika kipindi cha Novemba, 2020 hadi Februari, 2025, ilitumia shilingi trilioni 1.49 kununua ndege saba ambapo ndege sita ni za abiria na ndege moja ni ya mizigo. Ununuzi wa ndege hizo umelifanya Shirika kuwa na jumla ya ndege 16 ambazo zimeimarisha na kuongeza safari za ndege za ndani na nje ya nchi.

### Ukamilishaji wa Mradi wa Umeme wa Julius Nyerere (MW 2,115)



Serikali katika kipindi cha Novemba, 2020 hadi Februari, 2025, ilitumia shilingi trilioni 1.49 kununua ndege saba ambapo ndege sita ni za abiria na ndege moja ni ya mizigo. Ununuzi wa ndege hizo umelifanya Shirika kuwa na jumla ya ndege 16 ambazo zimeimarisha na kuongeza safari za ndege za ndani na nje ya nchi.

### Uunganishaji wa Umeme Vijijini



Katika kipindi cha Novemba, 2020 hadi Februari, 2025, Serikali imegharamia uunganishaji umeme katika vijiji 4,071 kwa gharama ya shilingi bilioni 1,593 na hivyo kuwezesha vijiji vyote 12,318 vya Tanzania Bara kuunganishwa na umeme.

Aidha, jumla ya vitongoji 33,657 kati ya 64,359, sawa na asilimia 52.3 vimeunganishwa na huduma ya umeme.

## Ujenzi wa Madaraja Makubwa



Serikali imekamilisha ujenzi wa madaraja makubwa ikiwemo Tanzanite (Dar es Salaam) lenye urefu wa kilomita 1.03 na Wami (Pwani) lenye urefu wa mita 510.

Aidha, imekamilisha ujenzi wa Daraja la Kigongo-Busisi (Mwanza) lenye urefu wa km 3.2. Lengo la ujenzi wa madaraja hayo ni kurahisisha shughuli za kiuchumi na ufikiwaji wa huduma za kijamii kwa haraka kwa kupunguza foleni na muda wa usafiri.

## Uwezeshaji katika Sekta ya elimu



Serikali ya Awamu ya Sita imetekeleza jambo la kihistoria kwa kuwafutia ada wanafunzi wa kidato cha tano na sita na kuwafanya wanafunzi hao kusoma kwa utulivu na kuendelea na utekelezaji wa programu ya Elimumsingi na Sekondari Bila Ada na kumalizia maboma yaliyokuwa yamekwama na kuongeza madarasa mengine, kuongeza ajira za waalimu.



Aidha, Serikali ya Awamu ya Sita imeanzisha programu ya ufadhili kwa wanafunzi wa elimu ya juu (Samia Scholarship Program) kwenye fani za sayansi, teknolojia, ubunifu, uhandisi, hisabati na tiba wenye ufaulu wa kiwango cha juu. Kiasi cha shilingi bilioni 6.63 kimetolewa tangu kuanza kwa programu hiyo na kunufaisha wanafunzi 1,313.

Kadhalika, Serikali inatoa ufadhili wa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya vyuo vya kati wanaosoma stashahada za fani za ufundi. Tangu kuanzishwa kwa mpango huo shilingi bilioni 20.08 zimetolewa na kunufaisha wanafunzi 7,732.

Vilevile, Serikali imeanzisha Mfuko wa Wabunifu unaojulikana kama Samia Innovation Fund ili kusaidia wabunifu kuchochea biashara za ubunifu na kuongeza fursa za ajira.

## Ugharamiaji wa Huduma za Afya

Utoaji wa huduma za afya nchini umeendelea kuimarika kutokana na jitihada zinazofanywa na Serikali kuhakikisha upatikanaji wa fedha za kugharamia mahitaji ya sekta hii muhimu kwa ustawi wa jamii. Jitihada hizo zimewezesha: kuongezeka kwa vituo vya kutolea huduma za afya kutoka 8,458 mwaka 2020 hadi 9,826 Februari, 2025; kuimarika kwa hali ya upatikanaji wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi vya kisasa na bidhaa za afya kutoka asilimia 73 mwaka 2020 hadi asilimia 89.3 Februari, 2025; na kuimarika kwa huduma za kibingwa na ubingwa bobezi ambapo huduma hizo sasa zinapatikana katika hospitali za rufaa za mikoa ambazo hapo awali huduma hizo zilikuwa zinapatikana katika ngazi ya kanda.

## Ugharamiaji wa Huduma ya Maji Mijini na Vijijini

Serikali ya Awamu ya Sita imeimarisha hali ya upatikanaji wa huduma za maji safi na salama kupitia utekelezaji wa miradi ya ujenzi na uboreshaji wa miundombinu ya kutolea huduma ya maji vijijini na mijini.

Jumla ya miradi 1,633 imetekelezwa, ambapo kati ya hiyo, miradi 1,335 ni ya vijijini na miradi 298 ya mijini.

Miradi hiyo imeongeza kiwango cha upatikanaji wa huduma ya maji vijijini kutoka wastani wa asilimia 70.1 mwaka 2020 hadi asimilia 79.6 mwaka 2025.

Kwa upande wa mijini, kiwango hicho kimeongezeka kutoka wastani wa asilimia 84 mwaka 2020 hadi asilimia 90 mwaka 2025. Kutokana na ongezeko hilo wananchi 12,547,526 wamenufaika na huduma ya maji safi na salama.

## Uendelezaji wa Makao Makuu – Dodoma

Serikali ya Awamu ya Sita imeendelea kugharamia utekelezaji wa mradi wa uendelezaji wa Mji wa Serikali ambao unajumuisha ujenzi wa majengo 34 na miundombinu wezeshi kama barabara, maji na umeme. Kati ya majengo hayo, 24 ni ya Wizara na 10 ni majengo ya Taasisi.



Aidha, hadi Machi, 2025 wastani wa ujenzi wa majengo ya Wizara umefikia asilimia 89.7 na kutumia jumla ya shilingi bilioni 534.4. Aidha, majengo matatu yamekamilika na kuanza kutumika. Kukamilika kwa majengo yote na miundombinu wezeshi kutawezesha wananchi kupata huduma kwa urahisi na kupendezesha Jiji na hivyo kuwa moja ya vivutio vya utalii mkoani Dodoma.

## Sensa ya Watu na Makazi

Miongoni mwa mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Sita (6) ni kugharamia uendeshaji wa zoezi la Sensa ya Watu na Makazi kwa mafanikio makubwa ambapo asilimia 99.9 ya watu walihesabiwa. Katika zoezi hilo la Sensa ya Watu na Makazi lililofanyika Agosti 23, 2022, takwimu zinaonesha idadi ya watanzania imefikia watu milioni 61.7, sawa na ongezeko la wastani wa asilimia 3.2 kwa mwaka.

Aidha, zoezi hili liliboreshwa kwa kujumuisha takwimu za majengo ili kuwezesha na kurahisisha upatikanaji wa takwimu za nyumba kwa ajili ya maamuzi ya kisera, hususan kodi ya majengo. Kwa mwaka 2024, idadi ya watu imefikia 66,278,276 ambapo kati ya hao, Tanzania Bara ilikuwa na watu 64,241,822, sawa na asilimia 96.9 ya watu wote na Tanzania Zanzibar ilikuwa na watu 2,036,454, sawa na asilimia 3.1.

## Michezo

Serikali ya Awamu ya Sita imeendelea kufanya jitihada mbalimbali za kuendeleza michezo hapa nchini pamoja na kuviwezesha vilabu vyetu kushiriki katika mashindano mbalimbali ndani na nje ya nchi. Aidha, Serikali inaendelea kufanya maandalizi ya mashindano ya CHAN yanayotarajiwa kufanyika Agosti, 2025 na mashindano ya AFCON yanayotarajia kufanyika mwaka 2027.

Hatua za maandalizi zinazotekelezwa ni pamoja na ugharamiaji wa ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya viwanja vya michezo.

Utekelezaji wa miradi hiyo unatarajiwa kuendelea kuchachua shughuli mbalimbali za kiuchumi ikiwemo sekta ya viwanda, utalii na huduma hivyo kuzalisha ajira na kuongeza kipato kwa wananchi katika maeneo ambayo shughuli za ujenzi zinatekelezwa.

## Kufungua Uchumi (Economic Diplomacy)

Serikali ya Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeendelea kuimarisha uhusiano na ushirikiano kati ya nchi yetu na mataifa mengine, jumuiya za kikanda na mashirika ya kimataifa. Kuimarika kwa ushirikiano huo ni matokeo ya jitihada zake za kuifungua nchi kiuchumi kwa kusimamia Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2020 pamoja na kutekeleza Sera ya Mambo ya Nje inayoweka msisitizo katika kutekeleza diplomasia ya Uchumi.

Katika jitihada za kufungua uchumi kupitia ushirikiano na mataifa mengine duniani, Mheshimiwa Rais amefanikiwa kuimarisha uhusiano kati ya Taifa letu na washirika wetu wa maendeleo ambao umetujengea heshima na kuaminika kimataifa. Katika kipindi cha miaka minne ya awali, Serikali ilipokea misaada na mikopo nafuu yenye thamani ya shilingi trilioni 13.71 ikiwemo mkopo usiokuwa na riba wa kiasi cha shilingi trilioni 1.29 uliotolewa na IMF kwa ajili ya kukabiliana na athari za UVIKO-19.

Chini ya uongozi thabiti wa Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Serikali iliandaa Mpango wa Kukabiliana na Madhara ya Kijamii na Kiuchumi ya UVIKO-19 Nchini Tanzania (TCRP) ambao uligharamiwa na fedha hizo kutoka IMF. Fedha hizi zilielekezwa kwenye sekta za afya, elimu, maji, utalii, kaya maskini, makundi maalum ya wanawake, vijana na watu wenye walemavu.

Aidha, Serikali ilitekeleza Programu ya TCRP kwa ufanisi mkubwa na kutuletea matokeo chanya kwa Taifa. Manufaa ambayo yanatokana na mpango huu hapa nchini kwetu ni ya kudumu na yanagusa watanzania karibu kila pembe ya nchi yetu, Bara na Visiwani.

## Mikopo kwa Sekta Binafsi

Wizara ya Fedha kupitia Benki Kuu imeendelea kusimamia utekelezaji wa Sera ya Fedha inayolenga kuweka mazingira wezeshi ya biashara na uwekezaji. Hii ni pamoja na kuhakikisha kuwa sekta binafsi inapata mikopo kwa ajili ya kuwezesha shughuli za kiuchumi za sekta binafsi.

Jitihada hizo zimewezesha kuongezeka kwa mikopo kwa sekta binafsi ambayo imekua kufikia asilimia 13.2 Januari 2024 ikilinganishwa na asilimia 2.6 Januari 2021. Aidha, kutokana na kuimarika kwa shughuli za kiuchumi kutokana na uwepo wa mazingira wezeshi ya biashara na uwekezaji, mikopo chechefu kwa sekta ndogo ya benki imepungua kutoka wastani wa asilimia 9.3 Juni 2021 hadi asilimia 4.4 Februari 2024 ambao ni chini ya ukomo wa kisheria wa wastani wa asilimia 5.

Mafanikio hayo yametokana na hatua za kisera, kiutendaji na kiutawala zilizochukuliwa na Serikali ya Awamu ya Sita (6) katika kuboresha mazingira ya uwekezaji na biashara.

## Mafanikio mengine

**(i)Marekebisho ya Sheria ya Ununuzi wa Umma, Sura 410:**

Kutoa upendeleo kwa bidhaa, kampuni za ndani na makundi maalumu katika ununuzi wa umma ili kuweka misingi ya utekelezaji wa sera ya uzawa (local content) katika utekelezaji wa mpango na bajeti ya Serikali.

Aidha, Serikali imeweka utaratibu maalumu wa ununuzi wa bidhaa, huduma na kandarasi kwa mashirika ya umma yanayojiendesha kibiashara ili kuongeza wigo na uwezo wa ushindani katika soko.

**(ii) Uzalishaji wa Ajira:** Serikali imeendelea kubuni na kutekeleza mikakati mbalimbali ya kuzalisha fursa za ajira nchini kupitia uwekezaji na utekelezaji wa miradi mikubwa ya kimkakati na kielelezo. Aidha, Serikali imeweka mazingira wezeshi kwa sekta binafsi kukua na kupanua wigo wa uzalishaji wa ajira nchini. Kutokana na jitihada hizo, katika kipindi cha Novemba 2020 hadi Februari, 2025 jumla ya ajira 8,084,204 zimezalishwa katika sekta ya umma na sekta binafsi.

**(iii) Programu ya Royal Tour:** Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ilitangaza utalii kwa vitendo kupitia programu ya Tanzania – the Royal Tour, ambayo imekuwa na mafanikio makubwa. Jitihada hizo zimechangia kuongeza idadi ya watalii kutoka 1,711,625 mwaka 2021 hadi 5,360,247 mwaka 2024.

Kati yao, watalii wa kimataifa waliongezeka kutoka 922,692 mwaka 2021 hadi 2,141,895 mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 132.24 na idadi ya watalii wa ndani iliongezeka kwa asilimia 307.94 kutoka watalii 788,933 mwaka 2021 hadi 3,218,352 mwaka 2024.

Kabla ya UVIKO-19, Tanzania ilikuwa inapokea wastani wa watalii milioni 1.5 kwa mwaka. Hii imeongeza mapato ya sekta ya utalii kutoka dola za Marekani milioni 1,248.0 mwaka 2021 hadi dola milioni 3,903.0 mwaka 2024.

**(iv) Amani na Usalama:** Kuendelea kuimarika kwa hali ya ulinzi, amani na usalama nchini kulikowezesha kuvutia uwekezaji wa nje na wananchi kutekeleza shughuli zao mbalimbali za kijamii na kiuchumi na hivyo kukuza kipato cha mwananchi mmoja mmoja na Taifa kwa ujumla.

**(v)Nishati Safi ya Kupikia:** Serikali ya Awamu ya Sita iliandaa na kuanza kutekeleza Mkakati wa Taifa wa Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia mwaka 2024–2034 kwa lengo la kuboresha afya za wananchi na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

## 2. MWELEKEO WA SERIKALI YA AWAMU YA SITA

Kwa kuzingatia mwenenndo mzuri wa ukuaji wa uchumi katika kipindi cha miaka minne ya Serikali ya Awamu ya Sita, ukuaji wa uchumi wa Taifa unatarajiwa kuongezeka na kufikia asilimia 6.0 mwaka 2025 kufuatia matarajio ya kuimarika kwa uchumi wa dunia. Mweleko wa ukuaji wa uchumi unatarajiwa kwenda sambamba na kuimarika kwa viashiria vingine vya uchumi jumla.

Aidha, ili kufikia azma hiyo, Serikali itaendelea kuchukua hatua mbalimbali za kisera na kiutawala ili kuboresha mazingira ya uwekezaji na biashara kama chachu ya ukuaji wa shughuli za kiuchumi. Hatua hizo ni pamoja na mapitio ya Sera za Kodi ili kutabirika katika kipindi cha muda wa kati, kuongeza kiwango cha ushiriki wa sekta binafsi katika usimamizi wa mpango na bajeti ya Serikali na kuongeza tija na ufanisi katika uwezeshaji ili kuvutia mitaji kutoka nje.

Vilevile, Serikali itaendelea kuimarisha mifumo ya ukusanyaji wa mapato ya kodi na yasiyo ya kodi ili kuzuia upotevu wa mapato na hivyo kuwa na uwezo wa kugharamikia miradi mikubwa ya maendelea na huduma za jamii.

## 3. HITIMISHO

Kwa miaka minne ya uwepo wa madarakani kwa Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi wa Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, mafanikio mengi yameweza kupatikana kama yalivyoelezwa hapo juu hususani katika ukuaji na uimarishaji wa uchumi, ustahimilivu wa mfumuko wa bei, ugharamiaji wa mahitaji ya kibajeti na kuimarishwa kwa mahusiano ya kidiplomasia.

Serikali itaendelea kulinda na kuendeleza mafanikio hayo sambamba na kushirikisha wadau wote, hususan sekta binafsi, washirika wa maendeleo na asasi za kiraia ili kujenga uchumi imara na endelevu.

Ushirikishwaji utahusisha katika kufanya mapitio na maboresho ya sera, sheria, kanuni na miongozo mbalimbali ya usimamizi wa masuala ya uchumi na fedha. Aidha, Serikali itaendelea kuimarisha ushirikiano na nchi washirika, jumuiya na mashirika ya kimataifa na kikanda ili kujenga misingi imara ya uchumi, na kuwezesha upatikanaji wa mitaji, kuvutia uwekezaji na kukuza biashara za ndani na nje.

**Mwisho**



# MCHANGO WA WASHIRIKA WA MAENDELEO KATIKA UCHUMI WA TANZANIA



Na. Farida Ramadhani

Maendeleo ya nchi, hususan zile zinazoendelea kama Tanzania hayategemei juhudi za ndani pekee, bali pia ushirikiano wa kimataifa. Washirika wa Maendeleo kwa kushirikiana na nchi zilizoendelea wameendelea kuwa sehemu muhimu ya juhudi hizi katika kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs).

Washirika hawa ni pamoja na Mashirika ya Kimataifa (Multilateral Organizations), Taasisi za Kifedha za Kimataifa, nchi wafadhili (Bilateral Countries) na Asasi Zisizo za Kiserikali (NSAs). Mashirika haya hutoa aina mbalimbali za misaada, ikiwemo fedha, utaalamu wa kiufundi, na msaada wa kibinadamu.

Kwa kuzingatia Mwongozo wa Ushirikiano wa Maendeleo Tanzania (Development Cooperation Framework - DCF), Serikali ya Tanzania imeendelea kuhakikisha kuwa ushirikiano wake na Washirika wa Maendeleo unazidi kuimarika.

Juhudi hizi zinaonekana wazi kupitia moja ya misingi mikuu ya Mwongozo huo, unaosisitiza kuwepo kwa Majadiliano ya Kimkakati yanayofanywa mara mbili kila mwaka. Majadiliano hayo kati ya Serikali na Washirika wa Maendeleo huendeshwa na Wizara ya Fedha upande wa Tanzania Bara (kupitia Idara ya Fedha za Nje) na Ofisi ya Rais – Fedha na Mipango upande wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Majadiliano hayo ya kisera na ushirikiano wa kimaendeleo hutoa fursa muhimu ya kujadiliana, kubadilishana maarifa, uzoefu, na ujuzi. Pia huwezesha kujumuisha maoni na maridhiano mbalimbali yanayotokana na mikutano ya majadiliano ya kisekta.

Lengo la majadiliano hayo ni kuwakutanisha Wadau wote wa Maendeleo ili kujenga uelewa wa pamoja kuhusu malengo ya maendeleo na mbinu za kuyafikia malengo hayo, kuimarisha ushirikiano, kuweka vipaumbele vya pamoja na kuhakikisha utekelezaji wa miradi ya maendeleo yenye tija kwa taifa.



Majadiliano ya Kimkakati yamekuwa chachu ya mafanikio mengi katika sekta mbalimbali, yakichangia moja kwa moja katika ukuaji wa uchumi kupitia uwekezaji unaofanywa na Washirika wa Maendeleo kwenye maeneo muhimu kama vile afya, elimu, kilimo, miundombinu, nishati na teknolojia.

Uwekezaji unaofanywa na Washirika wa Maendeleo una mchango mkubwa katika kuendeleza sekta mbalimbali nchini. Kwa kushirikiana na sekta binafsi pamoja na Asasi Zisizo za Kiserikali (NSAs), Washirika hawa wamekuwa daraja muhimu katika kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs). Ushirikiano huu umewezesha miradi mingi yenye tija kutekelezwa, na hivyo kuchochea ukuaji wa uchumi na kuboresha maisha ya wananchi.

Mchango wao umeonekana katika maeneo mbalimbali ikiwemo misaada na mikopo nafuu kwa ajili ya utekelezaji wa program na miradi mbalimbali ya maendeleo, mfano kwa mwaka 2024, Tanzania imepokea zaidi ya dola za Marekani bilioni 2.7 kutoka kwa Washirika wa Maendeleo, kwa ajili ya miradi ya miundombinu, afya, elimu na sekta nyingine, ambapo asilimia 51 ya fedha hizo ni misaada na asilimia 49 ni mikopo yenye masharti nafuu.

Katika Sekta ya Elimu, Washirika wa Maendeleo wamekuwa na umuhimu mkubwa katika kusukuma gurudumu la maendeleo ya elimu nchini kwa kuchangia kwa kiwango kikubwa katika kuboresha upatikanaji wa elimu bora, jumuishi na endelevu.

Mchango huo umekuwa ukionekana kupitia misaada na uwekezaji mkubwa katika miradi mbalimbali ikiwemo mradi wa Mageuzi ya Elimu Kidijitali (Smart WASOMI) ambao unalenga kuimarisha elimu ya sekondari kwa kutumia teknolojia, mradi wa Mafunzo Endelevu kwa Walimu (MEWAKA) ambao unalenga kuimarisha ubora wa ufundishaji na kuhakikisha walimu wanakuwa na maarifa ya kisasa na mbinu bora za kufundishia pamoja na mradi wa Mfumo wa Taifa wa Elimu Endelevu (EsD) ambao unalenga kuingiza maudhui ya mazingira, mabadiliko ya tabianchi, haki za binadamu, jinsia na uraia katika mitaala ya kitaifa.

Kwenye Sekta ya Afya, Tanzania imepiga hatua kubwa kwa kushirikiana na Washirika wa Maendeleo kupitia miradi mbalimbali ambayo imelenga kuboresha huduma za afya kwa wananchi wote, hususan walioko maeneo ya pembezoni.

Miradi hiyo ni pamoja na mradi wa kujenga na kukarabati vituo vya Afya, kurahisisha upatikanaji wa dawa na vifaa tiba, mapambano dhidi ya magonjwa kama vile malaria, UKIMWI, kifua kikuu na magonjwa ya mlipuko kama ebola na Uviko 19 kwa kushirikiana na Serikali ya Tanzania.

Upande wa Miundombinu, Washirika hawa wamechangia kwa kiasi kikubwa katika kuboresha miundombinu nchini kwa kufadhili ujenzi na ukarabati wa barabara, madaraja, reli na viwanja wa ndege. Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) na Shirika la Ushirikiano wa Kimataifa la Japan (JICA) ni miongoni mwa wafadhili hao.

Katika Sekta ya Nishati, Washirika wa Maendeleo wamekuwa wakisaidia upatikanaji wa umeme wa uhakika, endelevu na nafuu nchini kwa kukuza nishati mbadala, kuimarisha miundombinu ya uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa umeme. Kwa mfano, Korea Kusini imekubali kutoa mikopo ya dola za Marekani bilioni 2.5 kwa Tanzania katika kipindi cha miaka mitano ijayo, ikiwa ni sehemu ya makubaliano ya ushirikiano katika sekta za nishati safi na rasilimali za baharini.

Washirika wa maendeleo wamekuwa na mchango mkubwa katika kuboresha sekta ya kilimo nchini kupitia ufadhili wa miradi mbalimbali ya maendeleo kama vile Mradi wa Kuendeleza Kilimo Kusini mwa Tanzania (SAGCOT) unaofadhiliwa na mashirika kama USAID, Benki ya Dunia na Norway, ambao unalenga kuongeza tija ya kilimo kwa kutumia teknolojia bora, miundombinu ya kisasa na upatikanaji wa masoko kwa wakulima wadogo.

Vilevile, Serikali kwa kushirikiana na Mfuko wa Kimataifa wa Maendeleo ya Kilimo (IFAD) kupitia Mradi Kilimo na Usalama wa Chakula imekuwa ikiwasaidia wakulima kwa kuwapatia mikopo, mafunzo ya kilimo endelevu na miundombinu ya umwagiliaji. Miradi hii imechangia kuongeza uzalishaji, kipato cha wakulima na usalama wa chakula nchini.



Mradi mwingine ni Mradi wa Building a Better Tomorrow (BBT) ambao unatekelezwa kwa kushirikiana na Washirika mbalimbali wa maendeleo kama vile Shirika la Kilimo na Chakula (FAO), Mfuko wa Kimataifa wa Maendeleo ya Kilimo (IFAD), Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) na Shirika la Maendeleo umoja wa Mataifa (UNDP), kwa lengo la kuwawezesha vijana na wanawake kushiriki kikamilifu katika kilimo cha kisasa.

Mchango wa Washirika wa Maendeleo hauishii kwenye rasilimali fedha pekee bali unajumuisha pia utaalamu, utafiti wa kisera na teknolojia bunifu zinazosaidia Serikali kupanga na kutekeleza mipango ya maendeleo kwa ufanisi zaidi.

Hili pia limeonekana kwa kiasi kikubwa katika Sekta ya Kilimo ambapo Washirika wa Maendeleo wamekuwa wakichangia kwenye teknolojia za kisasa za kilimo ikwemo kuwawezesha wakulima kupata mbegu bora, pembejeo na mifumo ya umwagiliaji.

Washirika wa Maendeleo pia wamechangia kwa kiasi kikubwa katika kuimarisha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini ambayo imeiwezesha Serikali kutekeleza mageuzi ya Sera na Sheria kwa lengo la kupunguza urasimu, kurahisisha usajili wa biashara na kuboresha mfumo wa leseni.

Wahenga wanasema kidole kimoja hakivunji chawa, ni dhahiri kwamba mafanikio ya kiuchumi hayawezi kufikiwa kwa juhudi za upande mmoja pekee, ushirikiano wa dhati uliojengwa katika misingi ya uwazi na uwajibikaji kati ya Tanzania na Washirika wa Maendeleo ni njia bora ya kuhakikisha maendeleo endelevu ya kiuchumi kwa vizazi vya sasa na vya baadae.

Pamoja na mafanikio hayo, Serikali ya Tanzania imeonesha dhamira ya dhati ya kupunguza utegemezi wa misaada ya nje kwa kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani, kupambana na matumizi mabaya ya rasilimali na kukuza sekta za uzalishaji kama viwanda, kilimo na madini.

Aidha, kupitia utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (FYDP III), Tanzania inalenga kujenga uchumi wa viwanda unaotegemea rasilimali watu na maliasili kwa maendeleo endelevu.

Ni wazi kuwa ushirikiano kati ya Serikali na Washirika wa Maendeleo umeongeza kasi ya maendeleo ya kiuchumi. Tanzania inaweka mfano mzuri Barani Afrika kuhusu namna nchi zinavyoweza kutumia misaada ya maendeleo kama kichocheo cha kujenga uwezo wa ndani na kujinasua kwenye utegemezi wa muda mrefu.

**Mwisho**

# MFUMO WA GAMIS PORTAL WARAHISISHA UPATIKANAJI WA LESENI ZA UDALALI NCHINI



Na.
Peter Haule

Dalali maana yake ni mtu yeyote aliyeidhinishwa chini ya Sheria ya Udalali kumwakilisha mtu mwingine, shirika au kampuni katika uuzaji, ununuzi, upangishaji wa mali yoyote, au ukusanyaji wa madeni au kodi, ikiwa ni pamoja na mawakala wa mashamba na mazao.

Udalali ni kazi ya kuwa kiungo kati ya mnunuzi na muuzaji wa bidhaa au huduma kwa lengo la kusaidia mchakato wa uuzaji au ununuzi na anayefanya kazi hiyo ni lazima apewe kibali ili aweze kuuza, kununua, au kutafuta wateja kwa niaba ya mteja wake.

Katika muktadha wa Tanzania, udalali unajumuisha shughuli kama, uendeshaji wa minada ya hadhara, uuzaji wa mali zilizotaifishwa, udalali wa mali isiyohamishika kama nyumba na viwanja, kukusanya madeni au ushuru kwa niaba ya taasisi fulani na udalali wa kisheria wa mali zinazouzwa kwa amri ya mahakama.

Faida zinazotokana na udalali ni pamoja na kurahisisha biashara ambapo husaidia wateja kupata wanunuzi au wauzaji kwa haraka hivyo kurahisisha mchakato wa biashara, kuokoa muda na gharama

Kwa kutumia dalali, mteja anaepuka gharama na muda wa kusaka wanunuzi au wauzaji. Dalali ana mtandao mpana wa wateja na uzoefu katika soko, ufahamu wa soko, uwazi katika Manunuzi na Mauzo na kuongeza Ajira na Mapato.

Udalali ni kazi ya kitaalamu inayochangia kwa kiasi kikubwa katika mzunguko wa biashara, ukusanyaji wa mapato, na uwazi katika uhamishaji wa mali kati ya wahusika mbalimbali.

Serikali kupitia Wizara ya Fedha imeanzisha mfumo mpya wa kielektroniki wa utoaji wa leseni za udalali na uendeshaji minada, ikiwa ni hatua ya kurahisisha upatikanaji wa huduma hiyo ambayo awali ilikuwa ikipatikana kwa shida na gharama kubwa kwa waombaji walioko mikoani kutokana na umbali na mlolongo wa kupata kibali makao makuu.

Mfumo huo unaojulikana kama GAMIS Portal, umetengenezwa kwa lengo la kuondoa urasimu na kuwapa urahisi zaidi wananchi wanaohitaji leseni za udalali kuendesha shughuli zao kwa mujibu wa Sheria ya Waendesha Minada (Auctioneer's Act 1928, Cap 227 R.E 2002).

Leseni za udalali hutolewa kwa kipindi cha mwaka mmoja kwa gharama ya shilingi 150,000 au nusu mwaka kwa shilingi 75,000 ambazo hutumika katika minada ya hadhara, ukusanyaji wa madeni, ushuru, tozo mbalimbali na uuzaji wa mali kama nyumba na viwanja.



Changamoto zilizokuwepo kabla ya Mfumo wa GAMIS Portal ni pamoja na waombaji wa leseni kulazimika kusafiri hadi Makao Makuu ya Wizara ya Fedha jijini Dodoma kupata huduma hiyo jambo lililosababisha usumbufu mkubwa, gharama za usafiri na malazi kwa waombaji hasa kutoka mikoa ya mbali.

Wizara ilijipambanua kwa kutumia Teknolojia kwa njia za kielektroniki ambapo mwananchi mwenye uhitaji wa leseni za udalali wanaweza kutembelea Tovuti ya Wizara ya Fedha (www.mof.go.tz) na kujisajili na kuomba leseni hizo wakiwa mahali popote kwa kutumia simu ya kiganjani (Simu janja) au kompyuta zenye huduma ya intaneti.

Mfumo huo  ni rafiki kwakuwa unatoa maelekezo ya namna ya kujisajili ambapo mtu binafsi au mwakilishi wa kampuni anayetaka kujisajili anatakiwa kubonyeza kiungo cha GAMIS Portal kupitia Tovuti ya wizara na kisha kuchagua Create Account ili kuanzisha akaunti ambapo mwombaji anatakiwa kuchagua nywila salama na kuikumbuka kwa matumizi ya baadaye.

Akizungumzia Mfumo huo, Mkurugenzi wa Idara ya Usimamizi wa Mali za Serikali, Bw. Chotto Sendo, alisema kuwa mwombaji anapaswa kupakua fomu ya maombi kupitia sehemu ya Documents na kujazwa kikamilifu kabla ya kuwasilishwa kwa Katibu Tawala wa Wilaya anayotoka mwombaji kwa ajili ya uhakiki na saini.



Aidha Mwombaji anatakiwa kuandaa na kuambatisha nyaraka muhimu kikiwemo Cheti cha Tax Clearance kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Cheti cha Usajili wa Kampuni kutoka BRELA na Leseni ya Biashara kutoka Halmashauri au Manispaa.

Alieleza kuwa Nyaraka hizo zinapaswa kuskaniwa na kupakiwa kwenye mfumo kabla ya kutuma maombi rasmi kwa kuchagua Add Auctioneer Licence na kuambatisha mafaili husika na kubonyeza kitufe cha hifadhi (Save).

Bw. Sendo alisema kuwa Mfumo huo unaonesha hali ya maombi kwa hatua mbalimbali kama maombi yametumwa, yamekataliwa, yanahitaji malipo au malipo yamekamilika na ikiwa maombi yatakataliwa, mwombaji ataweza kuona sababu na kufanya marekebisho kabla ya kuyatuma tena.

Alisema baada ya maombi kukubaliwa, mwombaji atapokea Control Number kupitia mfumo kwa ajili ya kufanya malipo kupitia benki, wakala au mitandao ya simu na malipo hayo yanapaswa kukamilika ndani ya siku 30, vinginevyo mwombaji atalazimika kuomba namba mpya.

Zoezi hilo linamuitaji, mwombaji anatakiwa kufika katika Ofisi ya Uhakikimali ya Mkoa wake kwa ajili ya kuchukua leseni baada ya kukamilisha malipo akiwa na nyaraka halisi alizozituma wakati wa maombi. Iwapo kutakuwa na tofauti kati ya nyaraka hizo na zilizowasilishwa mtandaoni, leseni haitatolewa.

Aidha, mwombaji anatakiwa kuhakikisha kuwa leseni aliyopokea imesainiwa na kutiwa muhuri rasmi wa Ofisi husika ili kuthibitisha uhalali wake.

Kwa kuanzisha mfumo huo wa kisasa, Wizara ya Fedha imeonesha dhamira ya dhati ya kuimarisha utoaji wa huduma kwa wananchi kwa kutumia teknolojia, kupunguza gharama zisizo za lazima na kuongeza uwazi katika mchakato wa utoaji wa leseni.

Wizara inaendelea kuwahimiza waombaji wote kufuata maelekezo ya mfumo kwa makini ili kuepuka ucheleweshaji wa huduma au kukataliwa kwa maombi kutokana na taarifa zisizo sahihi.

**Mwisho**




# Pakua na Soma majarida yetu kupitia Tovuti yetu na Kurasa zetu za Mitandao ya kijamii

@mofURT
Wizara ya Fedha

Ministry of
Finance-Tanzania

@URTMof
Wizara ya Fedha

@mofURT
Ministry of Finance
Tanzania

Wizara ya Fedha
Tanzania

@mofURT
Hazina TV - Wizara
ya Fedha

**Scan Msimbo (QR Code) huu**

Tembelea Tovuti:
www.mof.go.tz



# MFUMO WA HAZINA YA MACHAPISHO, MAPINDUZI HALISI YA MAARIFA



Na. Joseph Mahumi

> MOF Repository imekuja na staili ya kisasa "modern", hakuna tena kuchafuka kwa vumbi au kukumbana na panya aliyegeuza faili kuwa makazi ya kudumu



Katika dunia ya leo inayoendeshwa na maarifa na taarifa, upatikanaji wa taarifa sahihi na kwa wakati ni msingi muhimu katika kupanga na kutekeleza mipango ya maendeleo.

Wizara ya Fedha kama msimamizi mkuu wa Sera za Uchumi na Fedha nchini Tanzania, imejikita katika kuhakikisha taarifa zake muhimu zinapatikana kwa urahisi, uwazi na ufanisi kwa wadau wake wote.

Kama njia bora ya kuimarisha utunzaji wa kumbukumbu na uongezaji wa upatikanaji wa taarifa zake, Wizara ya Fedha ilianzisha Maktaba yake iliyopo katika Ofisi zake (Treasury Square) jijini Dodoma na kuhakikisha huduma hiyo inapatikana kidigitali kupitia Tovuti yake ya *https://library.mof.go.tz/*

Maktaba ya Wizara ya Fedha ni moja ya vitovu muhimu vya maarifa serikalini, ikiwa na dhamira ya kutoa huduma bora za taarifa kwa watumishi wa Serikali, watafiti, wataalamu wa uchumi na wadau wengine wa maendeleo. Ilianzishwa kwa lengo la kutoa rasilimali za maarifa na kuendeleza utamaduni wa kujisomea, kujifunza na kufanya maamuzi yaliyojikita kwenye utafiti.

Ili kufanikisha hayo, Wizara ya Fedha ilianzisha Mfumo wa Hazina ya Machapisho (MOF Repository), ambao unatekeleza jukumu muhimu la kutunza, kusambaza na kurahisisha upatikanaji wa machapisho rasmi ya Wizara, ambayo ni nyenzo muhimu kwa maamuzi ya kisera, ufuatiliaji wa utekelezaji wa bajeti, utafiti wa kitaalamu na upashanaji wa maarifa kwa umma kwa ujumla.

Hii si maktaba ya kawaida ya kimya na mafaili ya rangi ya kaki yaliyochanika pembeni, bali ni maktaba ya kisasa inayofanya kazi kwa kasi ya "5G plus," na inayotoa huduma saa 24, hata wakati mlinzi wa jengo bado yuko usingizini!

## Mfumo wa Hazina ya Machapisho ya Wizara ya Fedha (MOF Repository)

MOF Repository ni Mfumo wa Kidigitali unaotumika kuhifadhi na kusambaza nyaraka na machapisho rasmi ya Wizara ya Fedha kwa njia ya mtandao *https://repository.mof.go.tz/* ambapo mtumiaji anaweza kutafuta, kupakua na kutumia machapisho kulingana na mahitaji yake. Mfumo huu umebuniwa kwa lengo la kuongeza uwazi wa kifedha, kukuza ushirikishwaji wa umma katika masuala ya uchumi, na kuimarisha utunzaji wa kumbukumbu muhimu za kiutawala na kitaalamu.

Kupitia Mfumo huu Machapisho mbalimbali hupatikana kama vile:

- Hotuba za bajeti za kila mwaka ya Serikali Kuu na Wizara ya Fedha
- Vitabu vya bajeti na maelezo ya ziada kuhusu mpango wa matumizi ya Serikali
- Ripoti za utekelezaji wa bajeti na uchambuzi
- Sera na Miongozo ya kifedha na kiuchumi (mfano: Sera ya Bajeti, Sera ya Madeni, Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango)
- Taarifa na tafiti za uchambuzi wa uchumi wa ndani na nje
- Maelezo ya mabadiliko ya fedha (mfano, noti mpya au hatua za usimamizi wa mfumuko wa bei)
- Ripoti za tathmini ya athari za Sera
- Jarida la Hazina Yetu

Matumizi ya Hazina ya Machapisho ya Wizara ya Fedha (MOF Repository) yana faida lukuki kwa watumiaji wa ndani na nje ya serikali. Kwanza, mfumo huu unarahisisha upatikanaji wa taarifa muhimu za kisera, bajeti, na tafiti kwa wakati na kwa urahisi kupitia mtandao.

Hii huwasaidia watunga sera, wachambuzi wa uchumi, watafiti, waandishi wa habari na wananchi wa kawaida kupata nyaraka rasmi zilizothibitishwa, jambo linalowezesha kufanya maamuzi sahihi, kuongeza uwazi wa Serikali, na kuimarisha ushiriki wa umma katika masuala ya kifedha na maendeleo ya Taifa.


*Pili,* MOF Repository huongeza ufanisi wa utunzaji wa kumbukumbu na kupunguza utegemezi wa karatasi, hivyo kuchangia katika utunzaji wa mazingira na kupunguza gharama za uchapishaji. Aidha, mfumo huu husaidia kuhifadhi historia ya nyaraka za Serikali kwa muda mrefu katika mfumo wa kidigitali, jambo ambalo linaweza kuwezesha ufuatiliaji wa mwenendo wa sera na bajeti kwa kipindi kirefu.

Kwa kutumia mfumo huu, Wizara ya Fedha inaongeza uwajibikaji wa taasisi za umma na kuwezesha kizazi cha sasa na kijacho kupata taarifa sahihi kwa maendeleo endelevu.

*Tatu,* matumizi ya MOF Repository yanasaidia sana sekta ya elimu na utafiti kwa kutoa nyenzo muhimu za kitaaluma. Wanafunzi wa elimu ya juu, wahadhiri, na watafiti wanapata fursa ya kutumia machapisho rasmi kama vile vitabu vya bajeti, tafiti za kiuchumi, na taarifa za utekelezaji wa miradi ya maendeleo kama rejea muhimu katika tafiti zao.

Hatua hii huchochea tafiti zenye tija zinazolenga kutatua changamoto halisi za uchumi wa nchi na kusaidia kupendekeza maboresho katika sera na mipango ya maendeleo.

Nne, Mfumo huu pia unachangia katika kurahisisha kazi za mawasiliano ya Serikali na umma. Kupitia MOF Repository, vyombo vya habari na wadau wengine wa mawasiliano wanaweza kunukuu taarifa rasmi moja kwa moja kutoka kwenye chanzo cha kuaminika, hivyo kupunguza upotoshaji wa taarifa za bajeti na mipango ya kifedha.






Kwa kuwa Mfumo huu unapatikana mtandaoni saa 24 kila siku, inamaanisha taarifa hizi zinapatikana popote pale duniani, wakati wowote, kwa yeyote mwenye mahitaji ya kitaalamu au kijamii.

Tano, kwa upande wa utawala bora, MOF Repository ni nyenzo muhimu ya kuongeza uwajibikaji wa serikali. Kwa kuweka taarifa wazi kwa umma, Wizara ya Fedha huweka msingi wa kujenga imani kwa wananchi na Washirika wa Maendeleo kuhusu namna rasilimali za umma zinavyopangwa na kutumika.

Hatua hii husaidia kuimarisha usimamizi wa fedha za umma, kupunguza mianya ya upotevu wa fedha na kuongeza uwazi katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo, sambamba na kufanikisha azma ya Serikali ya Awamu ya Sita ya kujenga uchumi shindani na jumuishi.

Kifupi, Hazina imebadilika kutoka 'ghala la makaratasi' hadi ghala la kidigitali 'smart library in your pocket.' Hakuna foleni, hakuna kukatishwa tamaa, hakuna kupiga hodi ofisi 10. Machapisho yapo Saa 24 Siku zote za wiki, vijana wa Gen Z wanasema 24/7, hata saa nane usiku ukiamka na kiu ya bajeti ya mwaka 2020/21, MOF Repository iko pale, inang'aa kama taa ya emergency!

Mifumo wa Hazina ya Machapisho (MOF Repository) na Maktaba ya Wizara ya Fedha ni rasilimali nyeti na ya kimkakati inayojenga msingi wa ufanisi wa utawala wa kifedha nchini Tanzania.


Kupitia mifumo hii, Wizara ya Fedha sasa inaonesha dhamira yake ya kuwa taasisi ya kisasa, inayowajibika, inayoendeshwa kwa ushahidi, na yenye uwazi kwa wananchi wake.

Ni wajibu wa kila mmoja mtumishi wa umma, mwanafunzi, mwananchi wa kawaida, au mdau wa maendeleo kuyatumia na kuyaendeleza kwa pamoja kama zana za kufanikisha ndoto ya Tanzania ya maendeleo jumuishi na endelevu.

Kazi yako sasa ni kujifunza kwa starehe, kufanya utafiti kwa raha, na kupanua maarifa yako bila hata kuinuka kutoka kwenye kiti chako cha ofisi (au hata cha bustani nyumbani).

> MOF Repository imekuja na staili ya kisasa "modern", hakuna tena kuchafuka kwa vumbi au kukumbana na panya aliyegeuza faili kuwa makazi ya kudumu.

Ukihitaji taarifa ya fedha ya 2018, unafungua tu laptop yako, unakunywa kahawa, unaweka password yako (usiisahau kama kawaida) kisha unapakua chapisho kwa sekunde 10 na kuhamaki umesoma chap chap, tayari upo kwenye ukurasa wa 32 wa bajeti, unafanya uchambuzi kama mtaalamu wa Benki ya Dunia (World Bank).







# MNYORORO WA UGAVI: MSINGI WA UWAJIBIKAJI NA UFANISI KATIKA MATUMIZI YA FEDHA ZA UMMA

Na. Josephine Majura

KATIKA mazingira ya sasa ambapo Serikali ya Tanzania inaweka mkazo mkubwa katika matumizi bora ya rasilimali, usimamizi wa mnyororo wa ugavi (Supply Chain Management) umekuwa nguzo muhimu ya kuhakikisha fedha za umma zinatumika kwa ufanisi na kwa manufaa ya moja kwa moja kwa wananchi.

Kwa mujibu wa Kamishna wa Sera za Ununuzi wa Umma kutoka Wizara ya Fedha, Dkt. Frederick Mwakibinga, takribani asilimia 70 ya bajeti ya serikali hutumika kwenye manunuzi ya bidhaa na huduma.

Kwa maana hiyo, asilimia 70 ya Bajeti Kuu ya Serikali ya 2025/26 ya Shilingi trilioni 56.49, fedha zitakazokwenda kwenye manunuzi ya vitu na huduma ni shilingi trilioni 39.543, na asilimia 30, sawa na shilingi trilioni 16.947 ndizo zitakazofanya kazi nyingine.

Hii inaonesha kuwa mnyororo wa ugavi una mchango mkubwa katika mfumo mzima wa bajeti ya taifa, hivyo usimamizi wake hauwezi kupuuzwa.

Dkt. Mwakibinga anasema kuwa iwapo hakutakuwa na usimamizi thabiti wa mnyororo huo, kuna hatari ya mianya ya upotevu wa rasilimali za nchi kukithiri. Ili kulinda fedha za walipa kodi, Wizara imejielekeza kuimarisha kila hatua ya mnyororo wa ugavi, kuanzia ununuzi, ugomboaji (creating and forwarding) usafirishaji, upokeaji, uhifadhi, hadi matumizi na uondoshaji wa mali.

## MAANA YA MNYORORO WA UGAVI

Mnyororo wa ugavi unahusisha mtangamano wa shughuli mbalimbali ikiwemo zifuatazo:

Mosi ni ununuzi ambao ni upatikanaji wa bidhaa au huduma kupitia michakato ya zabuni na mkataba.

Unahusisha upangaji, ukodishaji au upatikanaji wa bidhaa, kazi za ujenzi au huduma yoyote kwa taasisi.



Ununuzi unajumuisha kutambua na kuandaa mahitaji, kuchagua na kualika wazabuni, kuandaa mikataba, tuzo na kusimamia utekelezaji wa mikataba.

Ugomboaji na uondoaji wa forodha (clearing and forwarding) ni jambo la pili. Hii ni kuhakikisha bidhaa zinapitishwa kihalali na kufika sehemu husika.

Kwa lugha nyingine ni hatua za ukamilishaji wa taratibu za forodha kuhusu shehena zinazoingia au zile zinazotoka nje ya mipaka ya nchi.

Inajumuisha usafirishaji wa mizigo kutoka katika vituo vya kupakia na kushushia hadi kufika mahali ilipokusudiwa.
Tatu ni upokeaji na urejeshaji: Hili linahusisha kukagua, kukubali na kuthibitisha bidhaa zilizowasilishwa na kama hazifai ni kuzirejesha.

Hii ni hatua ya kutambua na kukiri kuwasilishwa kwa bidhaa, vifaa na huduma kutoka kwa muuzaji. Inahusisha ukaguzi wa nyaraka husika, uhakiki wa bidhaa, vifaa au huduma kabla ya kukubalika na Taasisi nunuzi.

Uhifadhi ni jambo la nne katika mnyororo huu wa ugavi. Hii inahususha kuhifadhi bidhaa zilizopokelewa kwa usalama hadi zitakapohitajika.

Usimamizi wa uhifadhi unajumuisha utunzaji wa kumbukumbu, kuweka hatua za ulinzi na usalama ili kuhakikisha ubora na kiasi cha bidhaa vinahifadhiwa ipasavyo hadi wakati wa usambazaji.

Tano ni usambazaji: Hii inahusisha kuusafirisha bidhaa kutoka sehemu ya uhifadhi kwenda kwa watumiaji wa mwisho.

Hatua za usambazaji zinahusisha uzingatiwaji wa masharti muhimu yanayolenga kulinda ubora na usalama wa mali zinazosafirishwa.

Vilevile, usambazaji unahusisha ukamilishaji wa nyaraka zote zinazohusika katika usambazaji wa bidhaa.

Sita, Matumizi na Uondoshaji: Kuhakikisha bidhaa zinatumiwa kwa lengo lililokusudiwa na kuondolewa kwa usahihi pindi zinapochakaa.

Kwa jumla, mnyororo huu hutoa picha ya namna fedha za umma zinavyotumika na kwa faida ya nani. Usimamizi bora wa mchakato huu unaakisi thamani halisi ya fedha za umma kwa kupunguza upotevu, rushwa, na matumizi mabaya ya rasilimali.

## FURSA ZA KIJAMII KUPITIA UGAVI

Mnyororo wa ugavi si tu njia ya kupata bidhaa au huduma, bali pia ni daraja la fursa za kiuchumi kwa wananchi. Kwa mujibu wa Dkt. Mwasimba, kila hatua ya ugavi kama vile clearing and forwarding, upokeaji wa bidhaa, uhifadhi, usambazaji na matumizi inahitaji nguvu kazi, jambo linalowezesha ajira kwa vijana na wanawake.

Kwa upande wake, Dkt. Mwakibinga anasema mfumo huo sasa unazitaka taasisi zitakapotangaza zabuni, zitenge angalau asilimia 30 kwa ajili ya wanawake, vijana, na watu wenye ulemavu. Hata kwenye hatua ya uondoshaji (disposal) wa mali kama magari ya zamani au vifaa vilivyochakaa, wananchi wa kawaida wanapewa nafasi kununua au kutoa huduma ya kuondoa taka hizo.

"Lengo ni kuhakikisha ushirikishwaji mpana wa wananchi katika mnyororo huu kwa kuwa ndio njia bora ya kuhakikisha mzunguko wa uchumi unawafikia wananchi wa kawaida," anasema Dkt. Mwakibinga.



## UGAVI WA KIJANI NA AJIRA KWA WAZAWA

Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Mzumbe, Dkt. Maige Mwasimba, anasisitiza umuhimu wa kuimarisha mnyororo wa ugavi wa kijani (green supply chain). Akitilia mkazo matumizi bora ya rasilimali na utunzaji wa mazingira, Dkt. Mwasimba anaeleza kuwa shughuli kama vile usafirishaji, uhifadhi, na uondoshaji wa taka zisiposimamiwa vyema zinaweza kuchochea uharibifu mkubwa wa mazingira.

Anatoa wito kwa taasisi za umma na binafsi kuzingatia mikataba ya ununuzi yenye masharti rafiki kwa mazingira, kuhamasisha matumizi ya teknolojia safi, na kushirikisha wanawake, vijana, na watu kutoka maeneo ya vijijini katika minyororo ya thamani. "Hii si tu inalinda mazingira bali pia inazalisha ajira na kupunguza umasikini," anasema

Mnyororo wa ugavi ni kiungo muhimu kati ya mipango ya serikali na ustawi wa wananchi. Kupitia mfumo huu, ajira mpya zinazalishwa, uchumi wa ndani unachochewa, huduma muhimu zinafika kwa wananchi kwa wakati na kwa gharama nafuu na kubwa zaidi thamani ya fedha inaonekana.

Ili kufanikisha azma ya maendeleo endelevu, Serikali kupitia Wizara ya Fedha imeonyesha dhamira ya kweli ya kujenga mfumo thabiti, wa kisasa na wa kidijitali wa usimamizi wa mnyororo wa ugavi. Lakini mafanikio hayo hayatawezekana bila ushirikiano wa karibu kati ya serikali, sekta binafsi, vyombo vya habari na wananchi wenyewe.

Akizungumza na wanahabari, Naibu Katibu Mkuu wa Wizara, Bi. Jenifa Christian Omolo, alieleza umuhimu wa masuala ya mnyororo wa ugavi ni muhimu yakaeleweka kwa wadau mbalimbali wakiwemo wananchi wa kawaida na kueleza umuhimu wa wanahabari hao kupewa mafunzo hayo ili kuwahusisha moja kwa moja ili waweze kutoa taarifa sahihi, kwa wakati na zenye kuelimisha umma kuhusu masuala hayo.

Ni wajibu wa kila Mtanzania kushiriki katika kulinda, kuimarisha na kuusimamia mnyororo wa ugavi ili kuhakikisha fedha za umma zinatumika kwa lengo stahiki na hivyo kuleta maendeleo kwa wote.

**Mwisho**



# KONGAMANO LA KODI NA UWEKEZAJI: NGUZO YA KUKUZA MAPATO YA NDANI NA UCHUMI JUMUISHI NCHINI TANZANIA



Na. Scola Malinga



Kongamano la Kodi na Uwekezaji linazidi kudhihirika kuwa jukwaa la kitaifa lenye mchango mkubwa katika safari ya Tanzania kuelekea uchumi wa kisasa, shindani na unaomjumuisha kila mwananchi.

Makongamano hayo yamekuwa chachu ya kuibua mawazo mapya pamoja na kupendekeza mikakati mipya ya kuwezesha nchi yetu kuibua fursa mpya za kuongeza makusanyo ya mapato ya ndani hali kadhalika kuibua mbinu mpya za vyanzo vya mapato na kubainisha namna bora ya Serikali kutekeleza mikakati ya kuongeza mapato ya ndani. Ni dhahiri yametengeneza fursa kwa watafiti nchini kuwasilisha na kujadiliwa matokeo ya tafiti zao kuhusu masuala ya uchumi, uwekezaji na kodi.

Tangu kuanzishwa kwake, makongamano hayo yamekuwa sehemu muhimu ya kuleta pamoja Serikali, sekta binafsi, taasisi za kitaaluma na wadau mbalimbali kwa lengo la kubadilishana mawazo, uzoefu na mapendekezo kuhusu namna bora ya kuboresha mfumo wa kodi na mazingira ya uwekezaji nchini.

Kongamano la Tatu lililofanyika hivi karibuni, limeonesha dhahiri kuwa linazidi kuwa jukwaa la kuimarisha mshikamano kati ya pande mbalimbali za Serikali Tanzania Bara na Zanzibar, pamoja na sekta binafsi na wadau wa maendeleo, katika juhudi za pamoja za kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani na kuchochea ustawi wa kiuchumi kwa wote.

Kauli mbiu ya Kongamano hilo ilihimiza umuhimu wa kuongeza ukuzaji wa rasilimali za ndani kupitia kustawisha fursa kwa wananchi. Kauli mbiu hii inaashiria dhamira ya Serikali kuhakikisha kuwa wananchi hawawi tuu watazamaji, bali wanashiriki kikamilifu katika shughuli za uzalishaji, ujasiriamali na ulipaji kodi.

Lengo kuu la Kongamano lilikuwa kupokea maoni kutoka kwa wadau kuhusu maboresho ya mfumo wa kodi, ada, tozo na sera za mapato kwa ujumla. Kupitia jukwaa hilo, wadau walipata nafasi ya kutoa mapendekezo ya kisera yanayolenga kuchochea uzalishaji mali, kuongeza ufanisi katika ukusanyaji wa mapato, na kuweka mazingira wezeshi kwa wawekezaji wa ndani na wa nje.

Mijadala ya Kongamano hilo ilijikita katika maeneo mbalimbali, ikiwemo uboreshaji wa sera za kodi ili ziendane na hali halisi ya uchumi na uwezo wa walipakodi, kupunguza urasimu katika usimamizi wa kodi, pamoja na kuanzisha utaratibu wa kusikiliza maoni ya walipakodi kabla ya kupitisha mabadiliko ya sheria. Vilevile, wadau walipendekeza upanuzi wa wigo wa kodi kwa kuhakikisha kuwa sekta zisizofikiwa kwa urahisi na Mamlaka ya Mapato (TRA) zinajumuishwa katika mfumo rasmi.

Mbinu bunifu ziliwasilishwa kuhusu namna ya kuongeza mapato kwa kutumia mfumo wa kidigitali, ikiwemo matumizi ya mifumo ya malipo ya kielektroniki, mifumo ya kusajili walipakodi kiotomatiki, na ushirikiano wa karibu kati ya taasisi za serikali ili kurahisisha ufuatiliaji wa shughuli za kibiashara. Wadau walisisitiza kuwa matumizi ya teknolojia ni njia mojawapo ya kuondoa mianya ya ukwepaji kodi na kuongeza ufanisi katika ukusanyaji wa mapato.

Aidha, Kongamano hilo liliangazia umuhimu wa kuwa na sera zinazojielekeza katika kujenga uchumi jumuishi unaotegemea rasilimali za ndani ili kupunguza utegemezi.

Hii ni pamoja na kuwekeza zaidi katika sekta zinazogusa maisha ya kila siku ya wananchi kama kilimo, viwanda vidogo na vya kati, biashara ndogo ndogo, na huduma za kijamii. Wadau walieleza kuwa kukuza uchumi wa ndani na kuwawezesha wananchi kiuchumi ni hatua muhimu ya kuongeza wigo wa walipakodi.

Katika kuangazia hali ya uchumi wa Taifa, ripoti zilizowasilishwa kwenye Kongamano hilo zilionesha kuwa uchumi wa Tanzania unaendelea kuimarika kwa kasi chanya.

Kwa kipindi cha Januari hadi Septemba 2024, Pato la Taifa lilikua kwa kiwango cha asilimia 5.6, ongezeko kutoka asilimia 5.1 katika kipindi kama hicho mwaka 2023.

Mambo yaliyohusishwa na ukuaji huu ni pamoja na kuimarika kwa uzalishaji wa umeme kupitia mradi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere, kuanza kwa huduma za usafiri wa abiria kupitia reli ya kisasa (SGR), upatikanaji wa huduma bora za kijamii na ongezeko la mikopo kwa sekta binafsi.

Pia, ilibainika kuwa mfumuko wa bei uliendelea kuwa chini na thabiti, ukibakia katika wastani wa asilimia 3.1 kati ya Julai 2024 hadi Februari 2025. Hii ilielezwa kuwa ni ishara ya uthabiti wa sera za fedha na uchumi, hali inayotoa mazingira mazuri kwa uwekezaji wa ndani na wa kimataifa.

Kwenye upande wa uwekezaji, takwimu kutoka Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) zilionesha ongezeko kubwa la thamani ya miradi ya uwekezaji kutoka dola za Marekani bilioni 5.720 mwaka 2023 hadi dola bilioni 9.312 mwaka 2024. Ongezeko hili linaakisi mafanikio ya juhudi za Serikali katika kuvutia wawekezaji kupitia maboresho ya sera na mazingira ya kibiashara.





Pia, katika kipindi cha Julai 2024 hadi Februari 2025, Serikali ilikusanya shilingi trilioni 22.58 kutoka mapato ya ndani, sawa na asilimia 99.9 ya lengo la kipindi husika. Ukuaji wa mapato kwa asilimia 16.6 ikilinganishwa na mwaka uliotangulia ni ishara ya ufanisi mkubwa katika usimamizi wa kodi na ushirikiano mzuri kati ya Serikali na sekta binafsi.

Katika kuhakikisha ushirikiano imara kati ya Serikali na sekta binafsi, wadau walipongeza juhudi za kujenga mahusiano mazuri na walipakodi kwa kutumia mbinu ya 4Rs inayojumuisha Maboresho, Ukusanyaji wa Mapato, Mahusiano na Walipakodi, na Uhamasishaji wa Rasilimali.

Kupitia mbinu hii, Serikali imefanikiwa kuhimiza ulipaji wa kodi kwa hiari, kushughulikia changamoto za walipakodi kwa wakati, na kupanua wigo wa kodi kwa kuvutia wawekezaji wapya.

Ili kuweka usawa na haki katika kuchangia Pato la Taifa kwa masuala ya mapato ya kodi, Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, aliteua Tume ya Rais ya Maboresho ya Mifumo ya Kodi kwa ajili ya kuchambua Mfumo wa Kodi na kutoa mapendekezo. Mapendekezo yatakayotolewa na Tume hiyo yatasaidia kwa kiasi kikubwa kuwezesha kuwepo kwa mfumo wa kodi utakaotatua changamoto zinazoikabili Serikali na watu wake.

Wadau wa kongamano walisisitiza umuhimu wa kuendelea kushirikisha wananchi, sekta binafsi na wataalamu wa ndani katika maandalizi ya sera na bajeti za Serikali. Walionesha kuwa ushirikishwaji huo huongeza uwazi, uwajibikaji na uhalisia wa sera zinazopitishwa.

Miongoni mwa viashiria vya matokeo Chanya ya Makongamano hayo ni pamoja na matokeo ya ukusanyaji mapato ya Serikali ambapo Katika mwaka wa fedha 2024/25, Serikali ilipanga kukusanya shs trilioni 50.29. Hadi Mei 2025, shilingi trilioni 45.07 zilikusanywa, sawa na asilimia 89.6 ya lengo la mwaka jambo linaloashiria utekelezaji mzuri wa bajeti na ushirikiano mzuri kati ya Serikali na sekta binafsi.

Kwa ujumla, Kongamano hilo linaendelea kujengeka kama nguzo muhimu ya mageuzi ya kiuchumi na kisera nchini Tanzania. Ni jukwaa ambalo linathibitisha kuwa ushirikiano kati ya Serikali, sekta binafsi, na wananchi ni silaha madhubuti ya kufikia uchumi wa kisasa, unaotegemea rasilimali za ndani na unaowanufaisha wananchi wote.

Kuwepo kwa makongamano ya mara kwa mara kunajenga utamaduni mpya wa kusikiliza, kujifunza, kubadilishana uzoefu na kufanya maamuzi ya kisera kwa misingi ya ushahidi na ushirikishwaji wa kweli. Ni dira ya Tanzania mpya inayoendelea kujenga msingi wa uchumi jumuishi kwa vizazi vya sasa na vijavyo.

**Mwisho**




# WIZARA YA FEDHA YANG'ARA MAONESHO YA WIKI YA UTUMISHI WA UMMA 2025



Na. Saidina Msangi

Wiki ya Utumishi wa Umma kwa mwaka 2025 imefikia kilele chake kwa mafanikio makubwa, na Wizara ya Fedha imeng'ara kama mdau muhimu katika kuhakikisha mafanikio ya maadhimisho hayo yanafikiwa.

Kama ilivyoshuhudiwa katika Uwanja wa Chinangali Park jijini Dodoma, katika Maadhimisho hayo ya kila mwaka kuanzia Juni 16 hadi Juni 23, Wizara ya Fedha imetekeleza majukumu yake kwa ufanisi mkubwa, ikionesha umuhimu wa uwajibikaji na uwazi katika sekta ya umma.

Maonesho ya Wiki ya Utumishi wa Umma ni jukwaa muhimu linalotoa fursa kwa Wizara zote, idara zinazojitegemea, na Wakala wa Serikali kuonesha huduma wanazotoa kwa wananchi. Lengo kuu la maadhimisho hayo ni kuongeza uwazi, uwajibikaji, na ufanisi katika utoaji wa huduma za umma.

Kwa wananchi, maonesho hayo hutoa fursa adhimu ya kujifunza zaidi kuhusu huduma mbalimbali zinazotolewa na Serikali, kuelewa taratibu, na hata kutoa maoni au kero zao moja kwa moja kwa watendaji.

Kwa upande wa Taasisi za Umma, maonesho hayo huruhusu kubadilishana uzoefu, kujifunza kutoka kwa wenzao, na kutambua maeneo yanayohitaji kuboreshwa. Aidha, ni fursa ya kutangaza mafanikio yaliyopatikana na kuelezea mikakati ya baadaye.

Kwa upande wa Wizara ya Fedha, maonesho hayo yamekuwa muhimu katika kuimarisha uhusiano kati ya Wizara na Umma, na pia kuongeza uelewa kuhusu masuala ya kiuchumi na kifedha.

Wizara pamoja na Taasisi zilizo chini yake ilitekeleza majukumu kadhaa ikiwemo:





- Kutoa Elimu ya Masuala ya Fedha na Bajeti: Wizara ya Fedha ilitoa elimu kwa wananchi kuhusu masuala ya kifedha, ikiwemo mchakato wa bajeti ya Serikali, umuhimu wa kulipa kodi, usimamizi wa rasilimali za umma, na fursa za uwekezaji. Wananchi wamepata fursa ya kuuliza maswali na kupata majibu kutoka kwa wataalamu wa Wizara, jambo lililosaidia kuondoa sintofahamu na kuongeza uelewa wa masuala hayo muhimu.

- Kutoa Huduma za Ushauri na Msaada: Timu ya wataalamu kutoka Wizara ya Fedha imekuwa ikitoa huduma za ushauri wa kifedha kwa wananchi na wafanyabiashara wadogo na wa kati. Ushauri huu umejumuisha masuala ya mikopo, fursa za biashara, usimamizi wa fedha binafsi, na namna bora ya kufikia huduma za kifedha zinazotolewa na taasisi mbalimbali. Huduma hiyo imepokelewa vizuri na imewezesha wananchi wengi kupata ufumbuzi wa changamoto za kifedha.

- Kutoa elimu ya Mifumo ya Kielektroniki ya Usimamizi wa Fedha: Katika jitihada za kuimarisha uwazi na ufanisi, Wizara ya Fedha imetoa elimu ya mifumo mbalimbali ya kielektroniki inayotumika katika usimamizi wa fedha za umma, ikiwemo mfumo wa bajeti, mfumo wa ununuzi ya umma, na mifumo ya ulipaji wa malipo ya Serikali. Elimu hiyo imewapa wananchi fursa ya kuelewa namna teknolojia inavyotumika kurahisisha na kuimarisha udhibiti wa fedha za umma.

- Kutangaza Fursa za Mafunzo: Wizara ya Fedha imetumika pia kama jukwaa la kutangaza fursa za mafunzo zinazopatikana ndani ya Wizara na Taasisi zake. Hii imewapa vijana wengi fursa ya kujifunza kuhusu mahitaji ya soko la ajira katika sekta ya fedha na kujiandaa ipasavyo.

- Kutoa elimu na kuhudumia wastaafu wanaolipwa na Wizara. Katika maonesho hayo wataalam wa Wizara walipata nafasi ya kuhudumia wastaafu wanaolipwa na Wizara kwa kuwapa uelewa kuhusu masuala mbalimbali muhimu wanayotakiwa kuyafahamu pamoja na kuwatatulia changamoto mbalimbali zilikuwa zinakwamisha malipo ya mafao yao pamoja na pensheni.

Pia wananchi walipata nafasi ya kupata elimu kuhusu utofauti wa wastaafu wanaolipwa na Wizara ya Fedha na wale wanaolipwa na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii.

Kwa ujumla, ushiriki wa Wizara ya Fedha katika Wiki ya Utumishi wa Umma 2025 umekuwa wa manufaa makubwa kwa Serikali na wananchi. Umeimarisha uhusiano, umeongeza uwazi, na umetoa fursa muhimu ya kuelimisha umma kuhusu masuala muhimu ya kifedha. Wizara inatoa wito kwa wananchi kuendelea kutumia fursa za maonesho kujifunza na kushiriki kikamilifu katika masuala yanayohusu maendeleo ya nchi.

Maonesho ya Wiki ya Utumishi wa Umma, yakiwa na kauli mbiu "Himiza Matumizi ya Mifumo ya Kidigitali ili Kuongeza Upatikanaji wa Taarifa na Kuchagiza Uwajibikaji", yaliyoanza tarehe 16 Juni, 2025 na kuhitimishwa tarehe 23 Juni, 2025 yalishirikisha Taasisi za Serikali 146, ikiwemo Wizara ya Fedha, pamoja na Taasisi zilizo chini ya Wizara.

**Mwisho**



Na. Benny Mwaipaja

*Tathmini ya uhimilivu wa deni iliyofanyika Oktoba 2024 imeonesha kuwa deni ni himilivu katika kipindi cha muda mfupi, wa kati na mrefu. Katika tathmini hiyo, viashiria vinaonesha kuwa kwa mwaka 2024/25: thamani ya sasa ya deni la Serikali kwa Pato la Taifa ni asilimia 40.3 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 55; thamani ya sasa ya deni la nje kwa Pato la Taifa ni asilimia 23.6 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 40; na thamani ya sasa ya deni la nje kwa mauzo ya nje ni asilimia 123.8 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 180,*

# JIELIMISHE KUHUSU DENI LA TAIFA:

**Bila kukopa mambo mengi yasingewezekana**
**Kuna miradi ingemaliza hata miaka 70 kukamilika**

BAADA ya Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Nchemba kusoma hotuba yake Bungeni kuhusu Bajeti Kuu ya Serikali, kama kawaida kumeibuka maneno maneno mitaani hasa kuhusa deni la Taifa ambalo sasa limefikia shilingi trilioni 107. Kuna wanaosema nchi itapigwa mnada, wengine kila Mtanzania anadaiwa shilingi milioni moja na ushee na maneno mengine mfano wa hayo. Lakini hii yote ni baadhi ya watu kukosa maarifa kuhusu Deni la Taifa.

## DENI LA TAIFA NI NINI?

Deni la Taifa ni kiasi cha fedha ambacho serikali ya nchi ikiwemo taasisi binafsi zinakopa ili kufidia upungufu wa mapato. Kwa upande wa serikali, hulazimika kukopa hasa pale ambapo matumizi yanapozidi mapato inayokusanya kutoka vyanzo mbalimbali kama kodi, gawio na tozo mbalimbali.

Serikali inaweza kukopa kutoka kwa wafadhili wa ndani kama benki za ndani au raia wake (mara nyingi kupitia hati fungani), na pia inakopa kutoka kwa wafadhili wa kimataifa kama mashirika ya fedha (Mfano IMF au Benki ya Dunia) au nchi nyingine.

Kuhusu hati fungani (dhamana za serikali), ni kwamba badala ya wananchi kuweka fedha kwenye baadhi ya mabenki kwa akaunti za muda maalumu, kupitia hati fungani wananchi hupata faida kubwa na hivyo kuboresha zaidi uchumi na maisha yao. Hati fungani hutumika sana katika kuwekeza kwa sababu zinatoa mapato ya riba ya kawaida na zina hatari ndogo ikilinganishwa na uwekezaji kama wa hisa. Kwa hiyo ni njia pia ambayo imekuwa ikitunisha mifuko ya wananchi na hivyo kuchangia pia kukuza mitaji na uwekezaji kwa wazawa.

Lingine la kufahamu ni kwamba serikali inapokopa kutoka kwa taasisi binafsi huongeza deni lake la taifa, lakini kwa upande mwingine taasisi hizi hupata riba kama faida ya uwekezaji wao. Hii ni njia mojawapo ambayo serikali hutumia kupata fedha za kufanyia miradi pasipo kulazimika kukusanya kodi zaidi au kupunguza matumizi.

## MIKOPO YA TAASISI BINAFSI KWENYE DENI LA TAIFA

Ufafanuzi wa hili ni kwamba, sekta binafsi inapokopa nje, deni hilo husajiliwa Benki Kuu (BoT) na hata malipo yake yanafanywa kwa fedha za kigeni zilizopo nchini.

Kuna sababu nyingi za serikali kulitambua deni linalokopwa na sekta binafsi, kubwa ikiwa

kwamba mhusika anaweza akahamisha fedha nyingi kwa mkupuo na kuleta athari katika uchumi wa nchi na pia ni lazima ieleweke fedha hizo zinakwenda kufanya nini zisije zikawa zinakwenda kutumika katika mambo yenye athari hasi kama kufadhili ugaidi, ushoga na mengine mfano wa hayo.

Kwa hiyo ukisikia Deni la Taifa, basi ujue kwamba zimo pia fedha zilizokopwa na sekta binafsi.

## DENI LA SASA LA TAIFA

Akiwasilisha Bajeti ya Serikali, Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Nchemba alisema bungeni hivi karibuni kwamba mpaka sasa mwenendo wa Deni la Serikali ni himilivu.

Alisema hadi Aprili 2025, deni la Serikali lilikuwa shilingi trilioni 107.70. Kati ya kiasi hicho, deni la nje ni shilingi trilioni 72.94 na deni la ndani ni shilingi trilioni 34.76.

"Tathmini ya uhimilivu wa deni iliyofanyika Oktoba 2024 imeonesha kuwa deni ni himilivu katika kipindi cha muda mfupi, wa kati na mrefu. Katika tathmini hiyo, viashiria vinaonesha kuwa kwa mwaka 2024/25: thamani ya sasa ya deni la Serikali kwa Pato la Taifa ni asilimia 40.3 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 55; thamani ya sasa ya deni la nje kwa Pato la Taifa ni asilimia 23.6 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 40; na thamani ya sasa ya deni la nje kwa mauzo ya nje ni asilimia 123.8 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 180," alisema.

Dkt. Mwigulu alisema kwamba Machi 2025, kampuni ya Moody's Investors Service ilifanya zoezi la mapitio ya kwanza ya tathmini ya nchi kukopesheka katika masoko ya fedha ya kimataifa kwa mwaka 2025. Kwamba baada ya kukamilika kwa zoezi hilo, kampuni hiyo ilichapisha matokeo ambayo yameendelea kuiweka Tanzania katika daraja la B1 kama ilivyokuwa kwa matokeo ya mwisho ya mwaka 2024.




*Aidha, kampuni nyingine kubwa ya Fitch Ratings inaendelea na mapitio ya kwanza kwa mwaka 2025 na inatarajia kuchapisha matokeo hivi karibuni.*

*Kampuni hiyo ilichapisha matokeo ya mapitio ya mwisho Desemba 2024, ambapo iliiweka Tanzania katika daraja la B+," alisema.*

Alisema matokeo ya tathmini ya nchi kukopesheka katika masoko ya mitaji ya kimataifa yanaendelea kuipa taswira chanya nchi yetu katika medani za kimataifa.

"Matokeo hayo ni bora kuliko nchi nyingine za ukanda wa Afrika Mashariki na Kati. Pamoja na mambo mengine, matokeo hayo yamechangiwa na jitihada za Serikali inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kuweka mazingira wezeshi ya uwekezaji kwa sekta binafsi, kukuza uchumi, kusimamia kwa makini deni la Serikali na kuimarisha ushirikiano wa kimataifa," alisema.

Mhe. Dkt. Nchemba alisema Serikali itaendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ili kuhakikisha deni linaendelea kuwa himilivu ikiwemo: Kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani ili kupunguza utegemezi wa mikopo katika ugharamiaji wa bajeti; kuelekeza fedha za mikopo katika miradi inayokuza mapato ya ndani na mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi; na kuendelea kuwahimiza Maafisa Masuuli kuzingatia maandalizi ya msingi ya miradi kabla ya kuingia mikataba kwa mujibu wa sheria, kanuni na miongozo iliyopo ili kuepuka ongezeko la gharama za mradi unaokopewa fedha.

## WANAOLALAMIKIA DENI LA TAIFA

Kama nilivyogusia hapo juu, baadhi ya Watanzania wamekuwa wakilalamikia ongezeko la Deni la Taifa kutokana na sababu kadhaa, kubwa ikiwa ni kukosa maarifa ya kutosha kuhusu Deni la Taifa au wanalizungumzia kisiasa zaidi.

Hata hivyo, mambo ambayo wamekuwa wakiyataja kusababisha hofu yao moja wapo ni ukuaji wa haraka wa deni na hivyo wamekuwa wakihofia kuwa litaiongezea nchi mzigo wa kodi au kupunguza huduma za msingi kama afya na elimu.

Pia wamekuwa wakidai kuwa miradi inayofadhiliwa na mikopo haileti faida ya moja kwa moja kwa wananchi wa kawaida. Lakini wapo pia ambao wamekuwa na hofu kwamba deni la sasa linaweza kuleta mzigo kwa vizazi vijavyo ambao watalazimika kulilipa. Wengine wamekuwa wakilalamika kuwa kuna ukosefu wa uwazi kuhusu jinsi mikopo inavyotumiwa na jinsi miradi inavyosimamiwa.

## SABABU ZA KUKOPA

Kimsingi, tangu awamu ya kwanza ya uongozi wa nchi yetu hadi awamu hii ya sita, serikali imekuwa ikikopa kwa sababu ya uhitaji wa kufanya miradi yenye tija kwa wananchi huku makusanyo ya fedha za ndani yakiwa hayatoshi na pia imekuwa ikifanya hivyo kwa sababu inakopesheka na inaaminika.

Kama tutakavyokuja kuona baadaye, takribani nchi zote duniani zinakopa zikiwemo nchi zinazoonekana kuwa na uchumi mkubwa kama Marekani, Japan na nyinginezo tena nyingine zina asilimia kuwa zaidi ya uwiano wa deni lilikofikia na GDP ya nchi hizo.

Mimi mwandishi wa makala haya nilibahatika kushiriki semina, ambayo pamoja na mambo mengine, deni la taifa lilifundishwa kwa ufasaha na kwa bahati nzuri mmoja wa walimu wetu alikuwa Gavana wa sasa wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Emmanuel Tutuba ambaye wakati huo alikuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha.

Wanasemina tulijifunza kwamba hatua ya kukopa au kutokopa inaanza na nakisi inayotokana na bajeti ya taifa. Kwamba ukishakuwa na nakisi unalazimika kukopa kwa ajili ya kufidia pengo hilo.

"Na kimsingi tunakopa kwa sababu sisi ni matajiri. Maskini hawezi kukopa. Tunakopa pia kwa sababu tunaaminika. Unaona mashirika makubwa kama Benki ya Dunia yanatukopesha ni kwa sababu tunaaminika," anasema Tutuba.

Anasema pesa hukopwa katika maeneo matatu; kwa ajili ya kuunga mkono bajeti (general budget support), kukopa kwa ajili ya sekta ambayo wadau wanadhani kuna changamoto zinazopaswa kutatuliwa kama vile sekta ya afya na tatu ni mikopo ambayo ni kwa ajili miradi ambayo wafadhili wenyewe huamua kupeleka fedha zao huko.

Kama ilivyo kwa mtu binafsi, mkopo unatakiwa uwe ni kwa ajili ya kuwekeza ama kufanya jambo muhimu la dharura na siyo kukopa kwa ajili ya, mathalan, kuolea mke mwingine au kustarehe. Na ukichunguza, matajiri wengi tunaowaona mitaani kwetu wakifanya vizuri kiuchumi, wamefika hapo walipo kwa sababu ya kukopa.

Na hivyo, Watanzania wanachopaswa kuuliza ni sababu za kukopa ambazo mara nyingi, kama si zote, huwa muhimu na zina majibu sahihi. Lingine la muhimu kwa Watanzania ni kufuatilia usimamizi thabiti wa matumizi ya mkopo.

Mtu yeyote makini, kama ilivyo nchi, hukopa leo ili afanye mambo ya maendeleo huku akilipa taratibu kwa sababu thamani ya fedha zake leo haiwi sawa na kesho au kadri muda unavyokwenda.

Gazeti moja liliwahi kumkariri Mchumi Mwandamizi wa Chuo Kikuu cha Mzumbe, Profesa Aurelia Kamuzora akifafanua kwamba endapo uwekezaji mzuri unafanyika katika mikopo inayochukuliwa, uchumi wa nchi unaendelea kukua.

"Deni la Taifa linavyozidi kukua, ndio uchumi wa nchi unakua na nafasi ya kuongezeka inakuwepo pia kama fedha zinapokopwa zinawekwa vizuri kwa sababu mtaji wa kufanya miradi mbalimbali unakuwepo," alinukuliwa na gazeti hilo akisema.

Profesa alizidi kufafanua kwamba mzunguko wa fedha nchini unaongezeka kama fedha zinazokopwa zinaingia katika miradi.

Kwa wanaokumbuka, fedha zilizobatizwa za korona, Sh trilioni 1.3 kutoka Shirika la Fedha Duniani (IMF) ambazo zilitumika kujenga miradi mingi ikiwemo ya madarasa na vituo vya afya, zilisababisha mzunguko mkubwa wa fedha kwa wananchi. Wapo ambao walishiriki kutoa huduma mbalimbali kwenye miradi husika ikiwemo mafundi na hivyo mzunguko wa fedha hizo kuleta athari nyingi chanya kwenye jamii.

"Unajua hata nchi zilizoendelea zinakopa kwa ajili ya kufanya miradi mbalimbali na kuongeza mzunguko wa fedha. Sioni shida ya deni kuongezeka kama zinatumika kwa tija na hazingii mifukoni mwa watu," alisema Profesa.

Nikirudi darasani kwenye semina, tulijifunza kwamba sababu ya kuwepo kwa haja ya kukopa ni pamoja na ongezeko la watu na mahitaji yao, mapato ya ndani kutokidhi mahitaji ya vipaumbele vilivyopo na haja ya kufungua miundombinu ya mitaji ili kuongeza pato la mtu mmoja mmoja
.
Sababu nyingine tukaelezwa kwamba ni kuongeza mapato ya ndani kwa kufungua miradi inayozalisha zaidi na kuzuia mtikisiko wa thamani ya shilingi. Sababu nyingine ni tabia za mkopaji kwamba tunakopa kwa mahitaji sahihi, uwezo wa kulipa tunao, dhamana ya mkopo na kuangalia masharti ya mikopo.

## AINA ZA MIKOPO

Wananchi wanapaswa kujua pia kwamba mikopo mingi ambayo nchi imekopa iko katika masharti nafuu ambayo riba yake ni chini ya asilimia moja na kipindi cha kuiva mikopo hiyo ni hadi miaka 40.

Kwa mfano, mwezi Juni mwaka jana, Tanzania ilipata mkopo kutoka Korea wa Dola bilioni 2.5 na watu wakavumisha kwamba eti Tanzania imetoa kipande cha bahari kama dhamana ya mkopo huo kitu ambacho hakikuwa kweli. Kwanza, licha ya kwamba si Tanzania pekee iliyopata mkopo huo, lakini unalipwa kwa miaka 40 na riba yake ni asilimia 0.01.

Ni mkopo utakaotolewa kwa muda wa miaka mitano na utaanza kulipwa baada ya miaka 25.

Hata hivyo, kuna mikopo iliyo katika masharti ya kati ambayo riba yake ni chini ya asilimia 3 na kipindi cha kuiva mkopo ni hadi miaka 15 mpaka 20.

Kadhalika kuna mikopo michache sana ambayo nchi imekopa ikiwa katika masharti ya kibiashara ambayo riba yake inalingana na hali ya soko na kipindi cha kuiva ni hadi miaka saba.

## DENI NI HIMILIVU

Kama tutakavyokuja kuona baadaye kulinganisha na nchi nyingine, deni la Tanzania bado ni himilivu (sustainable) kwani kuna nchi ambazo madeni yao si himilivu na hivyo tunaweza kusema 'hazikopesheki.'

Maana ya deni kuwa himilivu ni kwamba serikali inapokopa inakuwa pia na uwezo wa kulipa madeni yake ya sasa na madeni yake yatakayoiva baadaye bila kuathiri ukuaji wa uchumi na shughuli nyingine za serikali ikiwemo kutoomba msaada wa kulipiwa madeni kutoka mataifa au taasisi nyingine.

Hata hivyo, taarifa zilizopo ni kwamba Tanzania ni moja ya nchi inayokimbiliwa na wakopeshaji kutokana na uhimilivu wake.

Katika bajeti zake ikiwemo ya mwaka huu, serikali imekuwa ikieleza kuwa moja ya vipaumbele ilivyo navyo ni kulipa deni la taifa pamoja na kugharamia mishahara ya watumishi wa umma na maandalizi ya Uchaguzi Mkuu wa 2025.

Serikali pia imesema inaendelea na juhudi za kuimarisha miradi ya maendeleo ya kimkakati na kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji.

Cha msingi, elewa ndugu Mtanzania mwenzangu, kama si kukopa, kwa maana ya kutegemea makusanyo ya fedha za ndani baadhi ya miradi ingechukua hata miaka 70 kukamilika, lakini miradi hiyo zikiwemo barabara, madaraja, hospitali na miradi ya maji, tunandelea kutumia na kunufaika nayo huku tukilipa kidogo kidogo. Wale ambao miaka ya nyuma wakitaka kwenda Musoma kutoka Dar es Salaam walilazimika kupitia Nairobi, Kenya, hili wanaweza kulielewa zaidi.

Elewa pia kwamba Deni la Taifa limekuwa likiongezeka kwa miaka ya hivi karibuni kutokana na mikopo ya ndani na nje ambayo serikali imekuwa ikikopa kwa ajili ya kufadhili miradi mikubwa ya maendeleo, kama vile ujenzi wa reli ya kisasa (SGR), bwawa la kuzalisha umeme la Julius Nyerere, barabara, madaraja, na miundombinu mingine ya kijamii.

Kuna Mtanzania ambaye haoni haja ya kuwa na reli ya kisasa? Kuna ambaye haoni haja ya kuwa na umeme wa uhakika kupitia ujenzi wa Bwawa la Julius Nyerere? Hii miradi itanyanyua haraka uchumi wetu lakini kwa kutegemea makusanyo ya ndani pekee, pengine ingechukua miaka mingi sana kukamilika au ikashindikana kabisa.

## USIMAMIZI WA DENI, KUKOPESHEKA

Kama nilivyokwisha dokeza, deni la taifa bado ni himilivu na kwenye kila bajeti serikali inatenga fedha za kulipa deni. Kwa mujibu wa tathmini za taasisi za kimataifa kama IMF na Benki ya Dunia, serikali imekuwa ikilipa madeni yake kwa wakati huku ikiendelea na mikakati ya kupunguza utegemezi wa mikopo kwa kuboresha ukusanyaji wa mapato ya ndani, hususan kupitia kodi.

Kwa kifupi, taasisi hizi za kimataifa hususani Benki ya Dunia na Shirika la Fedha Duniani (IMF) zimekuwa zikifanya ukaguzi, ambapo huangalia uwezo wa nchi kurejesha mikopo kwa kuzingatia ukuaji wa uchumi, mapato ya ndani, na uwiano wa deni na pato la taifa (GDP).

Ripoti ya Benki ya Dunia imeonyesha kwamba ukuaji wa uchumi wa Tanzania ulikuwa asilimia 5.2 mwaka 2023 na makadirio ya sasa (mwaka 2025) asilimia 6.0 ambayo ni dalili nzuri kwamba nchi inajiimarisha kiuchumi.

Hata hivyo, Tanzania inachukua mikopo kwa uangalifu, kuhakikisha kuwa mikopo hiyo inatumiwa kwa miradi yenye faida na inayosaidia kuongeza mapato, hivyo kuongeza uwezo wa kulipa mikopo hiyo kwa wakati.

## NCHI ZA AFRIKA ZENYE MADENI MAKUBWA

Nchi nyingi za Afrika zinakabiliwa na changamoto za madeni, ambapo baadhi ya nchi zina viwango vya juu vya deni la taifa kutokana na sababu mbalimbali kama vile kushuka kwa mapato, vita vya ndani, changamoto za kiuchumi au uwekezaji mkubwa kwenye miundombinu.

Baadhi ya nchi za Afrika zenye deni kubwa kwa takwimu za mwaka jana ni pamoja na Sudan ambayo deni lake wakati lilikuwa ni takribani asilimia 211 ya GDP. Nchi ningine pamoja na uwiano wa deni na pato la taifa (GDP) kwenye mabano ni Eritrea (175%), Cape Verde (160%), Msumbiji (120%), Zambia (115%), Angola (100%), Ghana (80-85%), Kenya (70-75%), Afrika Kusini (70%) na Ethiopia (Karibu asilimia 60-65% ya GDP).

Lakini kama tulivyoangalia hapo awali, uwiano wa deni la Serikali ya Tanzania kwa Pato la Taifa (GDP) ni asilimia 40.3 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 55.

Inaelezwa kwamba nchi nyingi za Afrika zenye madeni ambayo si himilivu zinakopa kwa ajili ya maendeleo ya miundombinu na miradi mingine ya kijamii, lakini ukosefu wa usimamizi mzuri wa fedha na changamoto za kiuchumi zinafanya madeni haya kuwa mzigo mkubwa kwa baadhi ya nchi hizi.

## NCHI NYINGINE NJE YA AFRIKA ZENYE DENI KUBWA

Nchi nyingi duniani zina deni la taifa, lakini baadhi ya nchi zina madeni makubwa sana kutokana na ukubwa wa uchumi wao, sera za matumizi ya serikali, au hali ya kiuchumi. Zifuatazo ni nchi ambazo zina madeni makubwa (Kwa uwiano wa asilimia ya Pato la Taifa – GDP):

Inayoongoza ni Japan yenye karibu asilimia 260 ya GDP. Nchi nyingine zenye deni kubwa na uwiano wake na pato la taifa (GDP) kwenye mabano ni Ugiriki (180%), Italia (145%), Lebanon (150%), Venezuela (zaidi ya 300%), Marekani (120%) na Argentina (asilimia 100 ya GDP).

Nchi za Ureno, Hispania na Uingereza pia zina viwango vya juu vya deni, ingawa sio sawa na nchi hizo tajwa hapo juu. Lakini ni ukweli pia kwamba deni linapokuwa kubwa inaweza kuwa hatari kwa uchumi wa nchi ikiwa halidhibitiwi vizuri, kwani linaweza kupelekea kudorora kwa maendeleo au kutegemea zaidi mikopo ya kimataifa.

## NCHI AMBAZO HAZIKOPESHEKI

Nchi ambazo hazikopesheki kwa urahisi mara nyingi zinajulikana kama "nchi zenye hatari kubwa ya kufilisika au zilizoshindwa kulipa madeni (sovereign default) na hivyo zina uwezo mdogo au hazina kabisa uwezo wa kupata mikopo kutoka masoko ya kifedha ya kimataifa. Hii inatokana na mambo kama vile madeni makubwa, ukosefu wa utulivu wa kisiasa, migogoro ya ndani, au uchumi dhaifu.

Nchi hizi zinaweza pia kuwa na mikopo ya zamani ambayo hawajalipa (default), hali inayozuia uwezo wao wa kukopesheka. Baadhi ya nchi za Afrika na nje ya bara hilo zenye hali hii kwa takwimu za mwaka

## NCHI KUMI (10) ZENYE UWIANO WA JUU ZAIDI WA DENI LA SERIKALI DUNIANI 2025

| | | |
|---|---|---|
| 1. | JAPANI | 260% |
| 2. | SUDANI | 211% |
| 3. | SINGAPORE | 175% |
| 4. | UGIRIKI | 152.9% |
| 5. | ITALIA | 138.7% |
| 6. | MALDIVES | 133.6% |
| 7. | BAHRAIN | 129.8% |
| 8. | MAREKANI | 124.1% |
| 9. | LAOS | 118.3% |
| 10. | UFARANSA | 115.3% |

mmoja ni pamoja na Zimbabwe, Sudan, Eritrea, Somalia, Chad, Sudan Kusini na Venezuela.

Athari za kutokopesheka ni pamoja kukosa fedha muhimu za maendeleo, kama vile kwa ajili ya kujenga miundombinu, huduma za afya na elimu au kunapotokea majanga. Nchi hizi pia huwa na matatizo ya kijamii na kiuchumi kwa maana ya kwamba hali hii mara nyingi inasababisha kuporomoka kwa huduma za kijamii, kushuka kwa thamani ya sarafu na ugumu wa kuwekeza katika sekta za uzalishaji mali.

Nchi inapokosa sifa za kukopesheka pia hujikuta ikiongeza utegemezi wa misaada ya kimataifa kutoka kwa mashirika kama Umoja wa Mataifa au nchi wafadhili, badala ya kupata mikopo kwa masharti ya kibiashara.

Kukosa uwezo wa kukopesheka ni changamoto kubwa kwa nchi zinazoendelea, kwani kunadhoofisha uwezo wao wa kushiriki kikamilifu kwenye uchumi wa kimataifa na kuboresha maisha ya raia wao.

Watanzania tumshukuru sana Mungu hatuko huko. Deni letu bado ni himilivu, tunakopesheka na hivyo tuna uwezo wa kuendelea kubuni miradi ya maendeleo itakayosisimua uchumi na kuogeza uwezo wetu wa kuhudumia madeni. Tusihoji deni, bali tuhoji sababu ya deni na tujikite kwenye kujiridhisha kwenye usimamizi wa fedha tunazokopa,

**Mwisho**



# USHIRIKIANO PPP BARA NA ZANZIBAR KURAHISISHA UTEKELEZAJI MIRADI YA UBIA



Na. Asia Singano

Wizara ya Fedha, kupitia Kitengo cha Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPP), inaendelea kushirikiana vyema na Ofisi ya Rais – Kazi, Uchumi na Uwekezaji, Zanzibar kuhusiana na masuala ya PPP ambapo, ushirikiano huo umeleta mafanikio makubwa katika utekelezaji wa miradi mbalimbali inayotekelezwa kupitia Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi.

Dhana ya PPP, kwa mujibu wa Sheria ya PPP Sura 103 ni makubaliano ya kimkataba kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi ambapo Sekta Binafsi inatekeleza majukumu kwa niaba ya Sekta ya Umma kwa mkataba wa muda maalumu baada ya kumalizika kwa muda wa mradi huo hukabidhiwa kwa Serikali.

Majukumu ya Kitengo cha PPP, Wizara ya Fedha, ni pamoja na, Kuandaa Sera na Mfumo wa Usimamizi wa Miradi ya PPP, Kuandaa na kufanya mapitio ya Sera, Sheria, Kanuni na Miongozo, kuandaa na kutoa mwongozo wa masuala ya ubia PPP katika mikakati na mipango ya sekta mbalimbali, Utekelezaji wa miradi ikiwemo uchambuzi na mafunzo.

Kwa upande wa Zanzibar, Idara ya PPP ina majukumu mbalimbali yakijumuisha kuratibu na kusimamia miradi yote ya PPP kwa upande wa Zanzibar ambapo Idara hiyo imefanikisha utekelezaji wa Miradi 13 ya PPP ambayo hadi Desemba 2024 utekelezaji wake ulishaanza na unaendelea ambapo baadhi ya miradi hiyo ipo katika sekta za bandari, uwanja wa ndege, afya nk.

Mnamo Aprili 2019, Ofisi ya Makamu wa Rais, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SJMT) na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ), ziliandaa mwongozo maalumu wa vikao vya kuimarisha ushirikiano kuhusu miradi inayotekelezwa kupitia ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi ili kuziwezesha Wizara, Idara

na Taasisi husika kujiandaa na kushiriki kikamilifu katika vikao hivyo na kuhakikisha utekelezaji wa majukumu yao unazingatia mahitaji ya pande mbili za Muungano.

Malengo mahsusi ya vikao vya kuimarisha ushirikiano ni pamoja na: Kubadilishana uzoefu, sera, sheria, utaalamu na wataalamu kati ya Tanzania Bara na Zanzibar, kuimarisha ushirikiano wa kiutendaji na ziara za kikazi za mara kwa mara kati ya sekta zinazofanya shughuli zinazoshabihiana; na kujadili na kushughulikia changamoto mbalimbali zilizopo na zitakazojitokeza katika Muungano.

Katika kufikia malengo ya Mwongozo huo, Wizara ya Fedha, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SJMT), iliandaa na kuratibu kikao na Wizara na Taasisi zinazosimamia utekelezaji wa Sera na Sheria ya PPP kwa upande wa Tanzania Bara na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ).

Kikao hicho kilifanyika katika ngazi ya wataalamu kuanzia tarehe 16 -17 Desemba 2024 na kufuatiwa na kikao cha Makatibu Wakuu na Wataalamu tarehe 18 Desemba 2024, ambapo Wajumbe wa Kikao hicho walitoka Wizara ya Fedha (Kitengo cha PPP na Kituo cha PPP) kwa upande wa SJMT na Upande wa SMZ uliwakilishwa na Wajumbe kutoka Ofisi ya Rais – Kazi, Uchumi na Uwekezaji.

Katika kikao hicho wajumbe walibadilishana uzoefu kuhusu



dhana ya PPP, Sera, Sheria na Kanuni zinazosimamia utekelezaji wa programu za PPP ambapo pande mbili zilijifunza kuhusu Miundo ya Taasisi zinazosimamia PPP, taratibu za maandalizi, uidhinishaji na usimamizi wa miradi ya Ubia (PPP). Vilevile, washiriki walipata fursa ya kujadili mafanikio na changamoto za utekelezaji wa programu ya PPP katika Serikali hizo mbili.

Awali akizungumza kwa niaba ya Katibu Mkuu, Wizara ya Fedha, Dkt. Natu El-maamry Mwamba, jijini Dodoma katika kikao cha kwanza kuhusu ushirikiano kati ya Serikali zote mbili, Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Fedha, Bi. Jenifa Omolo, aliwaagiza Wataalamu wa PPP, kuhakikisha miradi yote mikubwa yenye mvuto wa kibiashara nchini inatekelezwa kwa ubia kati ya sekta hizo ili kuipunguzia Serikali mzigo wa kugharamia miradi hiyo.

Alisema kuwa utekelezaji wa miradi kupitia PPP ni sehemu ya kujenga uchumi imara na ni suala ambalo linatekelezwa na nchi nyingi ulimwenguni.

Kwa upande wake Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji, Zanzibar, Bw. Rashid Ali Salim, aliwaagiza wataalamu hao kuhakikisha wanayafanyia kazi yale yote waliyokubaliana katika kikao hicho, hususani suala la kuwa na mkakati wa pamoja wa kuuza fursa na kuibua miradi ya pamoja ya PPP.

Katika kuendeleza ushirikiano huo, Wizara ya Fedha, Tanzania Bara, kupitia kitengo cha PPP, kilishiriki kikao cha pili cha ushirikiano kati ya pande hizo mbili kilichofanyika Visiwani Zanzibar, katika Ukumbi wa ZURA, kikihusisha Wataalamu wa PPP wa pande zote mbili.

Timu ya Wataalamu wa PPP, kutoka Wizara ya Fedha, iliongozwa na Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Fedha, Bi. Amina Khamis Shaaban, wakiambatana na Kaimu Kamishna wa Kitengo cha PPP, Wizara ya Fedha, Bw. Bashiru Taratibu.

Akizungumza katika kikao hicho Katika ukumbi wa ZURA Visiwani



Zanzibar, Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Fedha, Bi. Amina Khamis Shaaban, alisema Serikali itaendelea kutoa ushirikiano kwa Sekta Binafsi ili kurahisisha utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo na kuhakikisha wananchi wanapata huduma nzuri katika nyanja mbalimbali ikiwemo afya, elimu na huduma nyingine zote muhimu kwa ubora na urahisi na kukuza uchumi wa nchi.

"Ni muhimu kushirikisha sekta binafsi katika mipango ya maendeleo, ambao wao wana ujuzi, wana utaalamu lakini vilevile wengine wana fedha kwa hiyo hilo ni jambo muhimu katika kushirikiana nao" alisema Bi. Amina.

Kwa upande wake Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji, Zanzibar, Bw. Rashid Ali Salim, ameitaka Sekta Binafsi nchini kutumia fursa zilizopo Serikalini za kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo kwakuwa pande zote mbili zitanufaika na fursa hizo.

> *Tunaialika Sekta Binafsi kuja kuwekeza katika miradi hii ambayo ina manufaa makubwa mbali na ajira na kulipa kodi, miradi hii hurejeshwa Serikalini baada ya muda tutakaokubaliana kwa mujibu wa mkataba" alisema Bw. Salim.*

Naye, Kaimu Kamishna wa Kitengo cha Ubia Kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPP), Wizara ya Fedha, Bw. Bashiru Taratibu, alisema Wizara ya Fedha, kupitia Kitengo cha PPP, itaendelea kuungana kwa pamoja na Idara ya PPP Zanzibar, kuendelea kushawishi Sekta Binafsi kushirikiana na Sekta ya Umma kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo.

Awali akizungumza kwa niaba ya Katibu Mkuu, Wizara ya Fedha, Dkt. Natu El-maamry Mwamba, jijini Dodoma katika kikao cha kwanza kuhusu ushirikiano kati ya Serikali zote mbili, Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Fedha, Bi. Jenifa Omolo, aliwaagiza Wataalamu wa PPP, kuhakikisha miradi yote mikubwa yenye mvuto wa kibiashara nchini inatekelezwa kwa ubia kati ya sekta hizo ili kuipunguzia Serikali mzigo wa kugharamia miradi hiyo.

Alisema kuwa utekelezaji wa miradi kupitia PPP ni sehemu ya kujenga uchumi imara na ni suala ambalo linatekelezwa na nchi nyingi ulimwenguni.

"Ahadi yetu sisi ni kushirikiana na wenzetu hawa kuhakikisha kuwa tunatengeneza mazingira mazuri yatakayowezesha kuvutia sekta binafsi kuja kuungana na Serikali zetu zote mbili kuhakikisha tunatekeleza miradi hii ya maendeleo" alisema Bw. Taratibu.

Kikao kilibaini kuwa katika utekelezaji wa Sera, Sheria na Kanuni kumekuwa na mafanikio mbalimbali ikiwemo kuongezeka kwa uelewa wa dhana ya PPP kwa wadau wake na hivyo kusababisha miradi inayoibuliwa na Sekta binafsi (Unsolicited project) kuongezeka kwa upande wa SMZ ambapo hadi kufikia mwezi Novemba, 2024 SMZ wana Miradi kumi na tatu (13) iliyo katika hatua ya utekelezaji.

Kwa upande wa Tanzania Bara, mafanikio yapo kwenye miradi inayoibuliwa na Mamlaka za Serikali (Solicited projects) ambapo hadi kufikia mwezi Novemba, 2024 jumla ya miradi 74 ipo kwenye hatua mbalimbali za maandalizi.

Serikali zote mbili zinatekeleza programu ya PPP kwa kuzingatia Sera za PPP ambazo kwa upande wa Tanzania Bara Sera iliandaliwa mwaka 2009 na upande wa Zanzibar Sera iliandaliwa mwaka 2014.

Mashirikiano kwenye eneo la PPP baina SJMT na SMZ yanasimamiwa na Mwongozo wa ushirikiano ulioandaliwa Aprili, 2019 kwa lengo la kubadilishana uzoefu na mikakati ya utekelezaji wa Programu ya PPP pamoja na mbinu za kutatua changamoto zinazojitokeza.

Kikao kinachofuata kinatarajiwa kufanyika mwaka wa Fedha 2025/2026 Tanzania Bara ambapo wataalamu wa PPP kutoka Zanzibar wanatarajiwa kuungana na Wataalamu wa PPP Bara ili kujadiliana masuala mbalimbali kuhusu utekelezaji wa miradi ya Ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi.

**Mwisho**





# IFAHAMU WIZARA YA FEDHA

Na. Eva Ngowi

Katika mfululizo huu wa makala za Ifahamu Wizara ya Fedha, tumeendelea kuchambua kwa kina majukumu, muundo na mchango wa Idara mbalimbali ndani ya Wizara hii muhimu katika ustawi wa uchumi wa Taifa.

Katika makala zilizotangulia, tulielezea historia ya Wizara ya Fedha tangu kupata Uhuru hadi ilivyo leo, sambamba na kutoa uchambuzi wa Idara nne, ambazo ni: Idara ya Uchambuzi wa Sera, Idara ya Usimamizi wa Deni la Serikali, Idara ya Fedha za Nje, pamoja na Idara ya Usimamizi wa Bajeti ya Serikali. Kila Idara ilielezewa kwa kina kwa kuangazia majukumu yake ya msingi pamoja na miundo ya kiutendaji inayoiwezesha kutekeleza majukumu hayo kwa ufanisi.

Katika makala haya, tunaendelea na uchambuzi wa Idara nyingine tatu ambazo nazo ni muhimu sana katika kuhakikisha usimamizi mzuri wa rasilimali za umma na maendeleo ya sekta ya fedha nchini. Idara hizi ni:

1. **Idara ya Sera za Ununuzi wa Umma**– inayosimamia na kuratibu mifumo ya manunuzi ya umma kwa kuhakikisha ufanisi, uwazi na thamani ya fedha katika matumizi ya serikali.
2. **Idara ya Uendelezaji wa Sekta ya Fedha–** yenye jukumu la kuendeleza na kusimamia sera zitakazowezesha ukuaji thabiti wa sekta ya fedha ili kusaidia maendeleo ya uchumi.

Makala haya yanalenga kuielewesha jamii na wadau kwa ujumla kuhusu kazi na umuhimu wa Idara hizi katika kuhakikisha uwazi, uwajibikaji na ufanisi katika usimamizi wa fedha za umma, sambamba na kuimarisha mifumo ya kifedha itakayowezesha ukuaji wa uchumi endelevu. Tafadhali endelea kujisomea makala hii muhimu ili kuielewa vyema Wizara ya Fedha na mchango wake katika maendeleo ya Taifa letu.

## IDARA YA SERA ZA UNUNUZI WA UMMA

Katika utekelezaji wa majukumu yake, Idara inaongozwa na Kamishna wa Sera ya Ununuzi wa Umma, ambaye ni mtaalamu mwandamizi wa ununuzi na ugavi aliyesajiliwa na Bodi ya Wataalam wa Ununuzi na Ugavi (PSPTB). Kamishna huteuliwa chini ya Wizara yenye dhamana ya ununuzi wa umma, na huwajibika moja kwa moja kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha.



DKT. FREDERICK MWAKIBINGA

Kamishna wa Sera ya Ununuzi wa Umma

## MAJUKUMU YA IDARA YA SERA YA UNUNUZI WA UMMA

Majukumu ya Kamishna yameainishwa katika Kifungu cha 7 cha Sheria ya Ununuzi wa Umma, Sura Na. 410.

Idara ya Sera za Ununuzi wa Umma (PPD) inajumuisha sehemu kuu mbili:

### 1. Sehemu ya Uandaaji na Ufuatiliaji wa Sera

Majukumu ya sehemu hii ni pamoja na yafuatayo:

a. Kuandaa Sera ya Taifa na Mkakati wa Ununuzi wa Umma na Ugavi;

b. Kupitia sera, kanuni na miongozo pamoja na maelekezo mengine yanayohusu ununuzi wa umma na ugavi kwa lengo la uhuishaji;

c. Kufuatilia utekelezaji wa Sera ya Ununuzi wa Umma na Ugavi;

d. Kushauri Serikali Kuu, Serikali za Mitaa na vyombo vilivyoundwa kisheria juu ya masuala yanayohusu Sera na usimamizi wa ununuzi na ugavi; na

e. Kufanya tafiti kuhusu Sera za ununuzi wa umma na ugavi na kushauri ipasavyo.

### 2. Sehemu ya Usimamizi wa Ununuzi

Majukumu ya sehemu hii ni pamoja na yafuatayo:

a. Kuendeleza na kusimamia kada ya ununuzi wa umma na ugavi;

b. Kufuatilia na kutathmini mifumo ya usimamizi wa ununuzi na ugavi;

c. Kushauri kuhusu maombi ya kibali cha kuhalalisha ununuzi uliokwishafanyika;

d. Kufuatilia na kutathmini utendaji wa Wakala na taasisi zinazosimamia ununuzi wa umma;

e. Kushauri kuhusu muundo, uteuzi wa wakuu wa vitengo vya usimamizi wa ununuzi na ugavi na kupendekeza uhamisho wa watumishi wa ununuzi na ugavi; na

f. Kuwa kiungo kati ya Serikali, taasisi za kitaaluma na wadau wengine katika masuala yote yanayohusiana na ununuzi na ugavi katika sekta ya umma.

## MAFANIKIO YALIYOPATIKANA

Tangu kuanzishwa kwa Idara ya Sera za Ununuzi wa Umma, mafanikio mbalimbali yamepatikana ikiwemo yafuatayo:

a. Kutungwa kwa Sera ya Taifa ya Usimamizi wa Mnyororo wa Ugavi ya Mwaka 2025, ambayo imeunganisha shughuli zote zilizopo katika mnyororo wa ugavi, zikiwemo ununuzi, ugomboaji na uondoshaji, upokeaji, utunzaji, uhifadhi, usambazaji, matumizi na uondoshaji.

b. Kutungwa kwa Sheria ya Ununuzi wa Umma Na. 10 ya Mwaka 2023, inayojumuisha shughuli zote zilizopo katika mnyororo wa ugavi pamoja na Kanuni za Ununuzi wa

Umma SN. 518 zinazotumika katika utekelezaji wa Sheria hiyo.

c. Kutungwa na kutumika kwa Kanuni za Maadili ya Watumishi wa Umma, Wataalamu na Wazabuni wanaoshiriki katika shughuli za ununuzi wa umma na ugavi.

d. Kuboresha Muundo wa usimamizi wa Vitengo vya Usimamizi wa Ununuzi (PMU) kwa kuwapandisha hadhi Wakuu wa Vitengo (HoPMU) kuwa Wakurugenzi wa Ununuzi na Ugavi (Directors of Procurement Management Units – DPMU), hatua iliyolenga kuimarisha mamlaka yao ya kiutendaji, kuongeza uwajibikaji na kuleta ufanisi zaidi katika utekelezaji wa shughuli za ununuzi ndani ya taasisi za umma

e. Kuanzisha Mfumo wa Kielektroniki wa Usimamizi wa Taarifa za Watumishi wa Ununuzi na Ugavi Serikalini (Procurement and Supplies Personnel Information System – PSPIS), kwa ajili ya kuratibu, kuhifadhi na kufuatilia taarifa za watumishi waliopo kwenye kada ya ununuzi na ugavi katika taasisi za umma.

f. Kuandaa na kuanza kutumia Mwongozo wa Ufuatiliaji na Tathmini ya Utendaji wa Taasisi za usimamizi wa ununuzi wa umma na ugavi, zikiwemo Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA), Mamlaka ya Rufaa za Zabuni za Umma (PPAA), Bodi ya Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi (PSPTB) na Wakala wa Huduma za Ununuzi Serikalini (GPSA), ili kuweka viwango vya uwajibikaji na utendaji vinavyopimika.

## IDARA YA UENDELEZAJI WA SEKTA YA FEDHA

Sekta ya Fedha ni miongoni mwa sekta muhimu katika ukuaji wa uchumi wa nchi. Maendeleo ya sekta ya fedha yana mchango mkubwa katika ukuaji wa uchumi na kupunguza umaskini. Sekta hii ina majukumu mbalimbali ikiwemo: ukusanyaji, uchakataji na utoaji wa taarifa kuhusu masoko, uwekezaji na upatikanaji wa mitaji; kufuatilia uwekezaji na utawala bora wa matumizi ya fedha katika kuchochea ukuaji wa uchumi.

Maendeleo ya sekta ya fedha yana mchango mkubwa katika kuimarisha uchumi na kupunguza umaskini. Sekta hii hufanya kazi kadhaa muhimu, ikiwa ni pamoja na kutoa taarifa za soko kuhusu uwezekano wa uwekezaji na mgao wa mtaji, kufuatilia masuala ya uwekezaji, kuwezesha ukuaji wa biashara, kutofautisha na kudhibiti hatari na kurahisisha ubadilishanaji wa bidhaa na huduma mbalimbali. Sekta ya fedha imegawanywa katika sekta ndogo tano ambazo ni benki, masoko ya mitaji, bima, huduma ndogo za fedha na hifadhi ya jamii.

Kwa kuzingatia umuhimu wa Sekta ya Fedha, Wizara ya Fedha iliunda Idara ya Uendelelezaji sekta hiyo ambayo ina jukumu la kuandaa na kutekeleza Sera, Mikakati na Sheria zinazolenga uendelezaji na ujumuishwaji wa wananchi katika sekta ya fedha ili kuleta maendeleo endelevu kwa Taifa na kupunguza umaskini.



**DKT. CHARLES MWAMWAJA**
Kamishna wa idara ya Uendelezaji wa Sekta ya Fedha

## LENGO LA IDARA YA UENDELEZAJI WA SEKTA YA FEDHA

Lengo kuu la Idara ya Uendelezaji wa Sekta ya Fedha ni kuratibu masuala ya fedha nchini, kuandaa na kufuatilia utekelezaji wa Sera, Mikakati , Sheria pamoja na kutoa ushauri wa kitaalamu kwenye masuala yanayohusu sekta ya fedha. Idara pia inashirikiana na wasimamizi wa sekta ya fedha kwa lengo la kuhakikisha utulivu wa mfumo wa fedha na kukuza ukuaji wa uchumi.

## MAJUKUMU YA IDARA

Idara ya Uendelezaji wa Sekta ya Fedha ina majukumu makuu mawili ambayo ni muhimu katika kukuza sekta ya fedha:

### 1. Kuandaa na Kutekeleza Sera na Mikakati ya Kitaifa ya Kuwezesha Maendeleo ya Sekta ya Fedha

Idara hii ina jukumu la kubuni, kuandaa, kutekeleza na kufanya ufuatiliaji wa Sera na mikakati ya kitaifa inayolenga kuendeleza sekta ya fedha nchini. Sera na mikakati hii inasaidia kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma za kifedha na kurahisisha upatikanaji wa huduma kwa wananchi na biashara mbalimbali. Mikakati ya kitaifa pia inaangalia namna ya kuhamasisha uwekezaji katika sekta ya fedha, na kuhakikisha kuwa kuna mazingira bora ya kibiashara ambayo yatavutia wawekezaji wa ndani na nje ya nchi.

### 2. Kuwezesha Upatikanaji wa Huduma na Bidhaa Tofauti za Kifedha Zilizo Endelevu na Zinazokidhi Mahitaji ya Makundi Mbalimbali

Moja ya changamoto kubwa katika nchi nyingi ni upatikanaji wa huduma za kifedha kwa makundi ya watu wa kipato cha chini. Idara hii inalenga kuimarisha upatikanaji na utumiaji wa huduma na bidhaa za kifedha zinazokidhi mahitaji ya wananchi wa rika zote na vipato tofauti. Hii inahusisha kuwahamasisha Watoa Huduma za Fedha kubuni na kutoa huduma za fedha zinazoendana na mahitaji ya makundi mbalimbali katika jamii, utoaji wa elimu ya fedha hususan kuhusu mikopo, uwekaji akiba, bima, kujiandaa kustaafu, uwekezaji, bima ya amana pamoja na uwepo wa fursa mbalimbali katika Sekta ya Fedha.

## BAADHI YA MAENEO YA KIPAUMBELE

Idara ya Uendelezaji wa Sekta ya Fedha, kwa kutambua umuhimu wa upatikaji na utumiaji wa huduma za fedha kwa wananchi, wajasiriamali, wanawake na watu wenye ulemavu, imekuwa ikitekeleza majukumu yafuatayo:

a. Kuratibu utekelezaji wa Mpango Mkuu wa Maendeleo ya Sekta ya Fedha wa Mwaka 2020/21 - 2029/30 na Mkakati ya Upatikaji wa Huduma za Fedha kwa Wajasirimali Wadogo na Wa Kati wa mwaka 2023/24-2028/28;

b. Kuratibu utekelezaji wa Programu ya Elimu ya Fedha ya mwaka 2021/22-2025/26. Miongoni mwa majukumu yanayotekelezwa katika eneo la elimu ya fedha ni pamoja na: Utoaji wa elimu ya fedha kupitia maadhimisho ya Wiki ya Huduma za Fedha Kitaifa yanayofanyika kila mwaka; Utoaji wa Elimu ya fedha kwa wananchi hususan wanaoishi maeneo ya vijijini ambapo Idara imepanga kufikia mikoa yote nchini.

   Kutoa elimu ya fedha kwa Wajasiriamali Wadogo na wa Kati ili kuwawezesha kuandaa, kusimamia biashara zao na kukopesheka kupitia fursa mbalimbali zilizopo katika sekta ya umma na biashara;

c. Kuratibu utekelezaji wa Mkakati wa Ugharamiaji wa Miradi ya Maendeleo kwa Njia Mbadala wa mwaka 2021. Katika kutekeleza Mkakati wa Serikali wa Njia Mbadala za Kugharamia Miradi ya Maendeleo katika sekta ya umma na binafsi yaani Alternative Project Financing Strategy, kuwezesha utoaji wa Hatifungani ya Miaka 10 ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira ya Jiji la Tanga yaani Tanga Urban Water Supply and Sanitation Authority (Tanga-UWASA), ambapo kiasi cha shilingi bilioni 54.7 kimepatikana, sawa na mafanikio ya asilimia 103.

Hatifungani hii imeorodheshwa kwenye Soko la Hisa la Dar es Salaam na Soko la Hisa la Luxemburg (LuxLE). Fedha zilizopatikana kupitia hatifungani hii zinatumika kutekeleza miradi ya ujenzi wa miundombinu ya huduma endelevu za maji, utunzaji wa mazingira katika Jiji la Tanga. Aidha, Idara imeendelea kutoa mafunzo kwa Wizara, Idara za Serikali namna ya kuandaa maandiko ya Miradi ya maendeleo ambayo itagharamiwa kwa vyanzo mbadala ikiwemo PPP, benki za biashara na masoko ya fedha na dhamana. Vilevile , sekta ya benki imeongeza ubunifu katika kutumia masokoa ya mitaji kupata mitaji.

Idara ya Uendelezaji wa Sekta ya Fedha ina nafasi muhimu katika kuleta mabadiliko katika sekta ya fedha nchini.

**Mwisho**

UTT AMIS
Asset Management and Investor Services

*Mshirika Hakika katika Uwekezaji*

# Uza vipande / Toa pesa kwa simu

**Chini ya Milioni 5**



1. Bonyeza 150*82#
2. Chagua akaunti
3. Kuuza vipande
4. Ingiza kiasi

**TEMBELEA OFISI ZETU, TUKUHUDUMIE**

**DAR ES SALAAM**
S.L.P 14825, Dar es salaam
Jengo la Sukari
Mtaa wa Ohio na Sokoine
Ghorofa ya pili

**DODOMA**
S.L.P 1310, Dodoma
Ghorofa la sita (6)
Jengo la PSSSF,
Mtaa wa Makole

**ARUSHA**
S.L.P 2490, Arusha
Ghorofa ya 4, Ngorongoro
Conservation Tower
(Karibu na B.O.T Arusha)

**MOROGORO**
Gorofa ya 3
Jengo la NHC - Barabara ya
2/D old Dar es salaam

**MWANZA**
S.L.P 640, Mwanza
Ghorofa ya Mezzanine,
NSSF Commercial Complex,
Kenyatta Rd. Nyamagana

**MBEYA**
S.L.P 1210, Mbeya
Ghorofa ya 2,
NHIF Tower, Barabara
ya Karume, Mbeya Mjini

**ZANZIBAR**
S.L.P 2190, Zanzibar
Ghorofa ya 3, Jengo la
Sheikh Thabit Kombo,
Mtaa wa Michenzani

**KAHAMA**
Ground floor, Shinyanga
NSSF-jengo Mafao house
Barabara ya Boma-Nyahonga

080 011 2020 www.uttamis.co.tz UTTAMIS App
Download on the App Store
GET IT ON Google Play



# MAJIBU YA WIZARA YA FEDHA KUHUSU HOJA MBALIMBALI ZA WABUNGE, BUNGENI-DODOMA

Na. Joseph Mahumi, Peter Haule na Josephine Majura

Katika robo ya Tatu ya mwaka wa fedha 2024/2025, Wizara ya Fedha ilitoa ufafanuzi kuhusu masuala mbalimbali yanayohusu majukumu yake ikiwa ni pamoja na Serikali kuweka mkazo utoaji huduma saa 24 vituo vya forodha, kuondoa vikwazo katika ukusanyaji kodi na kuhakiki wastaafu kidijitali.

## APR 9, 2025 | SERIKALI KUPITIA MAPENDEKEZO YA MABORESHO YA MFUMO WA KODI, ADA NA TOZO

Mnamo Aprili 29, 2025, Naibu Waziri wa Fedha, Mhe. Hamad Hassan Chande, akijibu swali la swali la Mbunge wa Viti Maalum Mhe. Jacqueline Ngonyani, aliyetaka kujua mpango wa Serikali wa kupunguza Tozo na Kodi za uingizaji wa samaki toka nje ya nchi.

Mhe. Chande alisema kuwa kupitia Kamati ya Maboresho ya Mfumo wa Kodi (Task Force on Tax Reforms) katika vikao vyake, inaendelea kupokea mapendekezo yanayowasilishwa na wadau kuhusu maboresho ya mfumo wa kodi, ada na tozo mbalimbali ikiwa ni pamoja na eneo la uingizaji wa samaki kutoka nje ya nchi.

Alisema kuwa Tathmini ya kina hufanyika ili kubaini hali ya soko, tabia za walaji, mahitaji, gharama, athari kwa mapato ya Serikali na kuzingatia umuhimu wa kulinda walaji na wafanyabiashara wa ndani ili kuongeza mchango wa thamani katika mnyororo wa Uchumi.

Mhe. Chande aliongeza kuwa maamuzi na mapendekezo ya kupunguza tozo na kodi za uingizaji wa samaki kutoka nje ya nchi yatafanywa kulingana na matokeo ya tathmini husika.

## APR 11, 2025 | TRA KUIMARISHA UTOAJI WA ELIMU KWA MLIPA KODI

Naibu Waziri wa Fedha, Mhe. Hamad Hassan Chande (Mb), alilieleza bunge kuwa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) imekuwa ikitoa elimu ya kodi kwa njia mbalimbali kwa makundi yote ya walipakodi pamoja na Vikundi vya Wanawake Wajasiriamali.

Amesema hayo bungeni jijini Dodoma,alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum, Mhe. Janeth Elias Mahawanga, aliyetaka kujua mpango wa Serikali wa kuanzisha madarasa ya Elimu kwa Mlipa Kodi kupitia Vikundi vya Wanawake Wajasiriamali.

Alisema TRA imekuwa ikielimisha wanawake wajasiriamali kupitia vikundi vyao mbalimbali ikiwemo chemba ya wafanyabiashara

wanawake "Tanzania Women Chamber of Commerce (TWCC)" na makundi mengine ya wajasiriamali wanawake.

Mhe. Chande alifafanua kuwa Katika kuhakikisha utoaji elimu ya mlipa kodi unakuwa endelevu na inawafikia wajasiriamali wanawake, TRA itaendelea kushirikiana kikamilifu na Wizara husika kuimarisha mawasiliano na mtandao wa wanawake wajasiriamali ili kupitia taasisi au jumuiya zao waweze kukidhi mahitaji ya elimu ya kodi na shughuli zao za kiuchumi.

Aidha, Mhe. Chande aliongeza kuwa kupitia utoaji Elimu kwa Mlipakodi TRA imefanikiwa kuongeza idadi ya usajili wa wajasiriamali wanawake wanaojisajili kwa hiari.

## APR 15, 2025 | SERIKALI IMEHAKIKISHA UMMA KUWA HAKUNA SEKTA ITAKAYOKOSA FEDHA KUTOKANA NA MABALILIKO YA SERA

Mnamo Aprili 15, 2025, Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb) alisema kuwa Serikali imewahakikishia Watanzania kuwa hakutakuwa na sekta itakayokosa fedha kwa sababu ya mabadiliko ya sera ya baadhi ya mataifa zinazolenga kupunguza kuyasaidia mataifa yanayoendelea ikiwemo Tanzania.

Alisema hayo bungeni jijini Dodoma, wakati akijibu hoja za wabunge zilizojitokeza katika Bunge la Kumi na mbili, mkutano wa 19 katika kikao cha sita.

Alisema Serikali imefanya tathmini katika sekta zote kupitia Timu iliyochini ya Waziri Mkuu na kuanza kuchukua hatua baada ya baadhi ya mataifa kubadili sera zao ili kupunguza fedha kwa nchi zinazoendelea kama Tanzania.



*Tulikuwa na mahitaji ya takribani shilingi bilioni 220 kwenye sekta ya Afya ili kuziba pengo la fedha ambazo tulikuwa tunazitarajia kutoka kwa wadau wa maendeleo, Serikali tayari imetoa kiasi cha shilingi bilioni 98 kwenda kwenye sekta ya afya ili kufidia pengo lililojitokeza na tathmini hiyo inaendelea katika maeneo mengine na utoaji wa fedha utaendelea katika maeneo mengine ambayo yanahitaji fedha", alisema Dkt. Nchemba.*

Aidha, Dkt. Nchemba alimpongeza Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa anayoifanya kwa kuwa ameweza kuivusha nchi kipindi ambacho dunia nzima imekuwa ikipita kwenye msukosuko ya kiuchumi ambayo imekuwa ikitokea mfululizo kwa kipindi cha miaka minne.

Alisema kuwa kulitokea changamoto ya Uviko 19, uhaba wa fedha za kigeni na sasa sera za nje za baadhi ya mataifa ambazo tayari Serikali imeanza kuchukua hatua na kama taifa linaamini litavuka.

Dkt. Nchemba alisema kuwa sekta ya Afya ndiyo iliyoguswa zaidi ambapo Serikali itaendelea kuchukua hatua zaidi ikiwemo kuwekeza fedha kwenye uzalishaji ndani ya nchi wa madawa na vifaa tiba vilivyokuwa vinapatikana kupitia wabia.

Alisema kuwa Mpango wa Maendeleo na Bajeti itakayosomwa katika Bunge linaloendelea, sehemu ya fedha itaelekezwa kwenye viwanda vinavyozalisha madawa ndani ya nchi ili kuweza kujitegemea kama nchi katika eneo hilo.

## APR 16, 2025 | FEDHA ZISIZOTUMIKA HADI MWISHO WA MWAKA KURUDI MFUKO MKUU WA SERIKALI

Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb), alilieleza bunge kuwa fedha ambazo hazijatumika hadi mwisho wa mwaka hurudi Mfuko Mkuu wa Serikali ikiwa ni utaratibu wa kusimamia uwajibikaji na uwazi katika matumizi ya fedha zilizotengwa katika bajeti.

Hayo yameelezwa bungeni jijini Dodoma na Waziri wa Fedha Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb), alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Tandahimba Mhe. Katani Ahmad Katani, aliyetaka kujua lini Serikali itarejesha fedha za miradi zilizochukuliwa na Hazina.

Mhe. Dkt. Nchemba, alifafanua kuwa kwa mujibu wa kifungu cha 29 cha Sheria ya Bajeti SURA 439, fedha ambazo hazijatumika

hadi mwisho wa mwaka zinakoma matumizi yake na kurudishwa Mfuko Mkuu wa Serikali.

Aliongeza kuwa iwapo kuna miradi au shughuli ambazo hazijakamilika, Fungu husika linatakiwa kutenga bajeti na kuwasilisha maombi kwa kuambatisha hati za madai au nyaraka za utekelezaji wa miradi hiyo.

Mhe. Dkt. Nchemba alisema kuwa azma ya Serikali ni kuhakikisha kuwa miradi yote inatekelezwa ili kuleta maendeleo kwa wananchi.

## APR 23, 2025 | KAMPUNI ZISIZO JIORODHESHA DSE KUTOFAHAMU THAMANI HALISI YA UWEKEZAJI

Naibu Waziri wa Fedha, Mhe. Hamad Hassan Chande (Mb), alilieleza bunge kuwa Kampuni ambazo hazijaorodheshwa katika Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE) hukutana na changamoto za kutofahamu thamani halisi ya uwekezaji kutokana na kukosekana kwa ukwasi wa hisa zao.

Amesema hayo bungeni jijini Dodoma, alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Geita Mjini, Mhe. Constantine John Kanyasu, aliyetaka kujua hasara na faida kwa kampuni kutotekeleza Sheria ya kujiorodhesha kwenye Soko la Hisa la Dar es Salaam.

Mhe. Chande alisema kuwa Kampuni ambazo hazijajiorodhesha katika Soko la Hisa hutawaliwa na kukosekana kwa uwazi na hivyo Serikali na wanahisa kushindwa kupata taarifa stahiki za mwenendo wa biashara na fedha.



*Kwa mujibu wa Sheria, ni Kampuni ya simu pekee ndio hulazimika kuuza hisa kwa umma na kuorodheshwa katika soko la hisa isipokuwa Kampuni ambazo Serikali ina umiliki wa hisa kwa asilimia 25 au zaidi na Kampuni ambazo zinatoa huduma ya minara ya simu", alisema Mhe. Chande.*

Aidha alizitaja faida za Kampuni kujiorodhesha kwenye Soko la Hisa kuwa ni pamoja na kuongeza mtaji, kuongeza ufanisi na tija, kuiwezesha Serikali kupata mapato stahiki na kutambua thamani halisi ya hisa zake ambapo wanahisa wanapata thamani ya hisa zao wanapotaka kuuza kwa kufuata mwenendo wa soko (demand and supply).

Alisema faida nyingine ni pamoja na kuwapa wananchi fursa ya kununua hisa na hivyo kuwezeshwa kushiriki katika uchumi wa nchi na kutoa fursa kwa wawekezaji wanaotaka kuuza uwekezaji wao wakati wanapohitaji fedha.

## APR 28, 2025 | SERIKALI KUJENGA VITUO SITA VYA FORODHA MWAKA UJAO WA FEDHA

Serikali imesema kuwa ina mpango wa kujenga vituo sita vya forodha mipakani katika mwaka wa fedha ujao wa 2025/26.

Hayo yalisema bungeni jijini Dodoma na Naibu Waziri wa Fedha, Mhe. Hamad Hassan Chande (Mb), alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum, Mhe. Oliver Daniel Semuguruka, aliyetaka kujua mpango wa Serikali wa kuanza ujenzi wa Kituo cha Forodha katika Kijiji cha Mukikoro, Kata ya Mugoma - Ngara.

Mhe. Chande alisema kuwa Serikali imetenga jumla ya shilingi bilioni 1.1 ya ujenzi wa vituo Sita vya forodha kikiwemo kituo cha forodha Mugoma kilichopo Wilaya ya Ngara, mkoani Kagera mpakani mwa Tanzania na Burundi kwa mwaka ujao wa fedha.

## MAY 5, 2025 | BODI YA MICHEZO YA KUBAHATISHA YAAGIZWA KUDHIBITI MICHEZO HARAMU

Naibu Waziri wa Fedha, Mhe Hamad Hassan Chande (Mb), ameliagiza Bodi ya Michezo ya Kubahatisha Tanzania (GBT), kuhakikisha sheria na taratibu za michezo hiyo zinafuatwa ili kulinda maadili ya vijana kwa kuendelea kufanya ukaguzi wa mara kwa mara ufuatiliaji wa karibu wa michezo hiyo.

Agizo hilo alilitoa bungeni jijini Dodoma wakati akijibu swali la Mbunge wa Bagamoyo, Mhe. Muharami Shabani Mkenge, aliyetaka kujua mpango wa Serikali wa kusitisha kutoa vibali vya mashine za kamari ili kupunguza umaskini kwa vijana.

Mhe. Chande alisema kuwa hivi karibuni kumekuwepo na wimbi la waendeshaji mashine za sloti

pasipo kuzingatia Sheria ya Michezo ya Kubahatisha na sheria nyingine za nchi ambapo waendeshaji haramu huweka mashine zao kwenye makazi ya watu, maduka ya bidhaa, maeneo ya vijijini na pia huruhusu watoto chini ya miaka 18 kushiriki kucheza.

> *Ili kukabiliana na michezo ya kubahatisha isiyozingatia Sheria, Bodi ya Michezo ya Kubahatisha imechukua hatua kadhaa ikiwemo, kusitisha utoaji wa leseni kwa waendeshaji wapya wa mashine za sloti na kuanzisha misako na operation ya kusaka waendeshaji haramu wa mashine za sloti nchi nzima kwa kushirikiana na mamlaka nyingine kama Polisi, Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na Uhamiaji",*

Alisema kuwa juhudi nyingine zilizofanywa na Bodi hiyo kukabiliana na changamoto hiyo ni pamoja na kuongeza kaguzi za mara kwa mara maeneo mbalimbali ya nchi ilipo biashara ya mashine za slot na kuendesha kampeni inayowalenga vijana na jamii kufanya kazi za uzalishaji na pindi wanapojihusisha na michezo ya kubahatisha basi wacheze kwa kiasi (Responsible gaming).

Mhe. Chande aliliambia Bunge kuwa Bodi ya Michezo ya Kubahatisha, imeongeza udhibiti wa uingizaji wa mashine za sloti nchini kwenye maeneo ya mipakani kwa kushirikiana na TRA na imeanza mchakato wa kutumia mifumo ya kielektroniki kudhibiti biashara ya mashine za sloti zinazoendeshwa mitaani (route operation) kama ilivyo kwa michezo mingine ya kubahatisha.

Alisema hatua nyingine ni kuingia makubaliano (MoU) na Mamlaka ya Serikali za Mitaa kwa lengo la kuwa na ushirikiano wa karibu wa kudhibiti waendeshaji haramu wa mashine za hizo na kupitia mara kwa mara Sheria ya Michezo ya Kubabatisha kwa lengo la kuondoa kasoro na mianya inayotumiwa na waendeshaji haramu wa mashine za sloti.

Aidha, alisema kuwa Bodi inakusudia kutekeleza hatua hizo kikamilifu ikiwa ni sehemu ya juhudi za kuhakikisha jamii wakiwemo vijana wanalindwa dhidi ya athari hasi za michezo ya kubahatisha ikiwemo umasikini.

## MAY 13, 2025 | MIRADI 80 IPO KATIKA HATUA ZA UTEKELEZAJI KWA UTARATIBU WA PPP

Miradi 80 imewezeshwa na Serikali na ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji kwa utaratibu wa Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPP).

Hayo yamesemwa na Naibu Waziri wa Fedha, Mhe. Hamad Hassan Chande (Mb) bungeni jijini Dodoma wakati akijibu swali la Mbunge wa Mbeya Vijijini, Mhe. Oran Manase Njeza, aliyetaka kujua idadi ya miradi iliyowezeshwa na Serikali kwa utaratibu wa ubia kati ya Serikali na Sekta Binafsi.

Alisema kuwa miradi hiyo ipo katika hatua mbalimbali ambapo miradi mitatu ipo katika hatua ya utekelezaji, miradi minne ipo katika hatua ya majadiliano, miradi miwili ipo katika hatua ya ununuzi, miradi 26 ipo katika hatua ya upembuzi yakinifu, miradi 13 ipo katika hatua ya upembuzi yakinifu wa awali na miradi 32 ipo katika hatua ya andiko dhana.

> *Sheria ya Ubia kati ya Sekta ya Umma na Binafsi (PPP), imeanzisha Mfuko wa Uwezeshaji Ubia (PPP Facilitation Fund – PPPFF), kwa lengo la kuziwezesha Mamlaka za Serikali kuandaa na kutelekeza miradi ya Ubia kati ya Sekta ya Umma na Binafsi (PPP)", alisema Mhe. Chande.*

Aliongeza kwa Sheria hiyo imekipa Kituo cha Ubia (PPP Centre) jukumu la kutoa usaidizi wa kiufundi kwa Mamlaka za Serikali na Sekta Binafsi wakati wa uibuaji, maandalizi na utekelezaji wa miradi ya Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPP).

Akieleza kuhusu ujenzi wa Barabara ya Igawa-Tunduma kwa utaratibu wa PPP, Mhe. Chande alisema kuwa, kwa sasa yupo mshiriki kutoka Sekta binafsi ambae anaandaa mradi huo kupitia utaratibu wa PPP.

Aidha Serikali ya Tanzania na Zambia zipo kwenye majadiliano na Serikali ya China na mwelekeo ni mzuri na wakati wowote Serikali hizo zitaweka saini makubaliano kupitia Kampuni ya China ya CECC kuhusu utekelezaji wa mradi huo.

Mhe. Chande alisema kuwa Serikali inaendelea kuhamasisha sekta binafsi kwa kuwashirikisha katika hatua za uandaaji wa miradi ili waweze kuwa na mchango katika maendeleo ya nchi na sekta hiyo.

## JUN 2, 2025 | SERA ZA WAHISANI HAZINA ATHARI ZA MOJA KWA MOJA ZA KIBAJETI

Serikali imesema kuwa hakuna athari za moja kwa moja za kibajeti kutokana na amri za kimamlaka alizotoa Rais wa Marekani, Dornald Trump za kusitisha misaada kwa Tanzania.

Hayo yalisemwa bungeni jijini Dodoma na Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb), alipokuwa akijibu swali la nyongeza la Mbunge wa Moshi Vijijini, Mhe. Prof. Patrick Alois Ndakidemi, aliyetaka kujua ni kwa kiasi gani amri za kimamlaka alizotoa Rais Dornald Trump wa Marekani za kusitisha misaada Tanzania, zilivyoathiri miradi iliyokuwa inaendelea nchini.

Dkt. Nchemba alisema kuwa Serikali ya Tanzania haikuwa na ushirikiano wa Serikali kwa Serikali kwa masuala ya fedha za miradi ya maendeleo na Serikali ya Marekani kwa kuwa ilikuwa inatumia taasisi zake ambazo zilikuwa zinashirikiana na taasisi za Tanzania.

> *Kwa upande wa taasisi zilizokuwa zinapokea fedha kutoka taasisi za Marekani, tayari Serikali imefanya tathmini si tu kwa tamko la Marekani bali kwa mwenendo wote unaohusisha fedha zinazotoka kwa washirika wa maendeleo na tayari hatua zimeanza kuchukuliwa", alisema Dkt. Nchemba*

Alisema kuwa huko nyuma kulikuwa na fedha za misaada zilizokuwa zinaenda kwenye bajeti kwa ajili ya miradi ya maendeleo lakini kwa sasa Serikali inatekeleza miradi ya maendeleo kupitia fedha za ndani kufidia pengo la miradi ambayo bajeti yake ilikuwa inatoka kwa nchi wahisani.

Dkt. Nchemba alisema kuwa kutokana na yaliyotokea hivi karibuni kuhusu Sera za nje kutoka kwa Wahisani tayari Serikali imepangilia upya matumizi yake kwa bajeti inayoendelea na kupata zaidi ya shilingi bilioni 220 zilizokuwa zinahitajika hasa kwenye maeneo yaliyoonekana kuathirika hususani sekta ya afya ambayo zimepelekwa zaidi ya shilingi bilioni 88 kuendelea na utekelezaji wa miradi.

Alisema kuwa kupitia tathmini iliyofanywa, Serikali itaendelea kutekeleza miradi ya maendeleo ambayo ilikuwa inapata fedha kutoka kwa washirika wa maendeleo ili kuhakikisha miradi ya maendeleo na maisha ya watanzania hayaathiriki kutokana na mabadiliko ya kisera kutoka kwa mbia yeyote wa maendeleo

Akijibu swali la msingi kuhusu namna Serikali ilivyojiandaa kukabiliana na mabadiliko ya Sera za baadhi ya nchi tajiri kulisaidia Taifa kukuza uchumi, Mhe. Dkt. Nchemba alisema Serikali inaendelea na jitihada mbalimbali za kuongeza mapato ya ndani ili kuhakikisha kuwa sehemu kubwa ya bajeti inagharamiwa kwa kutumia mapato ya ndani.

Alisema kuwa kwa kutambua umuhimu wa mahitaji ya kibajeti ikiwemo ugharamiaji wa miradi ya maendeleo, Serikali itaendelea kuvutia ushiriki wa sekta binafsi katika ugharamiaji wa miradi ya maendeleo kwa kutumia njia mbadala ikiwemo ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi.

Dkt. Nchemba alisema kuwa hatua hiyo itasaidia kuipunguzia Serikali mzigo wa kukopa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo na kupunguza utegemezi wa kibajeti kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

## JUNE 25, 2025 | TANZANIA KUTOATHIRIKA MOJA KWA MOJA NA UMOJA WA BRICS

Serikali imesema kuwa Tanzania haitapata athari za moja kwa moja kutokana na mafanikio au changamoto zozote katika Umoja wa BRICS (Brazil, Russia, India, China na Afrika Kusini), zinazoweza kutokea katika sekta ya kiuchumi na fedha hususani ya kujiondoa kwenye Dolarisation kwa kuwa sio nchi mwanachama wa BRICS.

Hayo yalisemwa bungeni jijini Dodoma na Naibu Waziri wa Fedha, Mhe. Hamad Hassan Chande (Mb), alipokuwa akijibu swali la Mheshimiwa Zahor Mohammed Haji (Mwera), aliyeuliza faida na hasara ya Tanzania kutokana na msimamo wa nchi za BRICS ambazo zimejipanga kujiondoa kwenye mfumo wa Dolarisation.

Alisema Serikali ya Tanzania imekuwa na ushirikiano wa muda mrefu na nchi za BRICS (Brazil, Russia, India, China na Afrika Kusini) katika nyanja mbalimbali ikijumuisha masuala ya kiuchumi, biashara na diplomasia kwa kuendelea kuwepo kwa balozi za nchi hizo hapa nchini na Tanzania kuwa na balozi katika nchi hizo.








# MATUKIO YALIYOJIRI



# DKT NCHEMBA AFANYA MAZUNGUMZO NA MKURUGENZI MTENDAJI WA SHIRIKA LA BIMA NCHINI ITALIA | Na. Benny Mwaipaja

Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb) ameishukuru Italia kwa kutoa dhamana ya mkopo wa kujenga Reli ya Kisasa (SGR), kipande cha Kwanza na cha pili kuanzia Dar es Salaam, Morogoro, Dodoma hadi Makutupora mkoani Singida, ambavyo ujenzi wake umekamilika na treni imeanza kutoa huduma kuanzia Dar es salaam hadi Dodoma.

Mhe. Dkt. Nchemba alitoa shukrani hizo mjini Rome nchini Italia, alipokutana na kufanya mazungumzo na Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Bima la Italia (SACE), Bi. Alessandra Ricci.

Alieleza kuwa kutokana na mchango huo, SGR imeanza kutoa huduma ya kubeba abiria kuanzia Julai mwaka 2024, ikiwa ni mafanikio makubwa katika historia ya usafiri nchini, ambapo muda wa safari kati ya Dar es Salaam na Dodoma umepungua kutoka saa nane hadi takriban saa tatu.

Aidha, Mhe. Waziri Nchemba alieleza kuwa Serikali inatambua na kuthamini nia njema ya SACE kuendelea kudhamini ujenzi wa reli toka Dodoma hadi Isaka

Aidha, Dkt. Nchemba aliwaalika wawekezaji kutoka Italia kwenda kuwekeza nchini Tanzania katika sekta mbalimbali ikiwemo uendeshaji wa miundombinu ya reli pamoja na ujenzi wa viwanda vitakavyosaidia kukuza ajira na kukuza uchumi wa nchi wa pande hizo mbili.

Alisema kuwa Tanzania iko katika eneo zuri la kimkakati kijiografia kwa kupakana na nchi 6 zisizopakana na Bahari na zinazotegemea Bandari ya Dar Es Salaam, hatua ambayo inalifanya eneo lote la nchi na nchi jirani kuwa soko zuri na la ukakika la bidhaa na huduma na kuishauri sekta binafsi ya nchi hiyo kuchangamkia fursa hizo.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Bima la Italia, SACE, Bi. Alessandra Ricci, alisema kuwa Italia imeichagua Tanzania kuwa miongoni mwa nchi 14 za Afrika zitakazonufaika na usadizi wa kifedha kutoka nchi hiyo kutokana na uhusiano mzuri wa kiuchumi uliopo kati ya nchi hizo mbili kupitia Mpango wake wa Ushhirikiano kati ya Italia na nchi za Afrika ujulikanao kama Piano Mattei.

Bi. Ricci aliahidi kuwa Shirika lake liko tayari kuendelea kushirikiana na Tanzania katika kugharamia mradi wa SGR kipande cha 3 na 4. kinachoanzia Makutupora mkoani Singida -Tabora hadi Isaka, kutokana na umuhimu wa mradi huo katika kukuza biashara katika ukanda wa Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC).







# SERIKALI YAISHUKURU SINOSURE KWA UDHAMINI WA KIPANDE CHA TANO CHA SGR

Na. Saidina Msangi



Naibu Waziri wa Fedha, Mhe. Hamad Hassan Chande (Mb), ameishukuru Serikali ya China kupitia Shirika lake la Bima  SINOSURE, kwa kudhamini mkopo wa kibiashara kwa ajili ya ujenzi wa kipande cha tano (lot 5) cha Reli ya Kisasa (SGR) kutoka Isaka hadi Mwanza chenye thamani ya dola za Marekani milioni 559, kupitia mkataba uliosainiwa Oktoba 21, 2024.

Shukrani hizo alizitoa wakati wa kikao cha majadiliano kati ya Ujumbe wa Tanzania ulioongozwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji Mhe. Prof. Kitila Alexander Mkumbo (Mb) na Ujumbe wa China ulioongozwa na Naibu Waziri wa Biashara wa Jamhuri ya Watu wa China, Mhe. Tang Wenhong, yaliyofanyika katika Hoteli ya Johari Rotana, jijini Dar es Salaam.

Pamoja na shukrani hizo, Mhe. Chande aliiomba China kuangalia uwezekano wa Kampuni ya Bima ya SINOSURE kushiriki katika ujenzi wa Kipande cha Sita cha Reli ya Kisasa kutoka Tabora hadi Kigoma chenye makadirio ya gharama ya dola bilioni 2.3.



> *Fedha za kukamilisha mradi wa ujenzi wa Reli kutoka Tabaora hadi Kigoma zinatarajiwa kutoka katika vyanzo mbalimbali ambapo, dola bilioni 1.1 zinatarajiwa kutoka kwa Taasisi za Fedha za Maendeleo (DFIs), ambapo SINOSURE ni miongoni mwa wadhamini", alisema Mhe. Chande.*

Aidha, Mhe. Chande alisema kuwa ushirikiano wa Tanzania na China umewezesha Serikali ya China kufanikisha upatikanaji wa dola za Marekani milioni 108.6 kwa ajili ya Mradi wa Kuongeza Wigo wa Mawasiliano Vijijini Awamu ya Kwanza na Dola milioni 270.3 kwa ajili ya Mradi wa Usafirishaji Umeme wa 400 kV kutoka Dar es Salaam hadi Arusha, awamu ya kwanza.



Mhe Chande aliongeza kuwa uchumi wa nchi unaendelea kuimarika kutokana na uwekezaji katika miundombinu, utulivu wa uchumi jumla, mfumuko mdogo wa bei na mazingira bora ya uwekezaji.

Kwa Upande wake Naibu Waziri wa Biashara wa Jamhuri ya Watu wa China, Mhe. Tang Wenhong, alisema kuwa Serikali ya China itaendelea kuimarisha mahusiano ya kiuchumi na kidiplomasia kati ya nchi hizo mbili kwa manufaa ya wananchi wa pande hizo mbili.





# FITCH YAITHIBITISHA TANZANIA KUWA NA MTAZAMO THABITI 'B+' KWENYE TATHMINI YA NCHI KUKOPESHEKA KATIKA MASOKO YA MITAJI YA KIMATAIFA (SOVEREIGN CREDIT RATING)

Na. Joseph Mahumi

Kampuni ya Kimataifa inayojihusisha na kufanya tathmini ya nchi kukopesheka katika masoko ya mitaji ya kimataifa ya Fitch Ratings, imeithibitisha Tanzania (Long-Term Foreign-Currency Issuer Default Rating – IDR) kuwa katika daraja la 'B+' ikiwa na Mtazamo Thabiti (Stable Outlook), jambo linalodhihirisha kuendelea kwa imani ya kimataifa juu ya misingi ya uchumi wa Tanzania na juhudi zake za mageuzi katika sera zake.

Kupitia taarifa yao waliyochapisha hivi karibuni, imesema uthibitisho huo umechangiwa na ukuaji imara wa Pato la Taifa (GDP), mfumuko mdogo wa bei, usimamizi mzuri wa sera za uchumi pamoja na kuimarisha ushirikiano na taasisi za kimataifa.

Kampuni ya Fitch inatarajia uchumi wa Tanzania utakua kwa asilimia 5.9 mwaka 2025, ukichochewa na sekta za kilimo, madini, utalii pamoja na na uwekezaji katika miundombinu kama mradi wa reli ya kisasa (SGR) na mradi wa umeme wa Mwalimu Nyerere.

Tanzania imepongezwa kwa kudhibiti mfumuko wa bei, ambao umebaki ndani ya lengo la Benki Kuu ya Tanzania la asilimia 3 hadi 5, na kwa kuboresha usimamizi wa fedha za umma, ambapo madeni yaliyokuwa yakisubiri kulipwa kwa wazabuni na marejesho ya VAT yamepungua kutoka asilimia 1.2 ya GDP mwaka 2022 hadi asilimia 0.4 kufikia Machi 2025.

Fitch pia imeeleza kuwa kupitia matokeo hayo, wanatarajia mwelekeo wa sera kuendelea kuwa thabiti chini ya uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan, jambo litakaloendelea kuwavutia washirika wa maendeleo na wawekezaji nchini.

Ripoti hiyo inaeleza pia kuwa, Tanzania imeweza kudumisha akiba ya fedha za kigeni, ambapo hadi Machi 2025 ilifikia Dola za Marekani bilioni 5.7, sawa na uwezo wa kulipia uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa miezi 4.2.

Aidha, Fitch imeeleza kuwa kuongezeka kwa akiba ya fedha za kigeni, kuendeleza utekelezaji mzuri wa sera za uchumi na kuendelea kuvutia wawekezaji wa sekta binafsi kunaweza kuiwezesha Tanzania kupandishwa daraja zaidi.



# WIZARA YA FEDHA YATOA ELIMU YA USIMAMIZI WA MNYORORO WA UGAVI KWA WAHARIRI WA VYOMBO VYA HABARI

Na. Josephine Majura na Joseph Mahumi





Serikali kupitia Wizara ya Fedha, imefanya mafunzo kwa Wahariri wa Vyombo vya Habari kwa lengo la kuwajengea uelewa kuhusu masuala ya usimamizi wa mnyororo wa ugavi katika sekta ya umma.

Akizungumza wakati akifungua rasmi mafunzo hayo, kwa niaba ya Katibu Mkuu Wizaravya Fedha, Dkt. Natu El-maamry Mwamba, Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha, Bi. Jenifa Christian Omolo, alisema kuwa mafunzo hayo ni sehemu ya utekelezaji wa programu shirikishi kati ya Wizara ya Fedha na wadau wake ikiwemo Sekta ya Habari, yenye lengo la kufikisha elimu sahihi kwa jamii kupitia wanahabari.

> *Mafanikio tunayoyaona katika usimamizi wa rasilimali za umma na thamani ya pesa katika miradi ya maendeleo yanaonesha kazi kubwa na juhudi zinazofanywa na wakaguzi wa ndani kutoka katika taasisi za Serikali. Juhudi hizi zinapaswa kuendelezwa kwa kasi zaidi ili nchi yetu iendelee kupiga hatua zaidi za maendeleo chini ya Uongozi wa Serikali ya Awamu ya Sita ya Rais Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan", alisema Bi.Omolo.*

Alisisitiza kuwa, mafunzo hayo yanatoa fursa kwa wanahabari kupata maarifa ya kina kuhusu shughuli zote muhimu zinazounda mnyororo wa ugavi kama vile ununuzi, usambazaji, uhifadhi, matumizi na uondoshaji wa bidhaa na huduma ndani ya taasisi za Serikali.

Bi. Omollo alifafanua kuwa, mafunzo hayo yanalenga kuwahusisha moja kwa moja wanahabari ili kusaidia kutoa taarifa sahihi, za wakati na zenye kuelimisha wananchi katika eneo la mnyororo wa ugavi kwa kuwa Serikali imekuwa ikitumia fedha nyingi katika kuhakikisha wananchi wanahudumiwa kikamilifu kupitia mnyororo wa ugavi.

> *kwa mfano, zaidi ya asilimia 70 ya Bajeti ya Serikali ya 2024/25 ya shilingi trilioni 50.29, shilingi trilioni 35.2 zinatumika katika kununua vifaa na vitendeakazi mbalimbali, kulipia kandarasi za ujenzi na pia huduma ambazo zinawafikia wananchi walaji" alisisitiza Bi. Omolo.*

Aliwasihi Wahariri na wanahabari kwa ujumla kulitumia jukwaa hilo kama fursa muhimu ya kujifunza, kujadili na kubadilishana uzoefu, na pia ushauri juu ya masuala ya usimamizi wa shughuli za mnyororo wa ugavi, ili kujiweka katika nafasi nzuri sana ya kuhabarisha umma kwa usahihi kupitia vyombo vyenu vya Habari.

Naye Kamishna wa Idara ya Sera za Ununuzi wa Umma, Wizara ya Fedha, Dkt. Frederick Mwakibinga, alisema kuwa kupitia kalamu za wanahabari, sauti, picha, na majukwaa mbalimbali ya vyombo vya habari, elimu kuhusu nafasi na mchango wa mnyororo wa ugavi katika maendeleo ya Taifa itafanikiwa kwa kiasi kikubwa.

Alifafanua kuwa mnyororo wa ugavi unaanzia katika upangaji wa mahitaji, ununuzi, ugomboaji na uondoshaji, upokeaji, uhifadhi, usambazaji, hadi matumizi na uondoshaji wa bidhaa, vifaa au huduma.



Dkt. Mwakibinga alisema kuwa, kukosekana kwa usimamizi madhubuti katika hatua yoyote kati ya hizo kunaweza kusababisha hasara kubwa kwa Serikali, upotevu wa rasilimali, au huduma duni kwa wananchi.

*Wizara ya Fedha kupitia Idara ya Sera za Ununuzi wa Umma na Kitengo cha Mawasiliano Serikalini tutaendelea kushirikiana nanyi kwa lengo mahsusi la kutoa uelewa mpana kuhusu shughuli za mnyororo wa ugavi kwa wadau muhimu wa mawasiliano kwa umma, ninyi Wahariri na waandishi wa habari", alisema Dkt. Mwakibinga.*

Naye Mwenyekiti wa Wahariri wa Vyombo vya Habari katika mafunzo hayo, Bw. Ben Mwang'onda, aliishukuru Wizara ya Fedha kwa kuandaa mafunzo hayo ambayo yatakua daraja la mahusiano kati ya Wizara hiyo na Umma katika kutoa taarifa kuhusu Mnyororo wa Ugavi.

*Kupitia mafunzo haya, tunaweza kufikisha taarifa sahihi kwa wananchi, jambo ambalo linasaidia kuongeza uelewa wa umma na kuhamasisha uwajibikaji serikalini," alisema Bw. Mwang'onda.*



Kwa upande wake Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini Wizara ya Fedha, Bw. Benny Mwaipaja, alisema kuwa Ushirikiano kati ya Wizara na Wanahabari umeendelea kuwa thabiti na imara na unaashiria matokeo mazuri ya elimu kwa umma.

*Tunaimani mafunzo haya ni mwendelezo wa Wizara wa kuangazia njia mbalimbali za kuelemisha umma kuhusu sera, program na matukio mbalimbali yanayofanywa na Wizara na niwasihi muendelee kushirikiana nasi ili kufikisha yale yanayofanywa na Serikali kwa wananchi" alisema Bw. Mwaipaja.*





# SH. TRILIONI 56.49 KUTEKELEZA BAJETI KUU YA SERIKALI 2025/26

Na. Saidina Msangi

Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb), aliwasilisha Hotuba ya Bajeti Kuu ya Serikali, ambapo ameliomba Bunge ridhaa ya kukusanya na kutumia jumla ya shilingi trilioni 56.49 kwa Mwaka wa Fedha 2025/26.

Dkt. Nchemba aliomba ridhaa hiyo bungeni jijini Dodoma, wakati akiwasilisha mapendekezo ya Serikali kuhusu makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka 2025/26, ambapo bajeti hiyo inatarajiwa kugharamiwa na mapato ya ndani ya shilingi trilioni 40.47, misaada shilingi trilioni 1.07 na mikopo ya shilingi trilioni 14.95.

Kati ya mapato ya ndani yanayotarajiwa, mapato ya kodi ni shilingi trilioni 32.31, mapato yasiyo ya kodi shilingi trilioni 6.48, na mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa shilingi trilioni 1.68. Aidha, mikopo inajumuisha shilingi trilioni 6.27 kutoka vyanzo vya ndani na shilingi trilioni 8.68 kutoka vyanzo vya nje




Alieleza kuwa makadirio ya matumizi ya Serikali ya shilingi trilioni 56.49 kwa mwaka 2025/26 yanajumuisha Stahiki za watumishi na michango ya pensheni (Serikali Kuu) shilingi trilioni 9.17 pamoja na ununuzi wa bidhaa na huduma shilingi trilioni 5.58.

Aliongeza kuwa matumizi mengine ni malipo ya riba za mikopo shilingi trilioni 6.49; na ruzuku kwa taasisi za Serikali, mashirika ya umma na Mamlaka za Serikali za Mitaa shilingi trilioni 22.17 na shilingi trilioni 7.72 kugharamia malipo ya mtaji kwa deni la ndani na nje.

> *Katika Mwaka wa Fedha 2025/26 Serikali inatarajia kuongeza kasi ya ukuaji wa Pato Halisi la Taifa kufikia asilimia 6.0 mwaka 2025 kutoka ukuaji wa asilimia 5.5 mwaka 2024, kuendelea kudhibiti kasi ya mfumuko wa bei na kuhakikisha kuwa unabaki kwenye wigo wa tarakimu moja ya wastani wa asilimia kati ya 3.0 - 5.0 katika muda wa kati", alifafanua Mhe. Nchemba.*

Aidha, Dkt. Nchemba alisema Serikali inatarajia kuongeza Mapato ya ndani kufikia asilimia 16.7 ya Pato la Taifa mwaka 2025/26 ikilinganishwa na asilimia 15.8 mwaka 2024/25 na mapato ya kodi kufikia asilimia 13.3 ya Pato la Taifa mwaka 2025/26 kutoka asilimia 12.8 mwaka 2024/25.

Dkt. Nchemba alisema vipaumbele vya bajeti ya mwaka 2025/26 ni pamoja na kuendelea kutekeleza na kukamilisha miradi ya kielelezo na ile ya kimkakati, kuimarisha sekta za uzalishaji zenye matokeo chanya katika kukuza uchumi, kuimarisha rasilimali watu hususan katika sekta za huduma za jamii na kuboresha mazingira ya ufanyaji biashara na uwekezaji nchini ili kuvutia ushiriki wa sekta binafsi katika shughuli mbalimbali za kiuchumi.

Aliongeza kuwa, Maeneo mengine mahsusi ya vipaumbele ni pamoja na ugharamiaji wa Deni la Serikali; mishahara na stahiki za watumishi wa umma, pamoja na ujenzi na ukarabati wa viwanja vya michezo kwa ajili ya maandalizi ya michuano ya AFCON 2027. Aidha, nipende kuwafahamisha Watanzania kuwa Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025 tutaugharamia kwa fedha zetu za ndani.

Aidha, Dkt. Nchemba alisema katika mwaka 2025/26, Serikali itaendelea kuchukua hatua mbalimbali za kuimarisha ukusanyaji wa mapato ikiwemo kuendelea kuhamasisha umma kuhusu kutoa na kudai risiti za malipo za kielektroniki za EFD na kuboresha utaratibu wa ukusanyaji wa mapato kutoka vyanzo vinavyosimamiwa na mamlaka za udhibiti.

*"Serikali itaendelea kuboresha Mfumo wa TAUSI ili kuhakikisha vyanzo vyote vya mapato vya Mamlaka za Serikali za Mitaa vinajumuishwa katika mfumo huo, kuongeza ufanisi wa mifumo ya ukusanyaji wa mapato ya mashirika, taasisi za umma na wakala za Serikali ili kuhakikisha gawio na michango stahiki inawasilishwa kwa wakati na kuendelea kutekeleza Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Biashara na Uwekezaji (MKUMBI)", alifafanua Mhe. Nchemba.*

## MABORESHO YA KODI

Dkt. Nchemba alisema Serikali inalenga kufanya maboresho ya mfumo wa kodi, ikiwemo baadhi ya viwango vya kodi, tozo na ada zinazotozwa chini ya sheria mbalimbali pamoja na kuboresha taratibu za ukusanyaji na usimamizi wa mapato ya Serikali ili kuwa na mfumo wa kodi ambao ni tulivu na wa kutabirika unaolenga kuchochea shughuli mbalimbali za uzalishaji mali ndani ya nchi.

Mapendekezo ya kurekebisha mfumo wa kodi kwa mwaka 2025/26 yanatarajiwa kuiongezea Serikali jumla ya shilingi milioni 4,260,023.77 ambapo baadhi ya mapendekezo hayo ni kusamehe kodi ya ongezeko la thamani kwenye viuatilifu vinavyotambulika kwa HS Codes 3808.61.00, 3808.62.00 na 3808.69.00, ili kuwapa unafuu wakulima ya kupata dawa za kuua wadudu mashambani na hivyo kuongeza uzalishaji wa mazao nchini.

Kusamehe kodi ya ongezeko la thamani kwenye miamala ya ununuzi wa bima mtawanyo inayofanywa baina ya kampuni za bima na zile za bima mtawanyo ili kuongeza ushindani wa kampuni za ndani, kukuza Sekta ya Bima na kuhamasisha matumizi ya bima katika kukabiliana na majanga nchini.

Kutoza kodi ya ongezeko la thamani kwa kiwango cha asilimia 0 kwenye bidhaa za nguo zinazotengenezwa kwa kutumia pamba inayolimwa nchini kwa kipindi cha mwaka mmoja ili kuleta unafuu kwa wakulima wa pamba na viwanda vinavyotengeneza nguo nchini.

Kutoza kodi ya ongezeko la thamani kwa kiwango cha asilimia 0 kwenye mbolea inayozalishwa ndani ya nchi kwa kipindi cha miaka mitatu ili kuleta unafuu kwa wakulima na walaji hasa katika kipindi hiki ambacho dunia imetoka kwenye mdororo wa kiuchumi duniani.

Kusamehe kodi ya ongezeko la thamani kwenye mafuta ya kula yanayozalishwa ndani ya nchi kwa kutumia mbegu zinazozalishwa nchini kwa muda wa mwaka mmoja ili kuendelea kuleta unafuu wa bei ya mafuta ya kula nchini.



Kufuta Msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani unaotolewa kwenye ununuaji na uingizaji wa gaming supply. Hatua hii inalenga kuleta usawa katika utozaji wa kodi kwa kuwa michezo mingine kama vile mpira wa miguu ipo katika wigo wa utozaji wa kodi ya ongezeko la thamani. Hatua hii inatarajiwa kuongeza mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi milioni 322,022.5.

Kuweka sharti la msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani kwenye matairi ya trekta yanayotumika kwenye shughuli za kilimo yanayotambulika kwa HS Code 4011.70.00; dam liners zinazotambulika kwa Heading 39.20; forks (HS Code 8201.90.00); reki (HS Code 8201.30.00); na shoka (HS Code 8201.40.00) kutolewa baada ya kupata ridhaa ya Waziri mwenye dhamana ya masuala ya kilimo.

Kufuta msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani kwenye lami zinazotambulika kwa HS Code 2713.20.00 na 2715.00.00 ili kuendana na azma ya Serikali ya kupunguza misamaha isiyo na tija ili kulinda mapato ya Serikali na kupunguza matumizi yanayohusiana na utoaji wa misamaha ya kodi. Hatua hii inatarajiwa kuongeza mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi milioni 85,606.2.

Kusamehe kodi ya ongezeko la thamani kwenye magazeti yanayozalishwa nchini pekee ili kupunguza gharama za magazeti hayo na hivyo kuwezesha upatikanaji wa taarifa muhimu. Hatua hii inatarajiwa kuongeza mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi milioni 1,274.4.

Kusamehe kodi ya ongezeko la thamani kwenye gesi asilia inayouzwa kwenda kwenye vituo vya kushindilia gesi kwa ajili ya matumizi ya magari ili kuweka unafuu kwa wawekezaji, kuvutia uwekezaji wa vituo vya kusambazia gesi asilia iliyosindikwa kwenye magari na kupunguza utegemezi wa mafuta na uzalishaji wa hewa ya ukaa.

Kusamehe kodi ya ongezeko la thamani kwenye matanki na mitungi ya gesi ya kupikia zinazotambulika kwa HS Code 7311.00.10 pamoja na mitambo ya kuondoa hewa ukaa yenye HS Code 8417.80.00 inayotumika katika uzalishaji wa mikaa mbadala. Hatua hii inalenga kupunguza gharama za upatikanaji wa bidhaa hizi ili kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia nchini.

Kujumuisha masoko mtandao na huduma za masoko za kimtandao kwenye wigo wa tafsiri ya neno wakala wa huduma za kimtandao ili kutanua wigo wa kodi kwa kuweka ufafanuzi utakaopelekea kutatua changamoto zilizopo katika utozaji na usimamizi wa kodi ambapo tafsiri iliyopo sasa haijumuishi huduma hizo katika utozaji kodi. Hatua hii inatarajia kuongeza mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi milioni 116,073.4.

Kuweka unafuu wa kutoza kodi ya mapato kwa kundi la pikipiki ya miguu miwili, pikipiki ya miguu mitatu (Bajaji) na magari ya kubeba mizigo yenye uzito usiozidi Kilogramu 500 ikiwemo Guta kwa kuweka utaratibu mpya wa kukadiria kodi ya mapato kwenye vyombo hivyo. Maboresho ya viwango vya kodi elekezi yanalenga kuweka unafuu wa kodi kwa kundi husika na hivyo kurahisisha utekelezaji wa sheria.

Kupunguza tozo ya ushuru wa huduma kutoka utaratibu wa sasa wa kutoza kiwango kisichozidi asilimia 0.3 ya pato ghafi kwenda kiwango mfuto cha asilimia 0.25 ya pato ghafi. Lengo la hatua hii ni kupunguza gharama za ufanyaji biashara na uwekezaji nchini pamoja na kuendana na masharti ya Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Biashara (MKUMBI).

Kupunguza kiwango cha ada ya ushuru wa hoteli (hotel levy) kutoka asilimia 10 hadi asilimia 2. Lengo la hatua hii ni kupunguza gharama za ufanyaji biashara na uwekezaji nchini.

Kufuta ada za upakiaji (loading) na upakuaji (offloading) zinazotozwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa zinazohusiana na usafirishaji wa mizigo. Lengo la hatua hii ni kupunguza gharama za ufanyaji biashara na uwekezaji nchini ili kuendana na masharti ya Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Biashara nchini (MKUMBI).

Kupunguza ada ya usajili wa pikipiki za biashara kutoka shilingi 340,000 hadi shilingi 170,000 kwa miaka mitatu ambapo ada husika italipwa wakati wa usajili wa awali pekee. Kupunguza ada ya leseni ya uendeshaji wa pikipiki, bajaji na guta kutoka shilingi 70,000 hadi shilingi 30,000.

## KUGHARAMIA BIMA YA AFYA

Serikali imeanzisha vyanzo mbadala vya mapato ili kupunguza nakisi ya kibajeti kwa kufanya marekebisho katika sheria mbalimbali. Aidha inapendekezwa asilimia 70 ya mapato yatakayoongezeka ipelekwe kwenye Mfuko wa Udhamini wa Kudhibiti UKIMWI (ATF) na asilimia 30 ipelekwe kwenye Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya kwa Wote. Marekebisho hayo ni kama ifuatavyo:

Kufanya marekebisho ya Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, SURA 147 ili kuongeza ushuru wa bidhaa kwenye vinywaji vya kilevi vinavyozalishwa na vinavyoingizwa kutoka nje ya nchi kama ifuatavyo: shilingi 20 kwa bia zinazotambulika kwa Heading 22.03; shilingi 30 kwa mvinyo unaotambulika kwa Heading 22.04, 22.05, na 22.06; shilingi 50 kwa spirits na vinywaji vingine vinavyotambulika kwa Heading 22.08.

Kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, SURA 147 ili kuongeza kiwango cha ushuru wa bidhaa kwenye huduma za mawasiliano ya kielektroniki kutoka asilimia 17 hadi asilimia 17.5.

Kufanya marekebisho ya Sheria ya Ushuru wa Barabara na Mafuta, SURA 220 ili kutoza kiasi cha shilingi 10 kwa kila lita ya mafuta ya Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa pamoja na kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Madini, SURA 123 ili kutoza kiwango cha asilimia 0.1 kwenye thamani ya soko ya madini.

Kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Michezo ya Kubahatisha, SURA 41 ili kuongeza kiwango cha kodi kwenye zawadi ya ushindi (Winning tax) kwenye michezo ya kubashiri matokeo (sports betting) kutoka asilimia 10 hadi asilimia 15; na kwenye michezo ya kasino ya ardhini (land based casino) kutoka asilimia 12 hadi asilimia 15.

Kutoza shilingi 500 kwa kila tiketi inayotolewa na mtoa huduma za usafirishaji kwa njia ya treni na kutoza shilingi 1000 kwa kila tiketi inayotolewa na mtoa huduma za usafirishaji kwa njia ya anga. Hatua hizi kwa pamoja zinatarajiwa kuongeza mapato ya Serikali kwa shilingi milioni 586,404.9.

Kutoza magari na mashine (heavy machines) zinazoingizwa kutoka nje ya nchi kama ifuatavyo: Shilingi 50,000 kwa magari yenye ukubwa wa injini (CC) kati ya 0 -1000; Shilingi 100,000 kwa magari yenye ukubwa wa injini (CC) kuanzia 1001-1500; Shilingi 150,000 kwa magari yenye ukubwa wa injini (CC) kuanzia 1501-2500; Shilingi 200,000 kwa magari yenye ukubwa wa injini (CC) kuanzia 2501 na zaidi; Shilingi 250,000 kwa mashine (Excavators, Bulldozers, Fork Lifts) zenye Heading 84.29 na 84.27.

## KUBORESHA MAZINGIRA YA BIASHARA

Ili kuiwezesha nchi kuwa na sera bora za biashara na kuweka mazingira mazuri ya ufanyaji biashara baina ya wazawa na wageni, Serikali inatarajia kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Utoaji wa Leseni za Biashara ikiwemo:

Kufuta kifungu cha 3(4) kinachozipa nguvu mamlaka za utoaji wa leseni za biashara kufunga biashara pale ambapo wafanyabiashara wamekiuka masharti ya Sheria husika. Lengo la hatua hii ni kuwaondolea kero wafanyabiashara na pia kutekeleza maelekezo ya Serikali ya kutofunga biashara.

Kuongeza kifungu cha 8(7) ambacho kinampa mamlaka Waziri mwenye dhamana na masuala ya biashara kuainisha shughuli za kibiashara ambazo hazipaswi kufanywa na wageni. Utaratibu wa utekelezaji wa kifungu hiki utafanywa kupitia Amri (Order) itakayotolewa na Waziri ambayo itakua na orodha ya shughuli za kibiashara ambazo hazipaswi kufanywa na wageni.

Dkt. Nchemba alisema bajeti hii inaendeleza na kukamilisha utekelezaji wa miradi, Kuchochea uchumi shindani na shirikishi, kuimarisha uzalishaji wa bidhaa viwandani na utoaji huduma, kukuza uwekezaji na biashara, kuchochea maendeleo ya watu na kuendeleza rasilimali watu ili kuhakikisha ufikiwaji wa malengo ya Dira 2025.



# BI. OMOLO ASISITIZA WAKAGUZI WA NDANI KUZINGATIA UADILIFU KATIKA UTENDAJI KAZI

Na. Saidina Msangi

Watumishi wa Idara ya Mkaguzi wa Ndani Mkuu wa Serikali wamehimizwa kuendelea kufanya kazi kwa uadilifu, uaminifu na kujituma kwa kuwa ni daraja muhimu kati ya usimamizi wa fedha za umma na mafanikio ya maendeleo ya wananchi.

Rai hiyo imetolewa na Naibu Katibu Mkuu anayesimamia Huduma za Hazina, Wizara ya Fedha, Bi. Jenifa Christian Omolo, wakati akifungua Mkutano wa Watumishi wa Idara hiyo uliofanyika katika ukumbi wa Olasite Garden, jijini Arusha.

Alisema mkaguzi wa ndani si tu mtathmini wa taarifa za kifedha, bali ni mshauri wa usimamizi bora, anayechangia kwa kiasi kikubwa katika kuhakikisha taasisi zinafanya kazi kwa ufanisi, uwazi na kwa kuzingatia misingi ya sheria, taratibu na kanuni.

*Mafanikio tunayoyaona katika usimamizi wa rasilimali za umma na thamani ya pesa katika miradi ya maendeleo yanaonesha kazi kubwa na juhudi zinazofanywa na wakaguzi wa ndani kutoka katika taasisi za Serikali. Juhudi hizi zinapaswa kuendelezwa kwa kasi zaidi ili nchi yetu iendelee kupiga hatua zaidi za maendeleo chini ya Uongozi wa Serikali ya Awamu ya Sita ya Rais Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan", alisema Bi.Omolo.*

Aidha, Bi. Omolo aliwasisitiza kuhusu umuhimu wa kuweka mikakati madhubuti ya kudhibiti mianya ya upotevu wa fedha, kutambua mapema maeneo yenye viashiria hatarishi, na kutoa mapendekezo yanayotekelezeka kwa wakati.



Aliongeza kuwa Serikali itaendelea kuthamini mchango wao na itaendelea kuweka mazingira bora ya kazi kwa kuhakikisha wanapata mafunzo, vifaa na msaada unaohitajika ili kutimiza majukumu yao kwa weledi.

Pia Bi. Omolo aliwasisitiza kuweka mikakakati ya kuhakikisha upatikanaji wa rasilimali zinazohitajika kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu ikiwa ni pamoja na kutoa mafunzo ya mara kwa mara kwa wakaguzi ili kuwajengea uwezo wa kukabiliana na mabadiliko ya teknolojia.

Akizungumza wakati wa kumkaribisha mgeni rasmi Mkaguzi wa Ndani Mkuu wa Serikali, Bw. Benjamin Magai alisema kuwa lengo la mkutano huo ni kujadili utekelezaji wa majukumu ikiwemo mafanikio na changamoto ili kuangalia namna ya kuboresha utendaji kazi.







*"Katika kutekeleza shughuli zetu kuna mafanikio ambayo tumeyapata ikiwemo usimamizi wa taasisi za umma kuona utendaji kazi wao na kutoa uelewa kwa taasisi mbalimbali kuhusu usimamizi wa vihatarishi, kufanya uthibiti katika taasisi mbalimbali, kufanya kaguzi za kiufundi na ufanisi na kaguzi maalumu", alisema Bw. Magai.*



# TANZANIA NA JAMHURI YA CZECH ZASAINI MKATABA WA KUONDOA UTOZAJI KODI YA MAPATO MARA MBILI NA KUZUIA UKWEPAJI WA KODI

Na. Joseph Mahumi

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Czech zimetia saini Mkataba wa Kuondoa Utozaji Kodi ya Mapato Mara Mbili na Kuzuia Ukwepaji Kodi, hatua itakayosaidia kufungua uchumi wa nchi kwa kuvutia uwekezaji wa kimataifa na utawezesha wawekezaji na wafanyabiashara wanaofanya shughuli kati ya Tanzania na Czech.

Mkataba huo ujulikanao kama Agreement on the Avoidance of Double Taxation and Prevention of Fiscal Avoidance and Evasion in Respect to Tax on Income, umesainiwa na Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb), kwa niaba ya Tanzania, na Balozi wa Jamhuri ya Czech nchini Tanzania mwenye makazi yake ya kudumu nchini Kenya, Mhe. Nicol Adamcová, kwa niaba ya Serikali ya Jamhuri ya Czech, katika hafla iliyofanyika Ofisi Ndogo za Wizara ya Fedha, jijini Dar es Salaam.

Akizungumza baada ya kusaini mkataba huo, Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb), alisema kuwa mkataba huo utasaidia kuondoa hatari ya kipato kilekile kutozwa kodi mara mbili katika nchi mbili tofauti, kuhamasisha sera za haki za kikodi, na kuimarisha imani ya wawekezaji.



*Mkataba huu ni hatua muhimu katika jitihada za Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, katika kufungua uchumi wa nchi kwa kuvutia uwekezaji wa kimataifa na utawezesha wawekezaji na wafanyabiashara wanaofanya shughuli kati ya Tanzania na Czech" alisema Dkt. Nchemba.*

Aliongeza kuwa Takwimu za Shirika la Ushirikiano wa Kiuchumi na Maendeleo (OECD) zinaonesha kuwa nchi zilizo na mikataba madhubuti ya kuepusha kodi ya maradufu huvutia hadi asilimia 30 zaidi ya uwekezaji wa moja kwa moja kutoka nje, ikilinganishwa na zile zisizo na mikataba hiyo.

*kupitia Mkataba huu tunatarajia kuvutia mitaji mikubwa kutoka Czech kuja kuwekeza Tanzania, hususan katika sekta za kutengeneza magari na ndege, vifaa vya umeme, mitambo na mashine mbalimbali na kupitia uwekezaji huo, Tanzania inatarajia kunufaika na ukuaji wa sekta za uzalishaji, maendeleo ya viwanda, na kuongezeka kwa ajira kwa wananchi" alisema Mhe. Dkt. Nchemba.*

Kwa upande wake Balozi wa Jamhuri ya Czech nchini Tanzania mwenye makazi yake nchini Kenya, Mhe. Nicol Adamcová, alisema kuwa ushirikiano kati ya Tanzania na Czech ni wa muda mrefu na wenye tija, hivyo kusainiwa kwa mkataba huo utawapa fursa kwa wawekezaji wa Kitanzania kuwekeza nchini Czech bila vizuizi vya kikodi.

Aliongeza kuwa makubaliano hayo ni muhimu na ni ushahidi muhimu wa utulivu wa mazingira na hali ya biashara katika nchi hizi mbili.


Kwa mujibu wa takwimu za UN COMTRADE, mwaka 2022 biashara baina ya Tanzania na Czech ilifikia takribani dola milioni 16.2 za Kimarekani, hasa katika sekta za mitambo, vifaa vya umeme, teknolojia za usafirishaji, na bidhaa za kilimo. Mkataba huu unatarajiwa kuongeza zaidi kiwango cha biashara na uwekezaji kati ya pande hizo mbili.







*Nina furaha kubwa kuwa tumetia saini mkataba huu na ni jambo muhimu, ni kipengele cha msingi kinachoonyesha kuwa kuna kiwango cha juu cha kuaminiana kati ya nchi zetu mbili, kama isingekuwa hivyo, tusingetumia muda na nguvu kujadiliana kuhusu" alisema Mhe. Adamcová.*



# SERIKALI YASISITIZA MATUMIZI YA MIFUMO RASMI YA KIFEDHA KUKUZA UCHUMI WA MWANANCHI

Na. Josephine Majura na Chedaiwe Msuya

Serikali imewataka Waratibu wa Huduma Ndogo za Fedha nchini kuongeza kasi, ubunifu na weledi katika kutoa elimu kwa wananchi kuhusu matumizi sahihi ya mifumo rasmi ya kifedha inayotambulika na kusimamiwa na Serikali ili kuhakikisha wanapata maarifa yatakayowawezesha kujikwamua kiuchumi kwa njia salama na endelevu.

Agizo hilo limetolewa na Kamishna wa Idara ya Uendelezaji Sekta ya Fedha, Wizara ya Fedha, Dkt. Charles Mwamwaja, wakati akufungua mafunzo maalum kwa Waratibu wa Huduma Ndogo za Fedha kutoka ngazi ya Wizara, Mikoa na Halmashauri, yaliyolenga kuwawezesha waratibu hao kutoa elimu sahihi kwa jamii wanazozihudumia.

Dkt. Mwamwaja alisisitiza umuhimu wa kutumia mafunzo hayo kama jukwaa la kubadilishana mawazo, uzoefu na mbinu bora za kukabiliana na changamoto zinazowakabili waratibu hao katika utekelezaji wa majukumu yao.



*Maarifa haya msiyabakize kwenye makabrasha, pelekeni kwa wananchi waelimisheni waelewe faida ya kutumia mifumo rasmi ya kifedha kama benki, SACCOS, VICOBA vilivyosajiliwa na taasisi zingine zilizo chini ya uangalizi wa Serikali kwa kuwa ndiyo njia salama ya kuwasaidia kuinuka kiuchumi," alisema Dkt. Mwamwaja.*

Aliongeza kuwa mafanikio ya sekta hiyo hayategemea tu uwepo wa Sera, Sheria na Kanuni nzuri, bali yanategemea zaidi utekelezaji



wenye tija, weledi, uwajibikaji na ufuatiliaji makini unaoanzia kwa Waratibu wa Huduma Ndogo za Fedha ambao ndio kiungo muhimu kati ya Serikali na wananchi katika kufikisha elimu na huduma bora za kifedha.

Aliongeza kuwa mafanikio ya sekta hiyo hayategemea tu uwepo wa Sera, Sheria na Kanuni nzuri, bali yanategemea zaidi utekelezaji wenye tija, weledi, uwajibikaji na ufuatiliaji makini unaoanzia kwa Waratibu wa Huduma Ndogo za Fedha ambao ndio kiungo muhimu kati ya Serikali na wananchi katika kufikisha elimu na huduma bora za kifedha.

Aidha, aliwapongeza Waratibu wote kwa kujitokeza kwa wingi na kwa wakati katika mafunzo hayo, na kuwataka kuyachukulia kama fursa ya kuimarisha uwezo wao wa kuwaelimisha wananchi kwa njia shirikishi, rafiki na yenye matokeo chanya.

Kwa upande wake, Mratibu wa Huduma Ndogo za Fedha kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo, Bw. Mohamed Nyange, alisema kuwa mafunzo hayo yamewapa maarifa ya kina na mbinu sahihi zitakazowawezesha kuwafikia wananchi kwa ufanisi, kutoa elimu inayoeleweka, na kusaidia jamii kuelewa umuhimu wa kutumia huduma rasmi za kifedha kwa maendeleo yao ya kiuchumi.

*Ili tuweze kutoa elimu sahihi kwa wananchi tunaowahudumia lazima nasi tuwe na uelewa wa kutosha kwanza, niwapongeze Wizara ya Fedha kwa kutujengea uwezo huu, tutaenda kutumia maarifa haya kwa kuhakikisha wananchi wetu wanajua, wanaelewa na wanatumia huduma za kifedha rasmi kama nyenzo ya kujikwamua kiuchumi," alisema Bw. Nyange.*

Jumla ya mikoa 13 imeshiriki katika mafunzo hayo, ambayo ni: Mbeya, Pwani, Njombe, Shinyanga, Dar es Salaam, Tanga, Singida, Morogoro, Dodoma, Simiyu, Iringa, Arusha na Kilimanjaro.





Mafunzo haya yameandaliwa kwa ushirikiano kati ya Wizara ya Fedha, Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Benki Kuu ya Tanzania (BoT) na Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC), lengo ni kuhakikisha nchi inakuwa na mtandao mpana wa waratibu waliobobea katika kutoa elimu ya kifedha kwa jamii.

Serikali imeendelea kuwekeza katika kuwajengea uwezo watendaji wake ili kuhakikisha elimu ya fedha inamfikia kila Mtanzania, kupitia elimu hiyo, wananchi wataweza kufanya maamuzi sahihi ya kifedha ikiwemo kutumia mifumo rasmi inayotambuliwa na Serikali kwa ajili ya maendeleo yao binafsi na ya taifa kwa ujumla.





# DKT. MWIGULU AWATAKA WATUMISHI WA WIZARA YA FEDHA KUZINGATIA MISINGI YA KAZI NA UTAWALA BORA

Na. Ramadhani Kissimba na Saidina Msangi

Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb), amewataka Watumishi wa Wizara ya Fedha, kutekeleza majukumu yao ya kila siku kwa kuzingatia misingi ya kazi na utawala bora ili kuepusha malalamiko yasiyo na lazima kutoka kwa wadau wake wakiwemo wananchi.

Mhe. Dkt. Nchemba alisema hayo wakati akifungua Mkutano wa 38 wa Baraza la Wafanyakazi la Wizara ya Fedha, lililofanyika katika katika Kituo cha Mikutano cha APC, kilichoko Bunju mkoani Dar es Salaam.

Aidha, Mhe. Dkt. Nchemba aliutaka Uongozi wa Wizara kumchukulia hatua stahiki kwa mujibu wa taratibu mtumishi yeyote atakayebainika na kuthibitika kwenda kinyume na misingi ya maadili katika utendaji kazi ili kulinda heshima ya Wizara.

*Ninatambua kwamba mnafahamu misingi ya utendaji kazi katika utumishi wa umma, hivyo, si jambo jema kusikia mtumishi yeyote wa Wizara ya Fedha anakiuka misingi ya utawala bora katika utumishi wa umma", alisema Mhe. Dkt. Nchemba.*

Pia, Mhe. Dkt. Nchemba aliwapongeza watumishi wote wa Wizara hiyo kwa kazi na mchango wao moubwa uliofanikisha majukumu yake ya kuismamia uchimi wa nchi na kuwezesha upatikanaji wa Fedha zinazotumika kutekeleza miradi mbalimbali ya kiuchumi na kijamii.

Aliwataka Watumishi wa Wizara kuendelea kufanya-kazi kwa ushirikiano kati ya Watumishi ndani ya Idara, Wizara na Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Fedha, na kuzielekeza Taasisi kutekeleza majukumu yao ya msingi kama inavyoratajiwa na Serikali pamoja na wadau wengine.



Mhe. Dkt. Nchemba aliongeza kuwa kutokana na Uwekezaji mkubwa uliofanywa na Wizara katika kuwapatia mafunzo Watumishi wake, hivyo ni lazima matokeo ya mafunzo hayo yaonekane kwa vitendo kupitia utendaji wa kila mtumishi, na kusisitiza umuhimu wa Watumishi kuendelea kupatiwa mafunzo ya mara kwa mara ili kuboresha utendaji na kuendana na kasi ya mabadiliko ya teknolojia.

Awali, akimkaribisha Mgeni Rasmi, Mwenyekiti wa Baraza hilo la Watanyakazi ambaye ni Katibu Mkuu Wizara ya Fedha, Dkt. Natu El-maamry Mwamba, alisema kuwa lengo kuu la Baraza la Wafanyakazi ni kuwashirikisha Wafanyakazi katika utekelezaji wa shughuli za Wizara kwa kushirikiana na Uongozi ikiwa ni pamoja na kuishauri Wizara juu ya ufanisi wa kazi na hatua zinazofaa kuchukuliwa ili huduma zinazotolewa na Wizara zikidhi matarajo ya wateja.

Dkt. Mwamba aliongeza kuwa katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2024/25, Wizara imepata mafanikio mbalimbali yakiwezo kupandishwa vyeo kwa Watumishi 484 wa kada mbalimbali na kulipa jumla ya shilingi 521,980,765/= yakiwa ni malimbikizo ya mishahara kwa Watumishi wa Wizara.



*Aidha, katika mwaka wa fedha 2024/25 Serikali imeshatoa kibali ili watumishi wenye sifa waweze kupandishwa vyeo. Uchambuzi wa awali umebaini kwamba watumishi 313 wana sifa za kupandishwa vyeo" alisema Dkt. Mwamba.*

Dkt. Mwamba aliongeza kuwa Mkutano wa 38 wa Baraza la Wafanyakazi ni mwendelezo wa mikutano mingine ambayo imekuwa ikifanyika kila mwaka ambapo kupitia mikutano hiyo wajumbe wamekuwa wakitoa maoni na mapendekezo ambayo yamesaidia kwa kiasi kikubwa kuboresha maslahi ya watumishi na utendaji kazi wa Wizara.

Mkutano wa 38 wa Baraza la Wafanyakazi wa Wizara ya Fedha, umekutanisha Wajumbe kutoka Makao Makuu ya Wizara, Wakuu wa Hazina Ndogo na Wahakikimali kutoka Mikoa yote ya Tanzania Bara.







# UFARANSA YAKARIBISHWA KUWEKEZA KWENYE VIWANDA VYA KUTENGENEZA DAWA MUHIMU NCHINI TANZANIA

Na. Benny Mwaipaja



Waziri wa Fedha Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb), ametoa wito kwa wawekezaji kutoka Ufaransa kuwekeza nchini Tanzania katika Sekta ya viwanda vya kuzalisha dawa za binadamu ili kukabiliana na upungufu wa dawa muhimu za binadamu hali inayosababishwa na mabadiliko sera za nchi mbalimbali duniani.

Dkt. Nchemba alitoa rai hiyo jijini Paris nchini Ufaransa, alipokutana na kufanya mazungumzo na ujumbe wa Shirika la Maendeleo la Ufaransa (AFD), ukiongozwa na Naibu Mkurugenzi Mkuu wa Shirika hilo, Bw. Bertrand Walckenaer.

Alisema Serikali ya Tanzania chini ya Uongozi wa Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, inajipanga kutekeleza miradi ya ujenzi wa viwanda vitakavyozalisha dawa muhimu zikiwemo za malaria, kifua kikuu na dawa za kufubaza virusi vya ukimwi (ARVs) ili kulinda maisha ya watu.

Dkt. Nchemba alikuwa akijibu hoja ya Kiongozi huyo wa Shirika la Maendeleo la Ufaransa (AFD) Bw. Walckenaer, aliyetaka kufahamu mipango ya Serikali ya kukabiliana na mabadiliko ya Sera za Serikali ya Marekani ambayo imesitisha utoaji misaada kwenye sekta mbalimbali ikwemo ya Afya.

Aliishauri AFD kuiunga mkono Tanzania katika kutekeleza azma ya kujenga miundombinu ya viwanda vya uzalishaji wa bidhaa hizo ili kunusuru maisha ya mamia ya wananchi waliokuwa wakitegemea misaada ya dawa kutoka nje ya nchi na kwamba wawekezaji watanufaika na soko kubwa la bidhaa na huduma katika eneo lote la Maziwa Makuu na nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC).



*Tunaikaribisha AFD kushirikiana na Serikali ya Tanzania pamoja na Sekta binafsi katika uzalishaji wa dawa na vifaa tiba ili nchi iweze kujitegemea katika eneo muhimu la Afya", alieleza Dkt. Nchemba.*

Aidha, alisema kuwa Serikali ya Ufaransa imekuwa ikiisaidia Tanzania katika agenda za maendeleo kuanzia mwaka 1980, ikiwa ni pamoja na ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Dar es Salaam, maendeleo ya sekta ya nishati, maji na kilimo, miradi ambayo imekuwa na manufaa makubwa kwa wananchi.

Kwa upande wake Naibu Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Maendeleo la Ufaransa (AFD), Bw. Bertrand Walckenaer, alisema kuwa suala la nchi za Afrika ikiwemo Tanzania kuwa na viwanda vyake vya kuzalisha dawa ni muhimu kwa ajili ya mustakabali wa maisha ya wananchi wake.

Alibainisha kuwa hatua ya Marekani ya kufuta misaafa ya sekta ya afya na misaada ya kibinadamu zilizokuwa zikisaidia mataifa mbalimbali duniani kupitia Shirika lake la Misaada (USAID), zinasababisha kuwe na ulazima wa nchi zinazoendelea zilizokuwa zinanufaika na misaada hiyo kutafuta namna ya kukabiliana na hali hiyo.

Aliahidi kuishawishi sekta binafsi kutoka Ufaransa kuwekeza nchini Tanzania katika sekta ya afya kwa kujenga viwanda vya kutengeneza dawa ili kutimiza lengo na matarajio ya nchi katika kuwahudumia wananchi.



Alisifu mazingira ya uwekezaji nchini Tanzania, pamoja na usimamizi mzuri wa uchumi wa nchi na mazingira mazuri ya uwekezaji unaopaswa kupigiwa mfano na mataifa mengine ya Afrika.

Bw. Bw. Bertrand Walckenaer, alisema Shirika la Maendeleo la Ufaransa limewekeza kiasi cha Euro bilioni 1.3 kwa miradi mbalimbali nchini Tanzania kutokana na utulivu wa sera na uchumi wake na kwamba wataendelea kushirikiana na Tanzania katika kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo kwa manufaa ya nchi hizo mbili.

Fedha hizi zimeelekezwa kwenye miradi ya sekta za; Maji, Nishati, Miundombinu ya Usafirishaji, Kilimo na Maliasili na Utalii.





# SERIKALI NA OECD YA UFARANSA KUSHIRIKIANA KUBORESHA SERA ZA KODI

Na. Benny Mwaipaja

Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb), alikutana na kufanya mazungumzo na Mtendaji Mkuu wa Shirika la Ushirikiano wa Kiuchumi na Maendeleo (OECD), Bw. Mathias Cormann, Makao Makuu ya Shirika hilo yaliyopo Jijini Paris nchini Ufaransa, ambapo pamoja na mambo mengine wamejadiliana namna Tanzania na Shirika hilo wanavyoweza kushirikiana katika kuimarisha usimamizi wa sera za kodi, usimamizi wa fedha za umma, mageuzi ya taasisi za kifedha na kuimarisha masuala ya uwekezaji nchini Tanzania.

Mhe. Dkt. Nchemba alieleza dhamira ya Serikali ya kuimarisha uwezo wa taasisi zake za kifedha kwa kupokea usaidizi wa kitaalamu kutoka OECD katika maeneo hayo, ikiwa ni sehemu ya juhudi za kuongeza mapato ya ndani, kuvutia uwekezaji na kuboresha mazingira ya biashara

Dkt. Nchemba alisema kuwa Tanzania ipo tayari kushirikiana na Shirika hilo kwa kupokea utaalam katika kuimarisha vyanzo vya mapato ya ndani, kuimarisha uwekezaji na kukuza uchumi jumuishi utakaochangia kuimarisha mapato yake ya ndani, kuboresha zaidi mazingira ya uwekezaji na ufanyaji biashara na hatimaye kukuza uchumi na maendeleo ya wananchi kwa ujumla.

Dkt. Nchemba alisema kuwa Tanzania inakubaliana na utozaji wa kodi wenye usawa katika uwekezaji hususani katika uchumi wa kidigitali hivyo Tanzania inaendelea kuliomba Shirika la OECD kutoa mafunzo ya kiufundi katika eneo hilo.

> *Tanzania itaweza kuimarisha usimamizi wa fedha za umma, kuongeza uwazi, na kuvutia mitaji ya kimataifa inayohitajika kwa utekelezaji wa Ajenda ya Maendeleo Endelevu ya 2030" alisema Mhe. Dkt. Nchemba.*



Kwa upande wake Mtendaji Mkuu wa Shirika la Ushirikiano wa Kiuchumi na Maendeleo (OECD), Bw. Mathias Cormann alisema kuwa Shirika lake liko tayari kushirikiana na Tanzania katika masuala ya usimamizi wa sera za kodi na uwekezaji ili kukuza Uchumi wa nchi kwa kuvutia zaidi mitaji kutoka nje ya nchi.

Ameipongeza Tanzania kwa juhudi zake katika kuhakikisha kunakuwa na kodi zenye usawa hususani katika mazingira yaliyopo sasa ya uchumi wa kidigitali na kuishauri walishauri Tanzania ijiunge na Kituo cha Maendeleo cha OECD, ambacho kwa sasa kina nchi wanachama 12 kutoka Afrika.

Bw. Cormann alizitaja faida za kuwa mwanachama wa kituo hicho ni pamoja na kuchapishwa kwa takwimu za mapato ya kodi (Revenue Statistics), ambazo hutoa uwazi kwa wawekezaji na wadau wa maendeleo, na kusaidia nchi kuonyesha uwezo wake wa kifedha kwa taasisi za fedha za kimataifa na wawekezaji binafsi.

Aidha, aliialika Tanzania kushiriki katika Mkutano wa Jukwaa la Misaada kwa Maendeleo Endelevu, utakaofanyika mwezi Mei mwaka huu, mkutano ambao utatoa nafasi kwa Tanzania kuwasilisha vipaumbele vyake vya maendeleo, kujifunza kutoka kwa wengine, na kuanzisha ushirikiano mpya katika sekta za mazingira, mabadiliko ya tabianchi na uchumi jumuishi.






# TANZANIA NA POLAND KUIMARISHA ZAIDI UHUSIANO WA KIUCHUMI

Na. Benny Mwaipaja




Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb), amekutana na kufanya mazungumzo na Naibu Waziri wa Mambo ya Nje wa Poland anayehusika na Bara la Afrika, Mjini Warsaw nchini Poland, Mhe. Anna Radwan-Röhrenschef, ambapo wamejadiliana namna ya kuimarisha diplomasia ya uchumi kati ya nchi hizo mbili kupitia utekelezaji wa miradi ya kimkakati inayotekelezwa nchini Tanzania katika sekta za kilimo, ujenzi wa miundombinu ya Reli ya Kisasa ya SGR na kuangazia fursa nyingine ambazo Poland pamoja na sekta binafsi ya nchi hiyo wanaweza kuwekeza ikiwemo Sekta ya nishati, usafiri, maji, afya na mingine mingi.



*Tunapoendelea kuimarisha ushirikiano wetu wa muda mrefu, ninaialika Poland kuangalia maeneo mapya ya ushirikiano yatakayoimarisha zaidi uhusiano wetu na kuimarisha zaidi uchumi wa Mataifa yetu mawili pamoja na watu wetu katika nyanja za ujenzi wa miundombinu ya maji, nishati, barabara, hususan katika Jiji letu la Dodoma ambalo idadi kubwa ya watu inazidi kuongezeka na kuhitaji huduma hizo muhimu" alisema Mhe. Dkt. Nchemba.*

Aidha, Mhe. Dkt. Nchemba alitoa rai kwa Poland kuisaidia Tanzania kuongeza ujuzi wa kiufundi kwa watanzania hususan vijana kupitia mafunzo maalumu ya ufundi na kutoa nafasi za masomo ama mafunzo ya juu kwa wataalam wa kitanzania ili kuwaongezea ubobezi katika taaluma zao kwa manufaa ya nchi, katika maeneo mahsusi ya fedha, teknolojia, na mapinduzi ya viwanda hali itakayochangia mageuzi makubwa ya kiuchumi yanayofanyika nchini Tanzania.

Kwa upande wake,  Naibu Waziri wa Mambo ya Nje wa Poland anayehusika na Bara la Afrika, Mhe. Anna Radwan-Röhrenschef, alisifu ushirikiano imara uliopo katı ya nchi yake na Tanzania na kuahidi kuendeleza uhusiano huo kwa kuchangia ujenzi wa miradi ya maendeleo inayotekelezwa nchini humo kwa faida ya nchi hizo mbili.

Alimpongeza Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kutekeleza miradi mikubwa ya kimkakati ikiwemo SGR, pamoja na kusimamia vizuri uchumi wa nchi ambao umekuwa imara kwa kusimamiwa vyema na Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Nchemba, ambaye ni msaidizi wake.

Alisema kuwa nchi yake inatamani kujifunza kutoka Tanzania kwa kuwa licha ya Taifa lake kuwa kubwa kiuchumi, lakini uchumi wake umepata changamoto katika kipindi hiki cha mzozo wa vita vya Ukraine na Urusi, pamoja na athari za UVIKO-19.

Mazungumzo hayo yalihudhuriwa pia na Balozi wa Tanzania nchini Ujerumani, ambaye pia anaiwakilisha Tanzania nchini Poland, Mhe. Hassani Iddi Mwamweta.







# IMF YAKUNWA NA UTEKELEZAJI MIPANGO YA TANZANIA YA KUKUZA UCHUMI NA KUKABILIANA NA MABADILIKO YA TABIANCHI

Na. Benny Mwaipaja

Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb), amelihakikishia Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) kwamba, Serikali itaendelea kufanya maboresho ya sera na mipango yake kwa kuhakikisha sekta mbalimbali za kiuchumi na kijamii pamoja na kuimarisha sekta binafsi zinapewa kipaumbele.

Dkt. Nchemba amesema hayo wakati akifunga vikao vya majadiliano kati ya Serikali na Timu ya Wataalam kutoka Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF), baada ya kukamilisha tathimini ya awamu ya tano ya utekelezaji wa program ya Extended Credit Facility-(ECF), inayohusisha mkopo nafuu kwa ajili ya kuimarisha uchumi wa nchi kupitia sekta za uzalishaji na huduma za jamii pamoja na awamu ya pili ya utekelezaji wa program ya kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi kupitia dirisha la Resilient and Sustainable Fund (RSF) kutoka Shirika hilo.

Akifunga vikao hivyo katika Kikao cha majumuisho kilichofanyika Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Jijini Dar es Salaam, Dkt. Nchemba, alieleza kufurahishwa kwake na taarifa iliyowasilishwa na Kiongozi wa Timu hiyo Bw. Nicolas Blancher, inayoonesha kuwa Tanzania imetekeleza ipasavyo vigezo vilivyowekwa na Shirika hilo katika mipango hiyo ya ECF na RSF.

Aliahidi kuwa Serikali itaendelea kusimamia ipasavyo utekelezaji wa programu hizo mbili zenye thamani ya dola za Kimarekani bilioni 1.832, ambapo kiasi cha dola bilioni 1.1 ni kwa ajili ya Mpango wa kuimarisha Uchumi wa nchi kupitia sekta za uzalishaji na kiasi cha dola milioni 786 ni kwa ajili ya Mpango wa nchi kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi, ambapo program hizo mbili zinatekelezwa katika kipindi cha miaka minne kuanzia mwaka 2022/2023 hadi 2025/2026.

Kwa upande wake, Kiongozi wa Timu ya Wataalam kutoka IMF waliofanya tathimini hiyo, Bw. Nicolas Blancher, alisema kuwa tathimini yao ya awamu ya tano imeonesha kuwa Tanzania imetekeleza vizuri mpango wa ECF na RSF



na kushauri hatua kadhaa zinazotakiwa kuendelea kuchukuliwa ikiwemo kuimarisha zaidi huduma za jamii na kuendelea kuimarisha mazingira bora ya kufanyabiashara na uwekezaji.



*Matarajio ya uchumi wa Tanzania ni mazuri kwakuwa utaendelea kukua kwa kasi, huku mfumuko wa bei ukiendelea kuwa chini, nakisi ya mauzo na manunuzi ya bidhaa na huduma nje ya nchi ikipungua, na upatikanaji wa fedha za kigeni ukiongezeka" alisema Bw. Blancher.*

Aliongeza kuwa hatua za kuwianisha vizuri mapato na matumizi ya serikali katika mwaka wa fedha wa 2025/26, zitasaidia kuhifadhi uhimilivu wa deni la serikali, huku zikilinda matumizi yenye kipaumbele katika huduma za kijamii.

Bw. Blancher alisema kuwa kuendelea kutekeleza sera za kukabiliana na athari na changamoto za mabadiliko ya tabianchi, zinazoungwa mkono na mpango wa RSF, kutasaidia kujenga ustahimilivu katika kushughulikia madhara ya mabadiliko ya tabianchi.

Alisema kuwa mapendekezo ya tathimini hiyo yatapelekwa mbele ya Bodi ya Wakurugenzi wa Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) na kwamba uamuzi utakaotolewa na Bodi utaiwezesha Tanzania kupokea ufadhili wa dola za Marekani milioni 441.

Tanzania imefanyiwa Tathimini ya Awamu ya Tano ili iweze kupata fedha kutoka IMF kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali ya kiuchumi na kijamii ambapo hadi sasa Program ya ECF imepokea kiasi cha dola za Marekani milioni 754.3 kati ya dola za Marekani bilioni 1.1 na kiasi kingine cha dola za Marekani milioni 55 zimepokelewa kupitia dirisha la RSF, mradi wenye thamani ya dola za Marekani milioni 786.

Kikao hichi kilihudhuriwa na Katibu Mkuu Wizara ya Fedha, Dkt. Natu El-Maamry Mwamba, Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania, Bw. Emmanuel Tutuba, na Manaibu Gavana, pamoja na Maafisa Waandamizi wa Serikali na wajumbe wa Timu ya Tathimini kutoka Shirika la Fedha la Kimataifa-IMF.



# SERIKALI IKO TAYARI KUSHIRIKIANA NA WADAU KUIMARISHA USAWA WA KIJINSIA

Na. Benny Mwaipaja

Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb), amesema kuwa Tanzania iko tayari kushirikiana na wadau mbalimbali zikiwemo serikali, mashirika ya kimataifa, sekta binafsi na asasi za kiraia ili kutafsiri kwa vitendo ahadi za Beijing+30 kuelekea Mkutano wa Nne wa Kimataifa kuhusu Ufadhili wa Maendeleo (FFD4), utakaofanyika kuanzia tarehe 30 Juni hadi 3 Julai 2025, Sevilla nchini Uhispania.

Dkt.Nchemba ameyasema hayo Jijini NewYork nchini Marekani, aliposhiriki mjadala ulioandaliwa na Taasisi ya Kimataifa inayojihusisha na masuala ya usawa wa kijinsia (UN Women), uliojikita kujadili namna ya kupata fedha kwa ajili ya kupunguza na kuondoa kabisa pengo la kijinsia katika uchumi na kuwawezesha wanawake kujikwamua kiuchumi wenye kauli mbiu isemayo *"Kutoka Beijing hadi FfD4: Kuunganisha Ahadi Kupitia Ushirikiano wa Wadau kwa Usawa wa Kijinsia, Uwezeshaji wa Kiuchumi wa Wanawake na Maendeleo Endelevu".*

Alizitaja baadhi ya hatua zilizochukuliwa na Serikali katika kuwawezesha wananwake na makundi mengine kiuchumi kuwa ni pamoja na kuwekeza katika elimu bora kwa wasichana hasa wa maeneo ya vijijini, kuwezesha upatikanaji wa huduma za kifedha kwa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake (WDF) na Mfuko wa Maendeleo ya Vijana (YDF).

Dkt. Nchemba kuwa Serikali inatoa msaada wa kisheria bure kupitia kampeni kama Mama Samia Legal Aid Campaign ambayo hadi Februari 2025 ilikuwa imetoa msaada wa kisheria kwa wanawake 681,326.

> *Tunatoa mafunzo ya elimu ya kifedha na ya kidijitali kwa wanawake na vijana kupitia huduma za uendelezaji wa biashara, tunatoa mikopo yenye masharti nafuu kwa wanawake, vijana, na watu wenye ulemavu na kukuza bajeti jumuishi kijinsia na kuhakikisha uchambuzi wa kijinsia unajumuishwa katika upangaji na utekelezaji wa bajeti ya umma" alisema Dkt. Nchemba.*

Alisema kuwa pamoja na mafanikio hayo, bado kuna vikwazo vya kimfumo vinavyozuia wanawake kufikia uwezo wao kamili wa kiuchumi na kubainisha kuwa mchakato wa FfD4 ni fursa muhimu ya kuhakikisha upatikanaji wa rasilimali za kifedha, sera jumuishi, na ushirikiano wa kibunifu unaoipa kipaumbele usawa wa kijinsia, kwa ajili ya kasi zaidi ya maendeleo.






*Tanzania inaipongeza UN Women kwa kuandaa nyaraka ya rasilimali (resource paper) inayotoa mwongozo wa kisera wa kifedha kwa mtazamo wa kijinsia. ambayo ni nyenzo muhimu itakayosaidia kuhakikisha kuwa uwezeshaji wa kiuchumi wa wanawake unakuwa kiini cha majadiliano na matokeo ya FfD4". Aliongeza Dkt. Nchemba*





Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Sera, Programu, Divisheni ya ushirikiano wa Kimataifa wa UN Women, Bi. Sarah Hendriks, alisema kuwa suala la kuwawezesha wanawake kiuchumi linapaswa kuwa agenda ya kudumu ya mataifa mbalimbali hususan ya kiafrika ili kujenga jamii yenye nguvu ya kiuchumi kupitia uwekezaji wa mitaji, elimu, biashara na kuwawezesha kufikia masoko kwa njia ya kidigiti.

Mkutano huo ulihudhuriwa pia na Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Fedha, Bi. Amina Khamis Shaaban na uliwashirikisha wadau kutoka sekta mbalimbali

# DKT NCHEMBA ASHAURI NCHI ZILIZOENDELEA KURAHISISHA UPATIKANAJI WA MIKOPO

Na. Benny Mwaipaja

Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb), ametoa rai kwa nchi zilizoendelea kupunguza gharama za mikopo na kutoa muda mrefu wa kulipa madeni ili kuziwezesha nchi zinazoendelea zikiwemo za Afrika kutekeleza miradi ya maendeleo itakayochochea ukuaji wa uchumi na maisha ya wananchi kwa ujumla.

Mhe. Dkt. Nchemba alitoa rai hiyo jijini New York nchini Marekani, wakati akichangia mada katika Jukwaa la Ufadhili wa Maendeleo la Umoja wa Mataifa kwa mwaka 2025 (ECOSOC Forum on Financing for Development Follow-Up (FfD Forum), linalofanyika Makao Makuu ya Umoja huo, Jijini NewYork nchini humo.

Alisema kuwa Mbinu za utoaji wa viwango vya mikopo zinapaswa kubadilika ili kuakisi kwa usahihi uwezo wa kweli wa nchi zinazoendelea kulipa madeni na kuhimiza matumizi zaidi ya fedha mchanganyiko (blended finance), upanuzi wa dhamana za hatari kutoka kwa Benki za Maendeleo ya Kielelezo (MDBs), na utekelezaji wa mipango ya uwazi wa madeni ili kusaidia kupunguza gharama za hatari zinazoonekana.

Dkt. Nchemba alipongeza juhudi zinazofanywa na mataifa pamoja na taasisi za fedha zinazokopesha kwa kuboresha upatikanaji wa mikopo nafuu lakini kwa nchi nyingi zinazoendelea, ikiwemo Tanzania, inakwazwa na viwango vikubwa vya gharama za mikopo na ulipaji wa madeni husika unaoathiri bajeti za nchi hizo.



Alipendekeza masuala matatu ya kufanyiwa kazi ikiwemo upatikanaji wa mikopo nafuu, kuongeza kasi ya kurekebisha muundo wa ulipaji madeni, kuwezesha upatikanaji wa mikopo mchanganyiko (blended finance) inayozingatia mahitaji pamoja na kuzisaidia nchi zinazoendelea kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi.

Akizungumzia umuhimu wa sekta binafsi katika kukuza uchumi, Dkt. Nchemba alisema kuwa uwekezaji wa sekta binafsi ni muhimu ili kutimiza malengo ya maendeleo ya milenia kwa kujenga uchumi himilivu, jumuishi na kuhakikisha hakuna mtu anayeachwa nyuma kimaendeleo.

Alishauri kuimarisha majukwaa ya kuwezesha uwekezaji ambayo yanaunganisha fursa na mitaji ya kimataifa, kuchochea athari chanya, na kuhakikisha hakuna anayeachwa nyuma na kwamba Tanzania iko tayari kushirikiana na washirika wote kufungua uwekezaji binafsi kwa maendeleo jumuishi na endelevu.

Dkt. Nchemba alisema kuwa Tanzania, chini ya uongozi mahili wa Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, imefanya mageuzi makubwa ya kisera ya upatikanaji wa fedha, kuweka uwazi wa matumizi na kutanua wigo wa upatikanaji wa mikopo nafuu kwa wanawake, vijana na watu wenye mahitaji maalum.

*Tunaendeleza ujumuishaji wa kifedha kupitia majukwaa ya kidijitali na kufanikisha urasimishaji wa sekta isiyo rasmi ili kuongeza upatikanaji wa masoko na fedha. Kwa ngazi ya kimataifa, tunatoa wito wa kuoanisha kwa kiwango kikubwa zaidi uwekezaji binafsi na vipaumbele vya kitaifa, kuimarisha ushirikiano wa kimataifa, na kuanzisha taasisi za msaada kama Kituo cha Kimataifa cha Msaada wa Uwekezaji kwa Nchi Zenye Maendeleo Duni (LDCs)" alisema Dkt. Nchemba.*

Alisema kuwa Kitaifa, Tanzania inatengeneza mikakati ya fedha endelevu, dhamana zenye mwelekeo mahsusi (thematic bonds), na inatumia ubunifu wa kidijitali ili kuvutia rasilimali. kuanzisha mifumo ya uwekezaji kutoka kwa diaspora na kuhamasisha uwekezaji katika miundombinu endelevu na inayostahimili mabadiliko ya tabianchi.

Alishauri kuimarisha majukwaa ya kuwezesha uwekezaji ambayo yanaunganisha fursa na mitaji ya kimataifa, kuchochea athari chanya, na kuhakikisha hakuna anayeachwa nyuma na kwamba Tanzania iko tayari kushirikiana na washirika wote kufungua uwekezaji binafsi kwa maendeleo jumuishi na endelevu.

Jukwaa la Ufadhili wa Maendeleo la Umoja wa Mataifa linawahusisha mawaziri wa Fedha, Mipango, Mambo ya Nje na sekta nyingine pamoja na wadau mbalimbali wa maendeleo yakiwemo mashirika ya Fedha ya Kimataifa kwa ajili ya kufanya tathmini ya utekelezaji wa Maazimio ya Umoja wa Mataifa kuhusu Ufadhili wa Maendeleo.






# SEMA NA BoT

**Mfumo wa Kushughulikia Malalamiko ya Watumiaji wa Huduma za Fedha**

**SKANI QR CODE KUPATA MFUMO WA SEMA NA BOT**

# DKT. NCHEMBA AZITAKA TAASISI ZA FEDHA KUJIUNGA NA MFUMO WA SEMA NA BOT

Na. Josephine Majura




Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb), ameiagiza Benki Kuu ya Tanzania (BoT), kusimamia na kuhakikisha Benki na Taasisi zote za Fedha nchini zinajiunganisha kwenye Mfumo wa Kushughulikia Malalamiko ya Watumiaji wa Huduma za Fedha kwa kuwa Mfumo huo utasaidia kutatua malalamiko ya wateja wao.

Dkt. Nchemba ametoa maagizo hayo wakati akizindua Mfumo wa Kushughulikia Malalamiko ya Watumiaji wa Huduma za Fedha (Sema na BoT) na Mazingira ya Majaribio ya Teknolojia ya Fedha (Bank of Tanzania Fintech Regulatory Sandbox), uliofanyika katika Ukumbi wa Mikutano wa Wizara ya Fedha wa Kambarage jijini Dodoma.

Akizungumzia kuhusu Mfumo wa Sema na BoT, alisema kuwa Mfumo huo utatoa fursa maalum katika kutatua malalamiko ya watumiaji wa huduma za fedha kwa ufanisi na uwazi na utakuwa suluhisho la malalamiko mbalimbali ambayo yamekuwa yakilamikiwa na watumiaji wa huduma za fedha ikiwemo mikopo umiza (kausha damu).

Aliongeza kuwa Mfumo wa Sema na BoT, utaongeza imani ya umma katika kutumia huduma rasmi za fedha na kuboresha uwajibikaji kwa watoa Huduma za Fedha wanaosimamiwa na Benki Kuu ya Tanzania.

Aidha, Dkt. Mwigulu, aliwataka watoa huduma za fedha kuhakikisha wanatoa elimu ya fedha kwa wateja wao na umma kama inavyoelekezwa katika Kanuni za Benki Kuu za Kumlinda Mtumiaji wa Huduma za Fedha za mwaka 2019.

Dkt. Nchemba akiongelea kuhusu kuanzishwa kwa Mazingira ya Majaribio ya Teknolojia ya Fedha (Bank of Tanzania Fintech Regulatory Sandbox), alisema Serikali imekusudia kuifanya Tanzania kuwa nchi ya mfano miongoni mwa nchi zinazoendelea katika ubunifu wa teknolojia ya masuala ya fedha, kwa kuweka mazingira yanayovutia uwekezaji wa kiteknolojia na kuwajengea uwezo vijana kushiriki katika kukuza uchumi wa kidijitali.



*Kuanzishwa kwa Mazingira ya Majaribio ya Teknolojia ya Fedha kunadhihirisha dhamira ya Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, ambaye anatamani kukuza matumizi ya teknolojia katika sekta ya fedha kuelekee kwenye uchumi wa kidijitali", alisema Dkt. Nchemba.*

Aidha, alizitaka taasisi za fedha kuendelea kutoa elimu kwa wananchi na kuwasisitiza kujitokeza kwa wingi wakati elimu ya fedha ikitolewa katika maeneo mbalimbali ili kuwa na uelewa mpana wa masuala ya fedha, elimu itakayowasaidia kupunguza kujihusisha na huduma za fedha zenye masharti yasiyo rafiki.

Kwa upande wake, Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango-Zanzibar, Dkt. Juma Malik Akil alisema kuwa kwa niaba ya Serikali wataenda kuusimamia Mfumo huo katika utendaji kazi wake ili kupata matokeo yaliyokusudiwa na Serikali.

Naye Gavana na Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Bw. Emmanuel Tutuba, alisema kuwa Mfumo wa Sema na BoT ni rafiki na utamwezesha kila mtumiaji wa huduma za fedha kuufikia na kuutumia wakati wowote, bila kujali mahali au uelewa wa teknolojia.

Aliongeza kuwa mfumo huo utawezesha Taasisi za Fedha kubaini na kushughulikia malalamiko ya watumiaji kwa wakati na kuboresha utoaji wa huduma kwa ujumla.













# SERIKALI YASAINI MIKATABA YA UNUNUZI NA USAFISHAJI DHAHABU

Na. Josephine Majura na Saidina Msangi

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Benki Kuu ya Tanzania imesaini mikataba ya ununuzi na usafishaji dhahabu na kampuni za uchimbaji madini na Kiwanda cha Usafishaji Dhahabu cha Geita Gold Refinery (GGR), hatua itayowezesha Benki Kuu kupata vyanzo vya uhakika katika kufanikisha programu yake ya ununuzi wa dhahabu.

Hafla ya utiaji saini wa mikataba hiyo imefanyika katika Ukumbi wa Kambarage, Treasury Square jijini Dodoma kati ya Gavana wa Benki Kuu na Kampuni za madini wakishuhudiwa na Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba Madelu (Mb) na Waziri wa Madini Mhe. Antony Mavunde.

Akizungumza katika hafla hiyo, Mhe. Dkt.Nchemba alisema hatua hiyo ni sehemu ya utekelezaji wa Kifungu cha 59 cha Sheria ya Madini ambacho kinawataka wachimbaji wa madini kutenga asilimia 20 ya uzalishaji wao kwa ajili ya kuiuza katika masoko ya ndani ikiwemo kuiuzia Benki Kuu ya Tanzania, ambayo imepewa haki ya kwanza kisheria ya ununuzi wa dhahabu.




*Sambamba na hiyo, hatua hii itaiwezesha Benki Kuu kupata vyanzo vya uhakika katika kufanikisha programu yake ya ununuzi wa dhahabu na itasaidia viwanda vya ndani vya usafishaji wa dhahabu kufikia malengo ya kupata ithibati ya kimataifa ya London Bullion Market Association (LBMA)", alifafanua Mhe. Dkt. Nchemba.*



Alisema kuwa mpango wa ununuzi wa dhahabu ni dhamira ya Serikali inayoongozwa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, katika kuhakikisha nchi inakuwa na akiba ya kutosha ya fedha za kigeni, kuongeza mchango wa madini katika pato la Taifa, pamoja na kuongeza thamani ya madini nchini ili kuhakikisha wananchi wote wananufaika na rasilimali za madini.

*Hadi leo Benki Kuu ya Tanzania, imenunua tani 5 za dhahabu sawa na dola za Marekani milioni 554 na kupitiliza malengo yake ya kununua dhahabu yenye thamani ya dola za Marekani milioni 350, Hatua hii ni kubwa na ya kihistoria nchini kwetu, kwa kuwa itatuhakikishia kuwa na dhahabu ya kutosha hapa nchini kwa ajili ya kusafishwa na viwanda vilivyopo hapa nchini, lakini pia kuipa Benki Kuu ya Tanzania, ambayo imeamua kununua na kutunza dhahabu kama sehemu ya fedha za kigeni", alifafanua Mhe. Dkt. Nchemba.*

Alisema tangu kuanza kutekelezwa kwa kanuni hiyo mpya, Benki Kuu imeweza kuongeza kwa kasi kiwango cha dhahabu inayonunua kutoka katika soko la ndani na hivyo matarajio ni kwamba itaweza kufikia malengo yake ya kununua tani 6 za dhahabu kwa mwaka wa fedha wa 2024/25 ili kutunisha akiba ya fedha za kigeni.

*Nitoe wito wa Serikali na wadau wote katika jambo hili kuhakikisha kwamba mkakati huu wa Serikali kununua dhahabu unakuwa endelevu. Lengo ni kwamba kama taifa tunakuwa na akiba ya kutosha ya fedha za kigeni katika dhahabu, kwani kwa muda mrefu sasa imedhihirika kwamba bei ya dhahabu imekuwa ni nzuri na inayozidi kupanda mwaka hadi mwaka", alisema Mhe. Nchemba.*

Kwa upande wake, Waziri wa Madini, Mhe. Antony Mavunde alisema sekta hiyo imeongeza mchango wake kwa pato la Taifa kutoka asilimia 9.0 mwaka 2015 hadi asilimia 10.1 mwaka 2024/25.

Alifafanua kuwa sekta ya madini ilikuwa inachangia kiasi cha Sh. bilioni 162 mwaka mzima katika Mfuko Mkuu wa Serikali lakini baada ya marekebisho ya Sheria kwa sasa inachangia kiasi cha Sh. bilioni 753 wakati lengo ni kufikia sh. trilioni moja, lengo ambalo alisema litafikiwa.

*"Hiki ni kiasi kikubwa kuwahi kutokea na hii inatokana na maelekezo ya Mheshimiwa Rais, Dkt.Samia Suluhu Hassan, ambaye anatuongoza vema katika nchi yetu, kuhakikisha madini yanaongezwa thamani na kuchangia katika Uchumi wa nchi yetu," alisema Mhe. Mavunde.*

Awali Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Bw. Emmanuel Tutuba, alibainisha kuwa Benki Kuu ya Tanzania ilianza rasmi Mpango wa Ununuzi wa Dhahabu nchini katika mwaka wa fedha 2022/23 kama sehemu ya utekelezaji wa mikakati ya Taifa ya kupunguza utegemezi wa mikopo ya nje kama chanzo kikuu cha akiba ya fedha za kigeni na hivyo kuongeza uwezo wa nchi kujitegemea kifedha.

NIC
SISI NDIYO BIMA

# Bima yako Mkopo wako!

## Huduma ya Mikopo midogo midogo ya muda mfupi

Kwa wateja wenye bima za Maisha ya Shirika la Bima la Taifa (NIC)

Nisogeze

Tanzania Commercial Bank
Growing stronger together




VOTED Superbrands EAST AFRICA'S CHOICE 2024-2026

ISO Certified 9001:2015




# KONA YA MIKUTANO YA MAJIRA YA KIPUPWE YA BENKI YA DUNIA NA SHIRIKA LA FEDHA DUNIANI-IMF JIJINI WASHINGTON, 2025

Na. Benny Mwaipaja na Joseph Mahumi



SPRING MEETINGS
WASHINGTON 2025




Mikutano ya Majira ya Kipupwe ya Benki ya Dunia (World Bank) na Shirika la Fedha Duniani (IMF), ni mikutano ya kila mwaka inayofanyika katika makao makuu yao jijini Washington DC, Marekani. Mikutano hii huwaleta pamoja mawaziri wa fedha na uchumi, magavana wa benki kuu, wataalamu wa maendeleo, mashirika ya kiraia, sekta binafsi, na waandishi wa habari kutoka pande zote duniani.

Asili ya mikutano hii inarejea tangu kuanzishwa kwa IMF na Benki ya Dunia mwaka 1944 kupitia Mkutano wa Bretton Woods, uliofanyika Marekani. Tangu wakati huo, taasisi hizi mbili zimekuwa zikikutana mara mbili kwa mwaka: wakati wa Majira ya Kipupwe (Spring Meetings) (miezi ya Aprili) na Mikutano ya Mwaka (Annual Meetings) (miezi ya Septemba/Oktoba).

Lengo kuu la Spring Meetings ni kujadili masuala ya kifedha ya kimataifa, maendeleo ya uchumi wa dunia, usaidizi kwa nchi maskini, mabadiliko ya tabianchi, ajira, uwekezaji wa kimkakati, na changamoto zingine zinazoathiri maendeleo endelevu. Ni jukwaa muhimu ambapo nchi wanachama huwasilisha hali ya uchumi wao, kupata ushauri wa sera, pamoja na kuimarisha ushirikiano wa kimataifa wa kifedha.

Kwa miaka ya hivi karibuni, Spring Meetings zimekuwa na umuhimu zaidi kwa nchi zinazoendelea, hasa za Afrika, kwani zimekuwa zikitumika kama nafasi ya kuzungumza moja kwa moja na wakuu wa taasisi hizi kuhusu mahitaji ya mikopo nafuu, unafuu wa madeni, na utekelezaji wa ajenda za maendeleo kama vile Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs) na Ajenda ya Afrika 2063.

Kwa kifupi, Mikutano hiyo ni nguzo muhimu katika mfumo wa utawala wa uchumi wa dunia, na zimekuwa zikiendelea kubadilika ili kukidhi changamoto na matarajio ya dunia ya sasa.

Tanzania imeshiriki mikutano mbalimbali katika Spring Meetings 2025 ambayo ilifanyika kati ya tarehe 21 hadi 26 Aprili na zilikuwa na mafanikio makubwa.







# TANZANIA IMEJIPANGA KUKABILIANA NA MABADILIKO YA SERA ZA NJE ZA MATAIFA MAKUBWA

Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb) amesema kuwa Tanzania imejipanga kukabiliana na mabadiliko ya sera za nje za Marekani kuhusu misaada kwa nchi za Afrika kwa kutumia rasilimali zake ndani kupitia Bajeti Kuu ya Serikali.

Mhe. Dkt. Nchemba alisema hayo alipokutana na kufanya mazungumzo na Mkurugenzi Mtendaji wa Kundi la Kwanza la Nchi za Afrika wa Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF), Bw. Adran Ubisse, kando ya Mikutano ya Majira ya Kipupwe ya IMF na Benki ya Dunia, inayofanyika Jijini Washington D.C, nchini Marekani.

Dkt. Nchemba alikuwa akijibu swali la Bw. Ubisse, aliyetaka kufahamu mipango ya Serikali ya kukabiliana na uamuzi wa Marekani wa kusitisha misaada yake kwa Bara la Afrika ikiwemo sekta ya afya pamoja na kuweka ushuru wa bidhaa zinazoingizwa nchini humo kutoka mataifa hayo na mengine duniani kote.

Alisema kuwa Serikali imetenga fedha na kuongeza mafungu ya matumizi kupitia Bajeti Kuu ya Serikali ya Mwaka wa Fedha 2025/2026, kwa ajili ya kugharamia sekta mbalimbali zinazoathiriwa moja kwa moja na uamuzi huo wa Marekani, ikiwemo sekta ya afya.

Dkt. Nchemba alifafanua kuwa Serikali imejipanga kubana matumizi yake ya kawaida na kuelekeza fedha nyingi katika maeneo ya huduma za jamii na sekta za uzalishaji ili kulinda uchumi wa nchi unaokua kwa kasi lakini pia kuhakikisha kuwa wananchi wanapata huduma muhimu za kijamii.



Kwa upande wake, Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Mhe. Stanslaus Nyongo, alisema kuwa Serikali imekamilisha Dira Mpya ya Taifa ya Maendeleo ya 2050, ambayo imeweka misingi ya kukuza uwezo wa nchi kujitegemea kwa kuimarisha sekta muhimu za uzalishaji, ikiwemo kilimo, matumizi ya teknolojia ya habari na mawasiliano, hatua itakayokuza kipato cha mtu mmoja mmoja na uchumi wa taifa kwa ujumla.



Alisema kuwa kupitia Dira hiyo itakayoanza kutumika kuanzia mwaka wa fedha 2025/2026, ambayo hivi sasa inaandaliwa mpango wa utekelezaji wa mwaka mmoja mmoja, utaongeza uwezo wa kipato cha Mtanzania, kwa mwaka, kutoka dola za Marekani 1,250 za sasa hadi kufikia dola 4,700 ifikapo mwaka 2050.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mtendaji wa Kundi la Kwanza la Nchi za Afrika wa Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF), Bw. Adran Ubisse, aliipongeza Tanzania kwa kuchukua hatua hizo madhubuti za kusimamia uchumi na kuhakikisha kuwa sera za nje za misaada za mataifa mengine haziathiri mustakabali wa maendeleo ya nchi na huduma za kijamii kwa ujumla.




Alisema kuwa IMF inakuna kichwa namna ya kuyasaidia mataifa mbalimbali ya Afrika kuwa na sera na uwezo wa kuhimili mikikimikiki hiyo kupitia program mbalimbali zinazosimamiwa na Shirika lake ikiwemoKujiandaa na maombi mengi ya fedha yanayotarajiwa kuwasilishwa na nchi mbalimbali ili yawe na uwezo wa kujiimarisha kiuchumi.











# DKT. NCHEMBA ATETA NA MKURUGENZI WA IMF ANAYESIMAMIA KANDA YA AFRIKA

Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb), alikutana na kufanya Mazungumzo na Mkurugenzi wa Shirika la Fedha la Kimataifa -IMF anayesimamia Kanda ya Afrika, Bw. Abebe Selassie, kando ya Mikutano ya Majira ya Kipupwe ya IMF na Benki ya Dunia, inayofanyika Jijini Washington D.C, nchini Marekani, ambapo wamejadiliana masuala mbalimbali ya ushirikiano ikiwemo utekelezaji wa programu ya Extended Credit Facility-(ECF), inayohusisha upatikanaji wa mkopo nafuu kwa ajili ya kuimarisha uchumi wa nchi kupitia sekta za uzalishaji na huduma za jamii pamoja na ufadhili wa kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi kupitia dirisha la Resilient and Sustainable Fund (RSF) kutoka Shirika hilo.











# TANZANIA YASHIRIKI MKUTANO WA MAWAZIRI WA FEDHA NA MAGAVANA WA BENKI KUU ZA AFRIKA

Katibu Mkuu Wizara ya Fedha, Dkt. Natu El-maamry Mwamba, alishiriki Mkutano wa Mawaziri wa Fedha na Magavana wa Benki Kuu za Afrika, uliojadili maeneo ya kipaumbele ambayo nchi za Afrika zinahitaji kuyasukuma kama agenda mahususi katika mikutano ya Kundi la nchi 20 Tajiri Duniani (G20) kwa mwaka 2025 ambapo Nchi ya Afrika Kusini ni mwenyekiti wa G20, Mkutano uliofanyika katika Ofisi za Kamisheni ya Umoja wa Afrika, kando ya mikutano ya Kipupwe ya Benki ya Dunia na Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF), Jijini Washington D.C, Marekani.

Aidha, majadiliano katika mkutano huo pamoja na mambo mengine, yaliangazia kuhusu Afrika kuwa na sauti moja katika kuzishawishi nchi za G20 kufanya mabadiliko yatakayosaidia upatikanaji wa fedha na mikopo nafuu kwa nchi zinazoendelea, namna ya kukabiliana na madeni, suala ambalo ni tatizo kwa nchi nyingi za Afrika kufuatia mabadiliko mbalimbali ya kiuchumi, kijiografia na kisiasa.










# DKT. NCHEMBA ATETA NA MKURUGENZI MTENDAJI WA UENDESHAJI WA BENKI YA DUNIA

Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba Mb), alikutana na kufanya Mazungumzo na Mkurugenzi Mtendaji wa Masuala ya Utawala na Uendeshaji wa Benki ya Dunia, Bi. Anna Bjerde, kando ya Mikutano ya Majira ya Kipupwe ya IMF na Benki ya Dunia, inayofanyika Jijini Washington D.C, nchini Marekani, ambapo pamoja na mambo mengine, Dkt. Nchemba aliishukuru Benki hiyo kwa mchango mkubwa wa maendeleo ya Tanzania kupitia miradi mbalimbali inayopata fedha kutoka Taasisi hiyo pamoja na kuonesha nia ya kusaidia ujenzi wa Mradi wa Reli ya kisasa (SGR)

Aidha, katika kikao hicho, alitambulishwa Makamu wa Rais Mpya wa Benki ya Dunia anayesimamia Kanda ya Afrika Mashariki na Kusini, Bw. Ndiamé Diop, ambaye ameteuliwa hivi karibuni baada ya Bi. Victoria Kwakwa kumaliza muda wake.










# DKT NCHEMBA AHIMIZA NCHI ZA AFRIKA KUVUTIA UWEKEZAJI WA NDANI

Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb), alizishauri nchi za Afrika kuweka mikakati ya kufanya uwekezaji na biashara ndani ya Bara la Afrika ili kukabiliana na changamoto za mabadiliko ya sera za kiuchumi zinazojitokeza hivi sasa duniani.

Mhe. Dkt. Nchemba alitoa ushauri huo jijini Washangton D.C, nchini Marekani, wakati akichangia taarifa ya Mwaka ya utekelezaji ya majukumu ya Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF), wakati wa Mkutano wa Majira ya Kipupwe (Spring Meetings) wa Magavana wa Shirika hilo wa Nchi za Afrika Kundi la Kwanza (Africa Group I Constituency – IMF).

Alisema kuwa mabadiliko ya kisera yanayojitokeza hivi sasa duniani ikiwemo vikwazo vya kibiashara vinavyotolewa na mataifa makubwa kwa kuongeza ushuru na tozo mbalimbali, iwe ni chachu kwa nchi za Afrika kutafuta njia za kujiimarisha kiuchumi kwa kuweka mipango madhubuti katika bajeti za nchi na kuuziana bidhaa.



Dkt. Nchemba alisisitiza kuwa hali ilivyo sasa inaonesha nchi za Afrika zinakuwa washindani wa kibiashara badala ya kuwa washirika hali inayotishia mustakabali wa kiuchumi wa nchi hizo.

Alisisitiza umuhimu wa nchi za Afrika kuangalia maeneo ya uwekezaji katika miundombinu mbalimbali ndani ya Bara hilo ikiwemo ujenzi wa viwanda vya kutengeneza dawa muhimu za binadamu na sekta nyingine zitakazochangia kukuza ajira kwa wananchi wao pamoja na kuimarisha uchumi wa nchi hizo.



Mhe. Dkt. Nchemba alisema kuwa ufinyu wa ufadhili wa kimataifa, unaochochewa na kupanda kwa viwango vya riba katika nchi zilizoendelea kiuchumi na kuhama kutoka kutoa misaada na ukopeshaji wa masharti nafuu, kumezuia zaidi nafasi ndogo ya kifedha katika nchi hizi kujiletea maendeleo.

Aliongeza kuwa matokeo yake, kuyumba kwa uchumi mkuu kumeongezeka, uwezo wa kitaasisi umemom-onyoka, na upatikanaji wa ufadhili wa masharti nafuu na wa soko umezidi kuwa na vikwazo, na kudhoofisha matarajio ya kufikia maendeleo yanayotarajiwa.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Mkutano huo ambaye ni Gavana wa Benki Kuu ya Botswana, Bw. Cornelius Dekop, aliunga mkono ushauri wa Tanzania na kusisitiza kuwa uchakataji wa bidhaa ndani ya nchi za Afrika pamoja na ushirikiano wa kibiashara, utakuwa na tija kubwa kuliko utegemezi wa biashara nje ya mipaka ya Afrika.

Alisisitiza kuwa changamoto za kibiashara zilizopo hivi sasa katika dunia itumike kama fursa ya kuliamsha Bara la Afrika kutafuta njia za kujiimarisha kiuchumi kwa kuwa katika Bara hilo kuna soko kubwa na pia fursa za uwekezaji na biashara kwa ujumla.










# DKT. NATU MWAMBA ATETA NA TIMU YA BENKI YA DUNIA

Katibu Mkuu Wizara ya Fedha, Dkt. Natu El-maamry Mwamba, alikutana na kufanya mazungumzo na Timu ya Benki ya Dunia Tanzania, ikiongozwa na Mwakilishi Mkazi wa Benki ya Dunia nchini Tanzania, Bw. Nathan Belete, kuhusu Ushirikiano wa Maendeleo kati ya Tanzania na Benki hiyo hususan Utekelezaji wa miradi inayotekelezwa nchini, pamoja na miradi inayotarajiwa kufadhiliwa na Benki hiyo kupitia mzunguko wa IDA 21, tukio lililofanyika kando ya Mikutano ya Kipupwe ya IMF na Benki ya Dunia, inayofanyika Jijini Washington D.C, nchini Marekani.











# DKT. NATU MWAMBA AKUTANA NA KUZUNGUMZA NA KATIBU MKUU WIZARA YA MAMBO YA NJE SWEDEN

Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mlipaji Mkuu wa Serikali, Dkt. Natu El-maamry Mwamba, alikutana na kufanya mazungumzo na Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Nje wa Sweden, Bi. Diana Janse, Kando ya Mikutano ya Majira ya Kipupwe, ya Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) na Benki ya Dunia ya mwaka 2025, inayofanyika jijini Washington D.C nchini Marekani.

Katika mazungumzo yao yaliyofanyika katika Ubalozi wa Tanzania nchini Marekani, Jijini Washington, Dkt. Mwamba na mgeni wake, walijadiliana masuala kadhaa ya kuimarisha zaidi ushirikiano wa kiuchumi kati ya Tanzania na Sweden, ikiwemo utekelezaji wa miradi mbalimbali ya kimkakati inayotekelezwa na Serikali na pia kuendeleza mashirikiano ya kibiashara na kiuchumi kati ya nchi hizo mbili.









# DKT. NCHEMBA ATETA NA MKURUGENZI MTENDAJI WA BENKI YA DUNIA

Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb), ameishukuru Benki ya Dunia kwa mchango wake mkubwa katika maendeleo ya nchi kupitia misaada, mikopo nafuu na utaalamu wa kiufundi ambao Taasisi hiyo kubwa ya Fedha Dunia inaipatia Tanzzania kwa miongo kadhaa sasa.

Mhe. Dkt. Nchemba amesema hayo alipokutana na kufanya mazungumzo na Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Dunia, anayesimamia Kundi la Kwanza la nchi za Kanda ya Afrika (Africa Group 1 Constituency), Dkt. Zarau Wendeline Kibwe, Makao Makuu ya Benki hiyo Jijini Washington D.C, nchini Marekani.

Pamoja na kuishukuru Benki ya Dunia kwa kuendelea kutoa fedha zinazotumika kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo, Dkt. Nchemba alionesha furaha yake kwa Benki ya Dunia kuonesha utayari wake wa kusaidia ujenzi wa mradi mkubwa wa kimkakati wa Reli ya Kisasa (SGR).



Aidha, Mhe. Dkt. Nchemba alimkumbusha Dkt. Kibwe, kuhusu maombi ya Tanzania ya kutaka Kiswahili kiwe sehemu ya lugha rasmi za mawasiliano katika mikutano ya Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) na Benki ya Dunia kutokana na umuhimu wake katika maendeleo ya Bara la Afrika na Dunia kwa ujumla.

Katika kikao hicho pia alishiriki Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Mhe. Stanslaus Nyongo, aliyezungumzia kuhusu kuanza kwa utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2050 itakayosaidia kuchochea maendeleo ya watu na kukuza uchumi wa nchi, huku Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango Zanzibar, Dkt. Juma Malik Akil, aliyeshukuru kwa mchango wa Benki ya Dunia katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii ya Zanzibar.



Alibainisha kuwa Benki ya Dunia itaendeleza ushirikiano huo kupitia mwelekeo mpya wa kisera ambapo msisitizo mkubwa umewekwa katika maeneo matano yenye kuziwezesha nchi wanachama husussan zilizoko katika Ukanda wa Kusini mwa Jangwa la Sahara, kuwekeza kwenye miradi itakayochangia kukuza ajira, kupitia sekta za kilimo biashara, ujenzi wa miundombinu ikiwemo reli, nishati, afya, utalii na uzalishaji viwandani vitakavyo changia kuongeza thamani ya bidhaa.



Uwekezaji wa Benki ya Dunia katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ya kiuchumi na kijamii nchini Tanzania umefikia dola za Marekani bilioni 10.9 ambapo miradi 38 ya maendeleo inatekelezwa katika sekta mbalimbali ikiwemo afya, maji, elimu, nishati, ujenzi wa miundombinu ya Barabara, na huduma za kijamii ikiwemo masoko na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.



Kwa upande wake, Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Dunia, anayesimamia Kundi la Kwanza la nchi za Kanda ya Afrika (Africa Group 1 Constituency), ambaye ni Mtanzania, Dkt. Zarau Wendeline Kibwe, alisema Benki ya Dunia inathamini ushirikiano mkubwa uliopo kati ya Benki yake na Tanzania.





# DKT. NATU MWAMBA ATETA NA MKURUGENZI MTENDAJI WA MFUKO WA CIF

Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mlipaji Mkuu wa Serikali, Dkt. Natu El-maamry Mwamba, alikutana na kufanya mazungumzo na Mkurugenzi Mtendaji wa Mfuko wa Uwekezaji katika Mabadiliko ya Tabianchi (Climate Investment Funds (CIF), Bi. Tariye Gbadegesin, Kando ya Mikutano ya Majira ya Kipupwe, ya Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) na Benki ya Dunia ya mwaka 2025, inayofanyika jijini Washington D.C nchini Marekani.


Katika mazungumzo yao yaliyofanyika katika Ubalozi wa Tanzania nchini Marekani, Jijini Washington, Dkt. Mwamba na mgeni wake, wamejadiliana masuala kadhaa kuhusu jinsi Mfuko wa CIF unavyoweza kusaidia juhudi za Tanzania katika kutekeleza Mpango wa Nishati (Energy Compact) na kuendeleza vipaumbele vya matumizi ya Nishati safi.












# BENKI YA DUNIA YAIMWAGIA SIFA TANZANIA KWA KUSIMAMIA VIZURI UCHUMI WAKE

Benki ya Dunia imeimwagia sifa Tanzania kwa usimamizi mzuri wa uchumi wa nchi na kuwa nchi ya kupigiwa mfano barani Afrika licha ya misukosuko mbalimbali ya kiuchumi inayoikabili dunia.

Pongezi hizo zimetolewa na Makamu mpya wa Rais wa Benki ya Dunia anayesimamia Kanda ya Afrika Mashariki na Kusini, Dkt. Ndiamé Diop, alipokutana na kufanya mazungumzo na ujumbe wa Tanzania, unaoongozwa na Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, kwenye Mikutano ya Majira ya Kipupwe ya Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) na Benki ya Dunia, Jijini Washington D.C, nchini Marekani.

Dkt Diop alisema kuwa Tanzania ni nchi ya mfano katika usimamizi wa sera za uchumi na fedha ambapo licha ya changamoto za UVIKO 19 na mizozo ya kisiasa inayoendelea sehemu mbalimbali duniani, tathimini ya Benki hiyo inaonesha kuwa uchumi wa Tanzania uko imara ikilinganishwa na nchi nyingine nyingi za Afrika.

Alisifu pia mikakati iliyowekwa na Serikali kwa ajili ya kukabiliana na changamoto ya Sera za nje za Marekani na duniani kwa ujumla za kupunguza misaada na kuondoa ufadhili katika miradi mbalimbali ikiwemo sekta ya afya, kwa kutumia fedha zake za ndani.







Aidha, alipongeza uhusiano imara uliopo kati ya Tanzania na Benki ya Dunia na kuahidi kuwa Benki yake itaendelea kuisaidia Tanzania katika jitihada zake za kukuza uchumi na kuwaondolea umasikini wananchi wake kwa kusaidia fedha zitakazotumika kutekeleza miradi mbalimbali ya kiuchumi na kijamii pamoja na kutoa misaada ya kiufundi itakayochochea ukuaji wa uchumi.

Kwa upande wake, Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba alimweleza Makamu mpya wa Rais wa Benki ya Dunia anayesimamia Kanda ya Afrika Mashariki na Kusini, Dkt. Ndiamé Diop, aliyechukua nafasi ya Bi. Victoria Kwakwa, aliyemaliza muda wake, kwamba Benki ya Dunia ni mdau mkubwa wa maendeleo wa Tanzania.



Alisema kuwa, usimamizi mzuri wa uchumi unatokana na mwongozo na maono makubwa ya Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambaye ameelekeza fedha nyingi katika sekta za uzalishaji na maendeleo ya jamii lakini pia ujenzi wa miundombinu inayochochea ukuaji wa uchumi.

Aliongeza kuwa Serikali imejipanga kuendelea kusimamia uchumi kwa kuimarisha sera za uchumi na fedha pamoja na kuishirikisha kikamilifu sekta binafsi katika kujenga uchumi wa nchi pamoja na kukabiliana na changamoto zinazotokana na mabadiliko ya mwelekeo ya kisera yanazotokea duniani ambayo kwa namna moja ama nyingine yameziathiri nchi nyingi za Afrika.

Uwekezaji wa Benki ya Dunia katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ya kiuchumi na kijamii nchini Tanzania umefikia dola za Marekani bilioni 10.9 ambapo miradi 38 ya maendeleo inatekelezwa katika sekta mbalimbali ikiwemo afya, maji, elimu, nishati, ujenzi wa miundombinu ya Barabara, ujenzi wa masoko na miradi ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.



# KONA YA MKUTANO WA MWAKA WA **BENKI YA MAENDELEO YA AFRIKA (AFDB) 2025**

Na. Benny Mwaipaja na Joseph Mahumi






Tanzania ilishiriki kikamilifu katika Mkutano wa Mwaka wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) 2025 uliofanyika jijini Abidjan, Côte d'Ivoire, kuanzia tarehe 26 hadi 30 Mei 2025. Ujumbe wa Tanzania uliongozwa na Makamu wa Rais, Dkt. Philip Mpango, ambaye alishiriki katika mijadala ya viongozi wa juu ya Afrika kuhusu mwelekeo wa maendeleo ya kiuchumi barani, ikiwa ni pamoja na matumizi ya rasilimali za ndani na umuhimu wa kuwekeza katika miundombinu na rasilimali watu. Kupitia ushiriki wake, Tanzania ilisisitiza ajenda ya maendeleo ya ndani na nafasi ya mageuzi ya kiuchumi kwa manufaa ya wananchi wake.

Katika mkutano huo, Tanzania pia ilinufaika na uwasilishaji wa mradi mkubwa wa maendeleo ya ujuzi kwa vijana katika sekta ya uchumi wa buluu (Blue Economy), ambapo AfDB ilitoa ufadhili wa zaidi ya dola milioni 54 kwa ajili ya kuongeza ajira na ushirikishwaji wa vijana na wanawake katika sekta hiyo. Mradi huu ulishirikisha wadau mbalimbali, wakiwemo wanaharakati wa kiraia kutoka Tanzania, waliotoa mchango wao katika kuhakikisha kuwa sauti za jamii zinazingatiwa katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Mbali na hilo, Tanzania iliendelea kunufaika na mikopo ya maendeleo kutoka AfDB inayolenga uboreshaji wa miundombinu ya kimkakati, kama vile reli ya kisasa ya SGR inayounganisha mikoa ya kati hadi magharibi mwa nchi na kupanuka hadi Burundi. Ingawa miradi hiyo haikuzungumzwa moja kwa moja katika ajenda kuu za mkutano, ni sehemu ya mafanikio ya ushirikiano endelevu kati ya Tanzania na AfDB unaolenga kuboresha mazingira ya biashara, usafirishaji na uchumi wa kikanda.

Kupitia jukwaa la mashirika ya kiraia, wanaharakati wa Tanzania walihudhuria na kushiriki mijadala iliyolenga kuhakikisha uwazi, uwajibikaji na ushirikishwaji wa jamii katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo inayofadhiliwa na benki hiyo. Hili linaonesha dhamira ya Tanzania ya kuendeleza maendeleo jumuishi na yanayozingatia usawa wa kijinsia na haki za kijamii.

Kwa ujumla, ushiriki wa Tanzania katika Mkutano wa AfDB 2025 umeonesha dhamira ya dhati ya Serikali kuendeleza sera za ndani zinazojikita katika ustawi wa wananchi, huku ikinufaika na fursa za kimataifa za fedha na usaidizi wa kiufundi kutoka kwa taasisi za maendeleo. Tanzania imejidhihirisha kama mshiriki muhimu katika ajenda ya maendeleo ya Afrika, kwa kuwekeza katika vijana, miundombinu na mageuzi ya kiuchumi yanayozingatia mazingira na ushirikishwaji wa jamii.



# TANZANIA YAIPA KONGOLE AFDB KWA KUCHANGIA MAENDELEO YA TANZANIA

Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb) amesema kuwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inatambua kwa dhati na kuthamini ushirikiano wa karibu na wa kimkakati na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) uliochangia utekelezaji wa miradi mikubwa ya maendeleo ya miundombinu, nishati, maji, kilimo, na ustawi wa kijamii.

Mhe. Dkt. Nchemba amesema hayo wakati akitoa majumuisho ya uwakilishi wa Tanzania katika Mkutano wa 60 wa Baraza la Magavana wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) na Mkutano wa 51 wa Baraza la Magavana wa Mfuko wa Maendeleo wa Benki hiyo (ADF), iliyofanyika katika Hoteli ya Sofitel Ivoire, Abidjan, nchini Côte d'Ivoire.

Alisema kuwa katika miaka ya hivi karibuni, Tanzania imekuwa na ongezeko kubwa la ushirikiano na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), ambapo hivi sasa Serikali inatekeleza miradi ya maendeleo ya kimkakati 25 ikiwemo 21 ya Serikali (Tanzania Bara na Zanzibar) na miradi 4 ni ya sekta binafsi katika sekta za miundombinu, nishati, usafirishaji, maji, usafi wa mazingira, pamoja na kilimo, yote kwa pamoja ikiwa na thamani ya dola za Marekani bilioni 3.54.

Mhe. Dkt. Nchemba aliitaja baadhi ya miradi hiyo kuwa ni pamoja na Ujenzi wa Reli ya Kisasa (SGR), Ujenzi wa Barabara za Mzungumko jijini Dodoma, ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Msalato mkoani Dodoma.

ambayo kukamilika kwake kutaleta mageuzi makubwa ya kiuchumi nchini Tanzania.

*"Kwa kuwa miradi hii inaendana na vipaumbele vya kitaifa na Ajenda ya Maendeleo ya 2063 ya Umoja wa Afrika pamoja na Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs), Tanzania inatarajia kuendelea kushirikiana na AfDB kupitia mikakati ya ADF-17 na vyanzo vingine vya fedha ili kuharakisha maendeleo jumuishi na endelevu kwa taifa na ukanda wa Afrika kwa ujumla" alisema Dkt. Nchemba.*

Alisema kuwa chini ya Mfuko wa Maendeleo wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (ADF) mzunguko wa 17, Tanzania itaendelea kupata rasilimali fedha kwa kutumia mifumo mbalimbali ikiwemo dhamana za mkopo ili kusaidia miradi mikubwa ya miundombinu kwa ajili ya maendeleo ya wananchi wa Tanzania.







Akizungumzia kuhusu Rais Mteule mpya wa Benki ya Maendeleo ya Afrika, Dkt. Sidi Quld Tah, alisema Rais huyo mpya wa AfDB si mgeni kwa Tanzania ambapo alimpongeza kwa ushindi wake na kwamba Tanzania itashirikiana naye kikamilifu kuhakikisha agenda za nchi za kuharakisha maendeleo yake zinafikiwa kama alivyofanya mtangulizi wake, Dkt. Akinumwi Adesina.

Benki ya Maendeleo ya Afrika, AfDB, imetimiza miaka 60 tangu kuzishwa kwake ikiwa na wanachama 81 zikiwemo nchi 54 za Afrika na imekuwa ikitoa mchango mkubwa wa maendeleo ya kiuchumi na kijamii katika nchi hizo, ikiwemo Tanzania.











# TANZANIA YASHIRIKI UCHAGUZI WA RAIS WA BENKI YA MAENDELEO AfDB

Waziri wa Fedha wa Tanzania, ambaye pia ni Gavana wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb), na Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha, ambaye pia ni Gavana Mbadala (alternating Governor) wa Benki hiyo, Dkt. Natu El-maamry Mwamba, wameshiriki-uchaguzi wa Rais Mpya wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), ambapo Bodi ya Magavana ya Benki hiyo ilimchagua kwa kura nyingi, Dkt. Sidi Quld Tah (Raia wa Mauritania), kuwa Rais Mteule mpya wa Benki hiyo, uchaguzi uliofanyika tarehe 29 Mei 2025, katika Hoteli ya Sofitel Ivoire, Jijini Abidjan nchini Côte D'ivoire, ambaye anachukua nafasi ya Rais wa Benki hiyo aliyemaliza muda wake, Dkt. Akinumwi Adesina.





Dkt. Tah, Waziri wa zamani wa Fedha wa Mauritania, ameshinda kwa wastani wa asilimia 76.18 ya kura zote zilizopigwa, raundi ya tatu ya mchuano huo.




Alikuwa akiwania nafasi hiyo na wagombea wengine wanne akiwemo Bw. Amadou Hott (Senegal), Samuel Maimbo (Zambia) Abbas Mahamat Tolli (Chad) na mwanamke pekee katika kinyang'anyiro hicho, Bi. Swazi Bajabulile Tshabalala kutoka Afrika Kusini.

Dkt. Ould Tah alianza kazi yake kama mtaalamu katika Benki ya Maendeleo na Biashara ya Mauritania (BMDC) kati ya mwaka 1984 hadi 1986, kisha akafanya kazi kama mchambuzi wa masuala ya kifedha katika Tume ya Usalama wa Chakula mwaka 1986. Aliteuliwa kuwa Meneja wa Utawala na Fedha katika Halmashauri ya Jiji la Nouakchott, Nchini Mauritania mwaka 1987. Kuanzia mwaka 1988 hadi 1996, alihudumu kama Mshauri wa Mkurugenzi Mkuu na pia Mkurugenzi wa Idara ya Ukaguzi wa Ndani katika Mamlaka ya Bandari ya Nouakchott.

Kati ya mwaka 1996 hadi 1999, alifanya kazi kama mchambuzi wa kifedha katika Mamlaka ya Kiarabu ya Kilimo, Uwekezaji na Maendeleo (AAAID) yenye makao yake mjini Khartoum, Sudan Kaskazini. Kuanzia mwaka 1999 hadi 2006, Dkt. Ould Tah alihudumu kama Afisa wa Uhamasishaji Uwekezaji na baadaye kama Msaidizi wa Kiufundi wa Rais wa Benki ya Maendeleo ya Kiislamu (IsDB).

Dkt. Ould Tah aliwahi kuwa mshauri wa Rais na baadaye wa Waziri Mkuu wa Mauritania kati ya mwaka 2006 hadi 2008. Mnamo Julai 2008, aliteuliwa kuwa Waziri wa Uchumi na Fedha. Kuanzia mwaka huo huo, alihudumu kama Waziri wa Masuala ya Kiuchumi na Maendeleo hadi alipoteuliwa kuwa Mkurugenzi Mkuu wa Benki ya Kiarabu ya Maendeleo ya Kiuchumi Afrika. (BADEA)





# DKT. NCHEMBA ANA KWA ANA NA MKURUGENZI WA BENKI YA DBSA

Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb), ameishukuru Benki ya Maendeleo ya Afrika Kusini (DBSA), kwa kushiriki katika ujenzi wa Reli ya Kisasa (SGR), mradi ambao ni muhimu kwa uchumi wa Tanzania na nchi jirani zitakazonufaika na mnyororo wa thamani wa mradi huo wa kikanda.

Mhe. Dkt. Nchemba alisema hayo alipokutana na kufanya mazungumzo na Mkurugenzi Mtendaji wa Benki hiyo, Bi. Buitumelo Mosako, kando ya Mikutano ya Mwaka ya Bodi ya Magavana wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) iliyofanyika, Abidjan nchini Ivory Coast.

*Bi. Boitumelo Mosako, kutokana na umuhimu wa mradi huu, nachukua fursa hii tena kuiomba benki yako iendelee kuunga mkono utekelezaji wa kipande cha 6 na 7 ya Reli ya Kisasa (SGR), ambavyo upatikanaji wake wa fedha za kutekeleza vipande hivyo unasimamiwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB)*

Aliongeza kuwa Tanzania imefungua milango ya ushiriki wa sekta binafsi katika kuendesha mradi huo wa kimkakati ikiwemo uwekezaji wa mabewa na vichwa vya treni na kutoa wito kwa wawekezaji kuchangamkia fursa hiyo.

Aidha, Mhe. Dkt. Nchemba aliishukuru Benki hiyo kwa kuonesha utayari wake wa kutaka kuwekeza zaidi katika maendeleo ya Tanzania katika sekta za elimu, maji, afya, ujenzi wa miundombinu pamoja na kilimo.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya DBSA, Bi. Buitumelo Mosako, alisema kuwa milango ya ushirikiano na Tanzania iko wazi na kwamba Benki yak eina subiri kukamilika kwa Dira ya Maendeleo ya Taifa ya 2050 ili waweze kuangalia maeneo ya kushirikiana.

Alisisitiza kuwa Benki yake iko tayari kuwekeza zaidi Tanzania katika kusaidia miradi ya kimkakati na kijamii katika sekta za m aji, afya, nishati, uchumi wa kidigitali, ujenzi wa makazi ya gharama nafuu na ujenzi wamiundombinu mbalimbali.

Kikao hicho kilihudhuriwa pia na Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha, Dkt. Natu El-maamry Mwamba, Katibu Msaidizi wa Baraza la Mawaziri, Bw. Fidelis Mkatte, Kamishna wa Fedha za Nje, Wizara ya Fedha, Bw. Rished Bade, Kamishna wa Idara ya Usimamizi wa Deni la Serikali, Wizara ya Fedha, Bw. Japhet Justine, pamoja na maafisa wengine waandamizi kutoka Serikali ya Tanzania.












ZOOM LENS EF-S 15-85mm 1:3.5-5.6 IS USM
KAMERA
YETU



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akiteta jambo na Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Nchemba, walipoungana na Rais wa Benki ya Maendeleo ya Afrika ( African Development Bank Group - AfDB), Dkt. Dr. Akinwumi Adesina, kutembelea na kukagua miradi miwili ya kimkakati iliyofadhiliwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) ukiwemo ujenzi wa barabara ya mzunguko wa nje ya Jiji la Dodoma (Dodoma outer ring road) yenye urefu wa kilomita 112.3, katika eneo la Mtumba, Jijini Dodoma, pamoja na Mradi wa Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Msalato Jijini Dodoma, unaohusisha njia ya kuruka na kutua ndege (runway) jengo la abiria, jengo la kuongozea ndege pamoja na Miundombinu mengine.



Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba Madelu (Mb) (kushoto), akiwa na Rais wa Benki ya Maendeleo ya Afrika ( African Development Bank Group - AfDB), Dkt. Akinwumi Adesina, wakati wa tukio la kumtunuku Rais huyo, Shahada ya Heshima ya Uzamivu (Honoris Causa), iliyotolewa na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam , kwa kutambua mchango wake mkubwa katika maendeleo ya Afrika katika zama za sasa.



Katibu Mkuu Wizara ya Fedha, Dkt. Natu El-maamry Mwamba akiagana na Kiongozi Mwakilishi wa Benki ya Dunia, Bi. Abha Prasad, baada ya kumalizika kwa kikao kazi kuhusu ushirikiano wa kimaendeleo kati ya Tanzania na Benki hiyo, kikao hicho kilifanyika katika Ofisi za Wizara ya Fedha, Treasury Square, jijini Dodoma.



*Waziri wa Fedha Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb), akiwa katika picha ya pamoja na Wakuu wa Idara na Vitengo wa Wizara hiyo, baada ya kufungua Mkutano wa 38 wa Baraza la Wafanyakazi wa Wizara ya Fedha, uliowakutanisha Wajumbe kutoka Makao Makuu ya Wizara, Wakuu wa Hazina Ndogo na Wahakikimali kutoka Mikoa yote ya Tanzania Bara, Katika Kituo cha Mikutano cha APC-Mbweni, Dar es Salaam.*



*Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba Madelu (Mb) (kushoto), akiagana na Mkurugenzi Mtendaji wa Kundi la Kwanza la Nchi za Afrika wa Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF), Bw. Adran Ubisse, baada ya kukutana na kufanya mazungumzo kando ya Mikutano ya Majira ya Kipupwe ya IMF na Benki ya Dunia, Jijini Washington D.C, nchini Marekani, ambapo pamoja na mambo mengine walijadiliana masuala mbalimbali ya ushirikiano katika ya Tanzania na Shirika hilo.*



*Naibu Waziri wa Fedha Mhe. Hamad Hassan Chande (Mb), akisalimiana na Bw. Chu Kun, Kansela wa Uchumi na Biashara wa Ubalozi wa China nchini Tanzania, alipowasili kwa ajili ya kumpokea Mhe. Tang Wenhong (hayupo pichani), Naibu Waziri wa Biashara wa Jamhuri ya Watu wa China, katika uwanja wa ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere jijini Dar es Salaam kwa ziara ya kikazi yenye lengo la kukuza ushirikiano wa kiuchumi na kidiplomasia kati ya Tanzania na China.*



*Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Fedha, Bw. Elijah Mwandumbya, akiagana na Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya ALSTOM, nchini Tanzania, inayojihusisha na uwekezaji katika ujenzi na uendeshaji wa miundombinu ya reli duniani, Bi. Kefilwe Mothupi, baada ya kumalizika kwa kikao chao kilichofanyika Ofisi za Wizara ya Fedha, Treasury Square, jijini Dodoma.*



*Kamishna wa Bajeti, Wizara ya Fedha, Bw. Meshack Anyingisye, akiagana na Balozi wa Czech Nairobi, Mhe. Nicol Adamcova', baada ya kukamilika kwa mazungumzo kati yao kuhusu utiaji saini wa Mkataba wa Kuondoa Utozaji Kodi Mara Mbili kati ya nchi hizo mbili, ambao unatarajiwa kuweka mazingira ya kodi yanayotabirika ili kuvutia uwekezaji wa mitaji ya muda mrefu pamoja na kuondoa mzigo wa utozaji kodi mara mbili kwa wawekezaji wanaondesha shughuli zao kati ya nchi hizo mbili, jijini Dodoma.*



*Afisa Usimamizi wa Fedha Mwandamizi, Idara wa Uchambuzi wa Sera, Wizara ya Fedha, Bw. David Massawe, akitoa elimu kwa mkazi wa jiji la Dodoma, Bi. Zainabu Kyama, kuhusu huduma zinazotolewa na idara hiyo katika Banda la Wizara ya Fedha, wakati wa Maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma, yaliyo-fanyika katika viwanja vya Chinangali, jijini Dodoma.*

LIMETOLEWA NA
KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI
WIZARA YA FEDHA
MJI WA SERIKALI - MTUMBA
MTAA WA HAZINA
S.L.P 2802, 40468 DODOMA, TANZANIA

www.mof.go.tz

TOLEO LA NNE 2025
ISSN: 3108-8597

ISSN 3108-8597
9 773108 859009